# Nipashe

Alhamisi Novemba 10, 2022 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581125

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

The Guardian digital nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710

LIKE & FOLLOW US





UKURASA 13


SUPA JACKPOT

TZS.1,048,875,802

KWA TZS. 1000 TU!

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!

SportPesa.CO.TZ

PIGA *150*87#




**Wabunge** washangaa bil. 54/- kutengewa vijiji vilivyofutwa

UKURASA 3



# Tundu Lissu, wadau wataka uwajibikaji ajali ndege Victoria

UKURASA 2

## YALIYOMO

UKURASA WA 5

**KCB YAJA NA 'FURSA SUKUK' UWEKEZAJI KWA WATANZANIA**

BENKI ya KCB Tanzania imezindua hati fungani ijulikanayo 'Fursa Sukuk' inayotoa fursa...

## Samia na El-Sisi waweka mikakati biashara, uwekezaji

UKURASA 3

## HALI ILIVYYO...



Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango akisikiliza maelezo kwa Ofisa Mtendaji Mkuu wa DAWASA, Mhandisi Crypian Luhemeja (kulia), alipotembelea mitambo ya uzalishaji maji ya Ruvu Chini, Pwani jana. **PICHA: OMR**




Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya KCB, Cosmas Kimario (kulia), akizindua hati fungani ya Fursa Sukuk na viongozi mbalimbali akiwamo Mkurugenzi wa Usimamizi wa Sekta ya Fedha wa Benki Kuu ya Tanzania (BoT), Sadati Musa (wa pili kulia) na Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana (CMSA), Nicodemus Mkama (wa nne kushoto), jijini Dar es Salaam jana. Wengine ni viongozi wa Bodi ya Shariah na Mkuu wa Masoko, Uhusiano na Mawasiliano Christine Manyenye (wa tatu kushoto). **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## PSSSF yatoa mwongozo malipo ya watumishi walioghushi vyeti

UKURASA 2

**MICHEZO** SIMBA YASHINDWA KUISHUSHA YANGA UK.32 **KABWELA** UK.7



Rais Samia Suluhu Hassan, akiagana na Rais wa Misri, Abdel Fattah El-Sisi, baada ya mazungumzo yao kwenye Ofisi ya Rais El-Sisi katika Mji wa Sharm El Sheikh, nchini Misri jana. **PICHA: IKULU**

# Tundu Lissu, wadau wataka uwajibikaji ajali ya ndege

**Na Beatrice Shayo**

MAKAMU Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), amesema Idara ya Maafa katika Ofisi ya Waziri Mkuu, inapaswa kuwajibika kutokana na kushindwa kuokoa abiria waliopata ajali mita 500 kutoka uwanja wa ndege wa Bukoba, mkoani Kagera.

Pia wadau wametaka hatua madhubuti kuchukuliwa kwa walioshindwa kuwajibika kuokoa watu na kwamba kwa kuacha hali hiyo kuendelea, matukio yataendelea kutokea na watu watapoteza maisha.

Akizungumza juzi kwenye mjadala mtandaoni, Lissu ambaye yuko Ubelgiji, alisema matukio mengi yametokea nchini lakini hakuna uwajibikaji wala kutafuta suluhisho la kudumu.

Alisema ni muhimu kwa Rais Samia Suluhu Hassan kueleza umma hatua zilizochukuliwa dhidi ya wateule walioshindwa kuwajibika kwenye nafasi zao licha ya kulipwa mishahara, posho na fedha zingine ambazo ni kodi za wananchi wanaoteketea kwenye ajali.

"Mwaka 2011 meli ya MV Spice ilizama karibu na Kisiwa cha Nungwi, Zanzibar iliua mamia. Mwaka 2012 meli ya MV Skagit ilizama ikaua mamia na miaka minne iliyopita MV Nyerere ilizama Ziwa Victoria ikaua mamia.

"Katika matukio yote hayo tumejifunza nini? Ukweli ni kwamba kama nchi hatuna utaratibu wowote wa uongozi. Kama kuna idara na watu wanalipwa mishahara wafanye hizo kazi, wanalipwa bila kufanya kazi yoyote. Kama kuna walipewa dhamana wasimamie majanga haya, wameshindwa kazi," alisema.

Kwa mujibu wa Lissu, serikali imeshindwa kuhakikisha kunakuwa na mfumo utakaozuia au utakaopunguza ajali na ikitokea zikatokea basi kunakuwa na hatua za haraka kuokoa maisha ya watu.

"Ndege inaanguka mita 500 kutoka pa kukimbilia. Uwanja wa ndege unatakiwa uwe na gari la kuzima moto. Jeshi la Polisi hakuna wanachofanya. Watu wamekufa kwa sababu ya uzembe si kwa sababu Mungu amewaita. Tusiposema kwa majina sahihi tutaendelea kujificha kwenye Bwana ametoa na Bwana ametwaa," alisema.

"Nimesoma mahali kuwa Waziri Mkuu, (Kassim) Majaliwa alikuwa Bukoba alipelekwa kwa helkopta iliyokuwa inaonyesha matokeo ya sensa. Nilichosoma ni helikopta maalum kwa uokozi na kutembeza viongozi na haikwenda kuokoa watu haraka,' aliongeza.

Naye mwanaharakati Tito Magoti, alisema Waziri Mkuu anapaswa kuwajibika kwa kuwa idara ya maafa iliyoko chini ya ofisi yake imeshindwa kuwajibika kuokoa watu licha ya kwamba ingewezekana.

Mchangiaji mmoja kwenye mjadala wa mtandaoni aliyejitambulisha kwa jina la Jordan alisema watu waliteseka kwa muda mrefu huku viongozi wakieleza umma kuwa wanawasiliana na rubani na wanapeleka msaada, kumbe hali haikuwa hivyo kwa kuwa wavuvi ndio waliokoa watu.

Nalo Jukwa la Wahariri Tanzania (TEF), limependekeza wavuvi wote waandaliwe kama Jeshi la Akiba la Uokozi kama ilivyo kwa mgambo kwenye Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania, kutokana na ushiriki wao kwenye matukio mengi.

"Wakati tukiendelea na maombolezo, tunaisihi serikali ifanye uwekezaji mkubwa katika mafunzo na vifaa vya uokoaji zikiwamo helikopta kwani hakuna mwenye uhakika kuwa ajali ya Precision majini ndiyo itakuwa ya mwisho," ilisema taarifa hiyo.


## NGOMENI ENTERPRISES

**NOTISI YA SIKU KUMI NA NNE (14) YA KULIPA DENI NA TANGAZO LA MNADA WA HADHARA.**

Kwa idhini na mamlaka tuliyopewa na crdb bank makao makuu Dar es salaam tunatoa notisi ya siku kumi na nne (14) tu ili uweze kulipa deni lako lote unalodaiwa Pamoja na gharama za dalali. Kukaidi au kushindwa kulipa deni hilo tutauza dhamana uliyoweka bank kwa mnada wa hadhara kama inavyoonesha kwenye jedwari hapo chini.

| S/N | JINA LA MDAIWA | DHAMANA / MAHALI | TAREHE/ MUDA |
|---|---|---|---|
| 1. | KENNEDY CHRISTOSIA MATHEMU | NYUMBA YA MAKAZI ILIYOPO ENEO LA UKONGA , MTAA WAMADAFU WILAYA YA ILALA. | 5.12.2022 KUANZIA SAA 4:00 ASUBUHI KUENDELEA |
| 2. | KASMERY YONATHAN MGWABATI | NYUMBA YA MAKAZI YENYE PLOT NO. 942, BLOCK "B" KIZINGA – KIVULE, WILAYA YA ILALA. | 5.12.2022 KUANZIA SAA 4:00 ASUBUHI NAKUENDELEA |
| 3. | THAMES VALLEY COMPANYLIMITED | NYUMBA YA MAKAZI YENYE PLOTNO 126, BLOCK 24 ILIYOPO BUNJU – WILAYA YA KINONDONI | 26.11.2022 KUANZIA SAA 5:00ASUBUHI NA KUENDELEA. |
| 4. | JUDITH JOSEPH TIMOTHY KESSY | NYUMBA YA MAKAZI ILIYOPO BUNJU 'B' KATA YA MABWEPANDEDAR ES SALAAM. | 26.11.2022 KUANZIA SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| 5. | EVELYNE STEPHEN MHINA | NYUMBA YA MAKAZI ILIYOPOWAZO - MADALE WILAYA YA KINONDONI. | 28.11.2022 KUANZIA SAA 4:00 ASUBUHI NAKUENDELEA |
| 6. | BENALD ESTARICO SAMAJE | NYUMBA YA MAKAZI ILIYOPO WAZO WILAYA YA KINONDONI. | 28.11.2022 KUANZIA SAA 5:00 ASUBUHI NAKUENDELEA. |
| 7. | BEATRICE GERAZI MTAKYAWA | NYUMBA YA MAKAZI ILIYOPO MTAA WA MSINGWA KATA YA MSIGANI WILAYA YA UBUNGO | 3.12.2022 KUANZIA SAA 4:00 ASUBUHI NAKUENDELEA. |
| 8. | ISMAIL JUMA MNANGO | NYUMBA YA MAKAZI ILIYOPO SAKU MKONDOGWA MBAGALA | 6.12.2022 KUANZIA SAA 4:00 ASUBUHI NAKUENDELEA. |
| 9. | ALOYCE PASCAL JAVA | NYUMBA YA MAKAZI ILIYOPO MIVUMONI DAR ES SALAAM | 8.12.2022 KUANZIA SAA 4:00 ASUBUHI NAKUENDELEA |
| 10 | ANGELA THEOBARD BASINDA | NYUMBA YA MAKAZI ILIYOPO GOBA KUNGURU WILAYA YA UBUNGO | 8.12.2022 KUANZIA SAA 4:00 ASUBUHI NAKUENDELEA |
| 11 | HASHIMU BAKARI ATHUMANI | NYUMBA YA MAKAZI ILIYOPOPLOT 37 BLOCK J, AREA E, MANISPAA YA DODOMA. | 06.12.2022, KUANZIASAA 4 ASUBUHI NA KUENDELEA |

**MASHARTI YA MNADA.**

1. Dhamana itauzwa kama zilivyo.
2. Mnunuzi atakayeshinda atalipa malipo ya awali ya asilimia 25 ya bei itakayofikiwa siku ya mnada na asilimia 75 atalipa ndani ya siku 14.
3. Mnunuzi atakayeshindwa kumalizia salio la asilimia 75 katika muda uliopangwa hapo juu, hatarudishiwa fedha alizolipa awali na mnada utarudiwa siku nyingine itakayopangwa.
4. Gharama zote za kubadilisha hati miliki, kutwaa nyuma na gharama nyinginezo zitakuwa juu ya mnunuzi.
5. Wateja wote mnakaribishwa kuona na kukagua nyumba muda wote isipokuwa usiku.

**MAWASILIANO:**
**CRDB BANK PLC, HEAD QUARTER. NGOMENI ENTERPRISES, DSM. SIMU: 0719974916/ 0784252048**

1171139702



Dev Recoveries Ltd

NIC Life House 4th Floor, Wing C
Sokoine Drive/Ohio Street
P. O. Box 6100
Dar es Salaam
Tel:+255 22 2112045
Fax: +255 22 2112045

## TANGAZO LA MNADA WA HADHARA

Kampuni ya DEV RECOVERIES LIMITED, kwa idhini waliyopewa na Benki ya ICBTL, watauza kwa njia ya mnada wa hadhara wa mali za mdaiwa kama dhamana ya mkopo. Hivyo basi, ifahamike kuwa utakapopita muda wa siku na nne (14) tangu kushikiliwa kwa dhamana husika, zitauzwa kwa njia ya mnada.Mali zipo chini ya Benki ya ICBTL kama dhamana ya mkopo dhidi ya KINGDOM TRADERS LIMITED na ALIABID RAZAHUSSEIN MAMDANI.

MCHANGANUO WA DHAMANA ITAKAYOUZWA

| NA. | MAJINA YA WADAIWA | MAHALI ILIPO DHAMANA NA TAARIFA ZAKE | TAREHE,MUDA NA MAHALI MNADA UTAKAPOFANYIKA |
|---|---|---|---|
| 1. | 1. M/S KINGDOM TRADERS LIMITED ( Mkopaji) 2. ALIABID RAZAHUSSEIN MAMDANI (Dhamana) S.L.P 20719, DAR ES SALAAM | Jengo la biashara/makazi yenye hati nambari.186002/7, Kitalu na. 1671/208, Ghorofa ya 2, Barabara ya Morogoro, Wilaya ya Ilala, Dar es salaam. | 26/11/2022 kuanzia saa 6 mchana na kuendelea. Mahali Barabara ya Morogoro, Kitalu na. 1671/208, Ghorofa ya 2. |

Mnada utafanyika tarehe 26 Novemba, 2022.Wanunuzi wenye nia na uwezo wanakaribishwa kuja kukagua mali kwa vigezo na masharti yafuatayo:

1. Mali/dhamana itauzwa katika hali ilivyo.
2. Mnunuzi atalazimika kulipa malipo ya 25% ya fedha taslimu papo hapo baada ya nyundo ya dalali kutua na salio la 75% liwe limelipwa ndani ya siku 14 tokea siku yam nada.
3. Gharama zozote ikiwemo ya kubadilisha taarifa za umiliki na nyinginezo zitakuwa juu ya mnunuzi.
4. Ukaguzi wa dhamana unaruhusiwa kufanyika siku yoyote kuanzia saa 3.00 asubuhi baada ya kutoka kwa tangazo hili.
5. Kwa taarifa zaidi, wasiliana nasi kwa namba : 0788438640/0712390460

2171141002


# PSSSF yatoa mwongozo malipo walioghushi vyeti

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

MKURUGENZI Mkuu wa Mfuko wa Pensheni kwa Watumishi wa Umma (PSSSF), Hosea Kashimba, amewataka watumishi wote walioondolewa kwenye ajira kwa kosa la kughushi vyeti, kwenda kwa waajiri wao ili kujaza fomu maalum kwa ajili ya malipo ya michango yao.

Pia amesema mfuko huo unakadiria kulipa zaidi ya watu 9,000 na Sh. bilioni 20 kutokana na malipo ya fedha walizochangia kwenye mifuko ya hifadhi ya jamii katika kipindi chao cha utumishi wa umma.

Kashimba alisema jana kuwa maelekezo ya serikali yaliyotolewa na Rais Samia Suluhu Hassan, yalielekeza kuwa watu wote walioondolewa kwenye utumishi wa umma kwa kughushi vyeti waanze kulipwa fedha za michango yao Novemba Mosi, mwaka huu.

"Rais alielekeza watumishi hawa waliobainika kuwa na vyeti feki waanze kulipwa fedha zao za michango. Lakini kinachotakiwa hivi sasa kwa watu wote ambao walikutwa na sakata hili ni kwenda kwa waajiri wao wa mwisho ili kujaziwa fomu ambazo zitaletwa kwetu kwa ajili ya malipo.

"Badala ya kuja PSSSF, wanapaswa sasa kwenda kwa waajiri wao wa mwisho ili kujaziwa fomu hizo na kuzileta kwetu na sisi tutatoa kipaumbele kwao kwa kulipa ndani ya siku 60 tangu kuletwa kwa madai hayo," alisisitiza.

Aidha, alisema kabla ya kuunganishwa kwa mfuko huo mwaka 2018 walikuwa wanalipa pensheni kwa wastaafu Sh. bilioni 34 kwa mwezi.

"Baada ya kuunganishwa mifuko hii tumekuwa tukilipa pensheni kwa wastaafu Sh. bilioni 60 kwa mwezi na kila mwezi tunalipa wastaafu wapatao 150,000 na kila inapofika tarehe 25 ya kila mwezi tunahakikisha tumelipa," alisema.

Kuhusu mchango wa uwekezaji wa mfuko katika uchumi alisema PSSSF ni mdau mkubwa katika kuchangia maendeleo ya kiuchumi. Alisema mfuko huo umewekeza Sh. trilioni 4.5 katika hatifungani za serikali.

"Pamoja na kuleta faida ya uwekezaji kwa mfuko kupitia riba na uwekezaji huu unauwezesha mfuko kutekeleza majukumu yake ya msingi. Vilevile mfuko umewekeza zaidi ya Sh. bilioni 500 katika Soko la Hisa la Dar es Saalam kupitia kampuni mbalimbali zilizoorodheshwa.

Pia alisema uwekezaji huo mkubwa wa mfuko unasaidia kukuza soko la mitaji nchini na kuchochea uchumi na maendeleo ya mwananchi mmoja mmoja.

Hata hivyo, alisema zaidi ya Sh. bilioni 400 zimewekezwa katika amana za muda (Fixed Deposit) katika benki mbalimbali nchini.

Msemaji Mkuu wa Serikali, Gerson Msigwa, aliwataka watumishi wa umma kuhakikisha kuwa wanafuatilia mara kwa mara waajiri wao kama wanawasilisha michango yao kwenye mifuko ya hifadhi ya jamii.

"Wafanyakazi ni jukumu lenu kuhakikisha kuwa mnafuatilia kama waajiri wenu wanapeleka michango yenu katika mifuko ya hifadhi ya jamii ili kusiwe na shida pale ambapo mtumishi akifika wakati wa kustaafu," alisema Msigwa.



Wananchi wakiangalia mabaki ya gari dogo lililoharibika vibaya baada ya kugongana na basi aina ya Coaster la kampuni ya Mangare, lililofeli breki na kuyagonga magari mengine matatu katika mteremko wa Iwambi, eneo la Mbalizi mkoani Mbeya jana na kusababisha vifo vya watu wawili ambao ni wanafunzi wawili wa kidato cha pili na wengine watatu kujeruhiwa. **Habari Uk. wa 5.** **PICHA: GRACE MWAKALINGA**

# Rais Samia, El-Sisi waweka mikakati biashara uwekezaji

**Na Mwandishi Maalum**

RAIS Samia Suluhu Hassan, amekutana na Rais wa Jamhuri ya Misri, Abdel Fattah El-Sisi, jana kwenye mji wa Sharm El Sheikh.

Katika mkutano huo, viongozi hao wamezungumzia masuala mbalimbali yanayohusu uhusiano na ushirikiano kati ya nchi hizo mbili hasa kuwapo kwa mikakati mahsusi ya kuongeza kasi ya biashara na uwekezaji.

Marais hao wamezungumzia ujenzi wa mradi wa kufua umeme wa Julius Nyerere unaojengwa na wakandarasi kutoka Misri na kuonyesha kuridhishwa na kasi ya ujenzi wa mradi huo uliofikia asilimia 77 mpaka sasa.

Vilevile, Rais Samia amemueleza Rais El-Sisi kwamba Tanzania ina mpango wa kuziba njia ya kuchepusha mto na kuanza kujaza maji kwenye bwawa hilo. Rais El-Sisi ameahidi kutuma ujumbe mzito katika tukio hilo muhimu.

Viongozi hao wawili wamesisitiza umuhimu wa kutekeleza mradi huo kwa ubora na viwango vya uhakika hata kama utachelewa nje ya muda uliotarajiwa hapo awali.

Pia Marais hao wamesisitiza kuwa timu ya wataalamu wa pande zote mbili wafanye kazi kwa karibu ili kutatua changamoto ndogondogo zinazojitokeza kwenye mradi huo.

Katika mkutano huo, Rais Samia aliongozana na Waziri wa Nishati, January Makamba, Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Dk. Stergomena Tax na Balozi wa Tanzania nchini Misri, Dk. Emmanuel Nchimbi.

# Wabunge washangaa bil. 54/- kutengewa vijiji vilivyofutwa

**Na Richard Makore,** DODOMA

BAADHI ya wabunge 'wamechafua hali ya hewa' bungeni na kusababisha mawaziri kusimama na kutaka kujitetea kutokana na hoja zilizogusa serikali.

Mbunge wa Makete (CCM), Festo Sanga alianza kuchafua hali ya hewa baada ya kusema kwamba serikali imetenga Sh. bilioni 54 kujenga miundombinu ya umwagiliaji katika vijiji 48 wilayani Mbarali wakati timu ya mawaziri wanane imevifuta na havipo.

Sanga aliyasema hayo jana bungeni jijini Dodoma wakati akichangia maoni yake kwenye Mpango wa Maendeleo wa Taifa na Mwongozo wa Maandalizi ya Bajeti wa mwaka 2023/2024.

Alisema fedha zimetengwa kupitia mikataba 15 ya kuwezesha kuanzisha umwagiliaji, huku akihoji nani atafaidika na miradi hiyo wakati tayari mawaziri wanane wamefuta vijiji hivyo.

Kwa mujibu wa Sanga, vijiji vilivyofutwa na serikali vilikuwa na kaya 100,000, ambazo zilikuwa zinazalisha tani 600,000 za mazao kwa mwaka pamoja na kujenga viwanda 30 vya kuchakata mazao hayo.

Alisema anashangaa kuona mawaziri wanane waliotembelea vijiji hivyo kuvifuta wakati ni serikali hiyo hiyo bila kushirikisha wananchi.

Wakati Sanga akiendelea kuchangia, alisimama Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba na kufafanua kwa kujitetea kuwa fedha zimetengwa kwa kuwa bado majadiliano baina ya wananchi na serikali yanaendelea ya ama kuvifuta au la.

Sanga alisema hakuna mawasiliano ndani ya serikali na kwamba kila wizara inafanya mipango yake bila kushirikisha mwenzake.

**ATAKA NAULI ZA ATCL ZISHUKE**

Wakati huo huo, Sanga aliomba kushuka kwa nauli za ndege katika Shirika la Ndege Nchini (ATCL), kwa kuwa zipo juu.

"Kwa sasa nauli hizi zipo juu, inaanzia kati ya Sh. 600,000 hadi Sh. 800,000 , hapa kulikuwa na shirika la ndege nauli yake ilikuwa Sh. 100,000 hadi Sh. 150,000, kwa nini hizi nauli zipo juu sana," alisema Sanga

Aidha, Sanga alitaka kuwekwa taa katika viwanja mbalimbali vya ndege hapa nchini ili ndege ziweze kufanya kazi saa 24, badala ya sasa ambapo zinalala saa 3 usiku.

"Yaani watu wakienda kulala na ndege nazo zinalala, kutokana na viwanja vya ndege kukosa taa za kuwezesha ndege kutua," alisema.

Mbunge mwingine aliyechafua hali ya hewa ni Mwita Waitara (CCM), alipokuwa akichangia mjadala huo na kusababisha Naibu Spika, Musa Azzan Zungu kumlazimisha akae chini.

Naibu Spika alichukua hatua hiyo baada ya Waitara kuchangia mpaka akapitiliza muda wake na alipoambiwa kukaa chini alikaidi na kuendelea kuzungumza mpaka alipozimiwa kipaza sauti.

Katika mchango wake, Waitara alisema watendaji wa serikali hawana mawasiliano na kwamba kila waziri anafanya kazi anavyojua yeye. Alisema licha mipango mingi ya serikali kuwa ya muda mfupi, lakini pia mawaziri hawana mawasiliano ya pamoja.

Aidha, alitaka serikali kuweka mkakati maalumu wa kuwezesha wananchi maskini kujikwamua kiuchumi kupitia mpango wa kunusuru kaya maskini unaotekelezwa na Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF).

Alisema serikali inatoa Sh. 34, 000 kwa mwezi kwa kaya maskini, kiasi ambacho alisema hakiwezi kumsaidia mtu huyo kujikwamua kiuchumi.

Baada ya kauli hiyo, Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Utawala Bora, Jenister Mhagama alifafanua kuwa fedha zilizotolewa kwa kaya 100 husaidia kujikwamua kiuchumi.

Akizungumza bungeni jijini Dodoma jana, Mbunge wa Kawe (CCM), Josephat Gwajima alisema serikali haina mipango ya muda mrefu inayolenga kuleta maendeleo.

Alisema nchi zote zilizofanikiwa kupiga hatua ya maendeleo ziliweka mipango mizuri ya maendeleo ambayo ni ya muda mrefu.

Alitoa mfano kuwa baada ya vita ya dunia kumalizika nchi za Ulaya zilikuwa maskini, lakini Marekani ikazisaidia kujenga uchumi wao na zikakubali kuweka mipango ya muda mrefu.

Gwajima alisema kuna miradi mikubwa inaendelea kujengwa hapa nchini, lakini hakuna mipango ya muda mrefu ya kuhakikisha inaleta maendeleo.

Alitoa mfano kuwa wakati serikali inajenga Bwawa la kuzalisha umeme la Mwalimu Nyerere, hakuna mpango wa muda mrefu wa kuhakikisha umeme utakaozalishwa unaingizwa katika gridi ya taifa.

Alisema hakuna miundombinu ya kusafirisha umeme na kuingiza kwenye gridi ya taifa na kwamba mipango mingi ya serikali imekuwa ni ya muda mfupi.

Gwajima alitoa mfano mwingine kuwa ujenzi wa Reli ya Kisasa (SGR), unaoendelea kwa ajili ya kusafirisha mizigo mingi kwenda mikoa mbalimbali nchini na nje ya nchi, lakini hakuna mpango wa kupanua bandari ya Dar es Salaam.

Alisema mizigo mingi inapokelewa bandarini kutoka nje ya nchi ambayo itasafirishwa kwenye reli ya SGR, lakini hakuna mpango wa muda mrefu wa kuipanua.

Kwa upande wake, Mbunge wa Muleba Kaskazini (CCM), Charles Mwijage alitaka wakaguzi wa hesabu za serikali katika ngazi za halmashauri, kufundishwa kukagua mifumo badala ya makaratasi.

Alisema kwa sasa wakaguzi wanatakiwa kupewa ujuzi ili kukagua mifumo ya mahesabu huku akiomba itungwe sheria itakayompa nguvu mkaguzi wa hesabu za serikali kuchukua hatua kwa aliyemkagua.


JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA NISHATI

MAMLAKA YA UDHIBITI WA HUDUMA ZA NISHATI NA MAJI (EWURA)

ewura
Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji
ISO 9001:2015 Certified

## TAARIFA KWA UMMA

**(Imetolewa chini ya kifungu Na.19 cha Sheria ya Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), Sura ya 414 ya Sheria za Tanzania na Kanuni Na. 21(4) ya Kanuni za Mafuta (Biashara ya Jumla, Uhifadhi, Reja Reja na Matumizi Binafsi), Gazeti la Serikali Toleo Na. 150 la 2022)**

TAARIFA inatolewa kwa umma kwamba Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) imepokea ombi la kubadili umiliki wa leseni na jina la kituo kama ifuatavyo:-

| | |
|---|---|
| **Jina la awali la kituo:** | **Milo Group Limited Petrol Station** |
| **Nambari Ya Leseni:** | **PRL-2020-082** |
| **Mahali Kituo Kilipo:** | **Kiwanja Na. 1421, Kitalu 'M', Eneo la Forest, Mkoa wa Mbeya** |
| **Jina Linalopendekezwa:** | **Njombe Filling Station** |
| **Mmiliki Wa Awali:** | **Milo Group Limited Petrol Station** |
| **Mmiliki Mpya:** | **Njombe Filling Station** |

Mtu yeyote mwenye maoni au pingamizi dhidi ya mabadiliko ya umiliki na majina ya leseni tajwa hapo juu, afanye hivyo kwa maandishi na kuwasilisha EWURA kwa anwani iliyotajwa hapa chini ndani ya siku kumi na nne toka tarehe ya tangazo hili.

**Mkurugenzi Mkuu,**
**Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji – EWURA**

117134002

# Hakimu wa pili kesi ya Zumaridi akataliwa

**Na Pelucy Yohana,** SAUT

WASHTAKIWA 84 katika kesi ya jinai na mshtakiwa namba moja, Diana Bundala maarufu 'mfalme Zumaridi' wameomba hakimu anayesikiliza kesi hiyo, Clescensia Mushi, kujiondoa wakidai ana upendeleo.

Kesi hiyo inayosikilizwa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Mkoa wa Mwanza, jana iliitwa kwa ajili ya kusomwa uamuzi wa pingamizi la upande wa utetezi katika kesi ndogo iliyoibuka kwenye kesi ya msingi.

Katika pingamizi hilo lenye madai ya kutilia shaka saini iliyowekwa kwenye maelezo ya mshtakiwa namba moja (Zumaridi), washtakiwa hao waliiomba mahakama kutopokea kielelezo hicho.

Akisoma uamuzi huo, Hakimu Mushi alisema, pingamizi la upande wa utetezi katika kesi ya msingi halina mashiko kwa kuwa upande huo ulishindwa kuwasilisha vielelezo walivyowahi kuiomba mahakama hiyo iagize wapewe kutoka Jeshi la Polisi.

Hakimu Clescensia alisema upande wa utetezi haukuweka pingamizi la kuendelea kudai vielelezo hivyo badala yake walighaili na kuleta mashahidi watatu kutoa ushahidi wao huku upande wa mashtaka ukileta shahidi mmoja, Sajini Robert, aliyedai kuchukua maelezo ya mshtakiwa huyo.

Hakimu Clescensia, alisema kati ya mashahidi watatu wa utetezi katika kesi ndogo, hakuna anayedai kushuhudia mshtakiwa namba moja akipigwa wakati wa mahojiano.

"Kutokana na sababu hizo mahakama imejiridhisha kuwa hoja za upande wa mashtaka zina mashiko hivyo pingamizi la upande wa utetezi limetupiliwa mbali na mahakama inaendelea kusikiliza ushahidi wa kesi ya msingi," alisema.

Baada ya hakimu kuamuru kesi hiyo iendelee, Sajini Robert, alipanda kizimbani kuendelea kutoa ushahidi kwenye kesi ya msingi, lakini Wakili wa Utetezi, Steven Kitale, alisimama na kudai wateja wao hawako tayari kuendelea na kesi hiyo.

Washtakiwa hao kupitia kwa Wakili Kitale walidai mahakama hiyo ina upendeleo na kuomba Hakimu Clescensia ajiondoe kusikiliza kesi hiyo ili kuondoa lawama.

Kitale alidai kutokana na wateja wake kutosomewa ushahidi walioutoa kwenye kesi ndogo ndani ya kesi ya msingi kama inavyoelekezwa kwenye Kifungu cha 210 (3) cha Sheria ya Mwenendo wa Mashauri ya Jinai (CPA) ya mwaka 2019, ni dhahiri hakimu huyo hatatenda haki kwa wateja wake.

Alidai kuwa wateja wake wanakosa imani na hakimu huyo kutokana na tabia yake ya kuchana karatasi wakati akirekodi mwenendo wa kesi hiyo bila kutoa taarifa kuwa ni nini kilichochanwa na nini kinaandikwa.

"Kutokana na tabia yako (hakimu) ya kuchana karatasi zaidi ya mara tatu wakati wateja wetu wakitoa ushahidi, wametilia shaka kuwa kuna uwekezano kukawa na upendeleo kwani hawakusomewa ushahidi walioutoa na ushahidi huo tayari umeshafungwa," alidai.

"Wakati unafunga ushahidi wa kesi ndogo niliiarifu mahakama kuwa utaratibu uliotumika kukusanya ushahidi umekiukwa kwani shahidi wa Jamhuri alisomewa maelezo ya ushahidi wake, lakini mashahidi wa utetezi hawakusomewa sasa kwanini haki iwe ya upande mmoja?" Alihoji.

Baada ya ukimya, Hakimu Clescensia alionekana kuchana karatasi nyingine na kuwafanya wafuatiliaji wa kesi hiyo kutazamana.

Hata hivyo, Mwendesha Mashtaka wa Serikali, Dorcas Akyoo, alipopewa nafasi kuzungumzia hoja zilizowasilishwa na washtakiwa, alidai pamoja na hoja hizo kuwa za kweli, hazina uzito wa kumfanya hakimu ajiondoe kwenye kesi.

Alidai jopo la mawakili wa utetezi ni sehemu ya maofisa wa mahakama walitakiwa kukumbusha mahakama hiyo kuwasomea wateja wao ushahidi walioutoa.

Baada ya kusikiliza mvutano huo wa kisheria kutoka pande mbili za kesi hiyo, Hakimu, Clescensia aliahirisha kesi hiyo hadi leo saa 3:00 asubuhi itakapoitwa kwa ajili ya uamuzi wa kujiondoa au kuendelea.

Katika kesi hiyo Zumaridi na wenzake 83 wanakabiliwa na shtaka la kufanya kusanyiko lisilo halali wanalodaiwa kulitenda Februari 23, mwaka huu katika mtaa wa Buguku Kata ya Buhongwa jijini Mwanza.




Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Usafiri wa Anga TCAA, Hamza Johari, akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam kuhusu ubora wa Uwanja wa Ndege wa Bukoba. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# TCAA yasema Uwanja Bukoba ni salama

**Na Romana Mallya**

SIKU tano baada ya ajali ya ndege ya Kampuni ya Precision Air kuanguka katika Ziwa Victoria, Bukoba mkoani Kagera, na kuwapo malalamiko ya uwanja wa Bukoba si salama, Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Usafiri wa Anga (TCAA), Hamza Johari, amesema kuwa uwanja huo ni salama.

Jumapili, wakati ndege hiyo ikitoka Dar es Salaam kwenda Mwanza kupitia Bukoba, ilianguka Ziwa Victoria na kusababisha vifo vya watu 19 na manusura 24.

Akizungumza na waandishi wa habari jana jijini Dar es Salaam, mkurugenzi huyo alisema ni wajibu wa TCAA kuliweka sawa suala hilo.

Baada ya ndege hiyo kuanguka, wadau mbalimbali wakiwamo marubani na wahandisi wa ndege, walizungumzia ugumu wanaoupata wakati wa kutua katika viwanja vya Arusha na Bukoba.

Johari alisema mamlaka hiyo ina jukumu la kutoa huduma ya uongozaji ndege kwa kuhakikisha anga la Tanzania liko salama wakati wote, vifaa vya kuongozea vimefungwa maeneo mbalimbali vikiwamo viwanja 14 ambavyo vina uwezo wa kutoa huduma hizo.

Alisisitiza kuwa mkataba wa Chicago una viambatisho 19 ambavyo kila kimoja lazima kitekelezwe kwa mujibu wa viwango vya kimataifa.

"Tanzania katika utekelezaji wa viwango vya kimataifa alama zake ni asilimia 69.7 na kimataifa ni asilimia 60," alisema.

"Habari zilizopo ni kwamba uwanja wa ndege wa Bukoba ni hatari, uwanja wa ndege ni hatarishi, kama Mkurugenzi Mkuu wa TCAA nina jukumu la kuweka hili sawa, vinginevyo tutapotosha umma na watu wataogopa kwenda na kuwanyima fursa watu wa Bukoba.

Alisema Kagera ni miongoni mwa viwanja vikongwe ambacho kilijengwa mwaka 1940 na Kampuni ya Precision ilianza kwenda huko tangu mwaka 1992 ikianza na ndege ya abiria saba.

"Mwaka 1996 waliongeza ndege ya abiria wanane pamoja na akiba ya abiria 11, mwaka 1998 wakaamua kupeleka ndege iliyobeba abiria 18 na mwaka 2008 aina hii ya ndege iliyopata ajali ndiyo ilianza kwenda Bukoba na sasa ni miaka 14. Kama uwanja huu ni hatari tungekuwa na mlolongo wa ajali kila siku.

"Ajali hii ninaweza kusema ni bahati mbaya kutokea, uwanja ungekuwa hatari tungekuwa na matukio mengi," alisema Johari.

Alisema Shirika la Ndege la Tanzania (ATCL) lilianza kupeleka ndege zake huko kutoka mwaka 1980 na liliendelea mpaka mwaka 1995 na mwaka 2017 waliendeleza safari hizo na sasa ni mwaka wa tano.

"Tusipoweka haya sawa tutanyima fursa Bukoba, Kiwanja cha Bukoba kina urefu wa mita 1,500 (sawa na kilometa 1.5) na upana wa mita 30 ambazo zina uwezo wa kuhudumia ndege zenye uzito wa tani 29.

"Ndege iliyopata ajali uzito wake ni tani 18.5, mita 1,165 au kilometa 1.165 ili aweze kuruka, kutua anahitaji mita 964 au kilometa moja," alisisitiza.

# Adaiwa kuua mkewe kwa kumnyonga

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

KASANA Masanja (25) mkazi wa Kijiji cha Kizungu Kata ya Lyamidati wilayani Shinyanga, amedaiwa kuuawa na mume wake, Hamis Katunduru (35), kwa kumnyonga shigo hadi kufariki dunia kisha kumfungia ndani na kuondoka.

Tukio hilo lilitokea juzi majira ya 4:00 asubuhi katika kijiji hicho na mtuhumiwa baada ya kutekeleza mauaji hayo alikimbilia kusikojulikana.

Kamanda wa Polisi mkoani Shinyanga, Janeth Magomi, akizungumza na Nipashe jana, alisema chanzo cha mauaji hayo ni wivu wa kimapenzi na kwamba mtuhumiwa tayari ametiwa mbaroni na wanaendelea na upelelezi ili hatua za kisheria zichukuliwe.

"Baada ya bwana huyu kutekeleza mauaji dhidi ya mke wake, alimfungia ndani kisha akaondoka. Lakini majirani zake walianza kuuliza mbona mwanamke mwenzao hawamwoni, ndipo wakaanza kufuatilia na kubainika ameuawa na mume wake na kufungiwa ndani," alisema Magomi.

Alisema polisi baada ya kupata taarifa, walifika eneo la tukio na kuvunja mlango na kumkuta mwanamke huyo akiwa ameuawa. Alisema taarifa za uchunguzi wa daktari wa serikali ilionyesha alinyongwa shingo hadi kufa.

Pia alisema mwili wa marehemu tayari umeshakabidhiwa kwa ndugu zake kwa ajili ya mazishi.

Diwani wa Lyamidati, Veronica Mabeja, alisema mwanamke huyo aliuawa na mume wake mwezi uliopita akafungiwa ndani, sababu waliukuta mwili wake ukiwa umeanza kuoza.

## HABARI KITAIFA

# KCB yaja na 'Fursa Sukuk' uwekezaji kwa Watanzania

**Na Mwandishi Wetu**

BENKI ya KCB Tanzania imezindua hati fungani ijulikanayo 'Fursa Sukuk' inayotoa fursa ya uwekezaji kwa Watanzania wote kwa mtaji wa 500,000 na kuendelea.

Kwa mujibu wa taarifa ya benki hiyo, Fursa Sukuk ni ya miaka mitatu, inafuata misingi ya Shariah na haitoi riba bali gawio la faida la asilimia 8.75 kwa mwaka.

Akizungumza wakati wa hafla ya uzinduzi, Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya KCB, Cosmas Kimario, alisema hatifungani hiyo imelenga kukusanya Sh. bilioni 10 ambazo zitatumika kuendeleza idara ya KCB Sahl inayotoa huduma za Kiislamu ikiwamo mikopo, huduma za miamala za benki na uwekezaji.

"Huu ni uwekezaji wa uhakika ambao unakupa gawio la faida la asilimia 8.75 kwa mwaka ambapo litatolewa mara nne kwa mwaka (mara moja kila robo mwaka). Mtu yeyote anaweza kununua hati fungani ya Fursa Sukuk kwa kiwango cha kuanzia Shilingi laki tano na kuendelea," alisema.

KCB Sahl Banking inatoa huduma za kifedha zisizotoza au kulipa riba kwa wateja mbalimbali ikiwamo watu binafsi, wafanyabiashara, kampuni ndogo na kubwa, vikundi, wazazi na watoto wao, wanafunzi na wafanyakazi.

Kimario aliwakaribisha Watanzania kuchangamkia fursa hiyo ya uwekezaji ambayo inampa mwekezaji thamani halisi ya pesa na kwa muda mfupi wa miaka mitatu.

"KCB ni benki kubwa zaidi Afrika Mashariki na Kati iliyoanzishwa mwaka 1896 visiwani Zanzibar. Baadaye ikaenda Kenya, Tanzania, Uganda, Sudani ya Kusini, Rwanda, Burundi, Ethiopia na hivi karibuni itafungua milango nchini Congo (DRC)," alisema.

Naye Mkuu wa Idara ya Huduma za Kibenki za Kiislaamu Sahl Banking, Amour Muro, alisema pesa zinazokusanywa kwa wawekezaji zitatumika katika biashara au huduma zinazofuata Shariah na faida inayopatikana hupewa kama gawio kwa wawekezaji.

"Faida itakayopatikana kupitia hizi huduma za KCB Sahl Banking itatolewa kama gawio kwa wawekezaji kupitia mkataba wa Mudharaba. Mkataba wa Mudharabah ni aina ya ushirikiano ambapo mteja anachangia mtaji na benki inasimamia hazina hiyo ili kuzalisha faida. Faida hugawanywa kati ya mteja na benki kwa uwiano uliokubaliwa awali," alisema.

Kadhalika, alisema Watanzania watakaohitaji kuwekeza watajaza fomu za maombi zinazopatikana katika matawi yote ya Benki ya KCB Tanzania na Benki ya CRDB Plc na ofisi za madalali na wafanyabiashara wa Soko la Hisa la Dar es Salaam waliopewa leseni na Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana (CMSA); au kutoka kwenye tovuti ya Benki ya KCB: https://tz.kcbgroup.com/kcb-sahl-tz/fursa-sukuk.

"Fursa Sukuk ofa iko wazi kuanzia Novemba 9, 2022 na itafungwa Desemba 5, 2022. Baada ya muda wa awali wa ofa, Fursa Sukuk itaorodheshwa kwenye Soko la Hisa la Dar es Salaam (DSE)," alisema.

Kadhalika, alisema maombi yatakamilika kwa kufanya malipo kwenye akaunti maalum ya Benki ya KCB Tanzania au kwa CRDB Bank Plc kupitia amana ya fedha kwenye tawi la benki au kupitia uhamishaji fedha wa kielektroniki au kupitia simu za mkononi.

# Watoto wa familia moja wapoteza maisha katika ajali magari matatu

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

WATOTO wawili wa familia moja, wamefariki dunia papo hapo na watu wengine watatu wamejeruhiwa katika ajali ambayo imehusisha basi dogo la abiria linalofanya safari zake kati ya Mbeya na Sumbawanga mkoani Rukwa.

Basi hilo lilifeli breki na kuyagonga magari mengine matatu kwenye mteremko wa Iwambi, barabara kuu ya Tanzania na Zambia (TANZAM), eneo la Mbalizi, nje kidogo ya Jiji la Mbeya.

Ajali hiyo ilitokea jana asubuhi baada ya basi hilo, mali ya kampuni ya Mangare, lenye namba za usajili T 601 DXC, kuyagonga magari mengine matatu na kusababisha vifo vya watoto hao.

Waliopoteza maisha katika ajali hiyo ni wanafunzi wa kidato cha pili ambao ni Maria Alute (15), mwanafunzi wa Shule ya Sekondari St. Francis na Halima Mwaijumba (14) mwanafunzi wa Shule ya Sekondari Panda Hill zote za mkoani Mbeya.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mbeya, Kamishna Msaidizi (ACP) Benjamin Kuzaga, alithibitisha kutokea kwa hali hiyo na kusema kuwa chanzo cha ajali ni mwendokasi wa dereva wa basi.

Alisema basi hilo likiwa kwenye mteremko wa Iwambi, liligonga gari lingine dogo lenye namba za usajili T 452 DHD aina ya Toyota Raum ambamo kulikuwa na watu watano.

Kamanda Kuzaga alisema ndani ya gari hilo, ndimo walikuwamo watoto hao wawili waliopoteza maisha, huku watu wengine watatu ambao ni wanamume na wanawake wawili wakijeruhiwa vibaya na kupelekwa katika Hospitali ya Rufani ya Kanda Mbeya kwa matibabu na kwamba hali zao si nzuri.

Mbali na Toyota Raum, Kuzaga alisema basi hilo pia liliyagonga magari mengine mawili ambayo ni lori lenye namba za usajili T 673 DMC aina ya Scania lenye tela namba T 362 DMG na lori lenye namba za usajili DAD 3981 likiwa na tela lenye namba ADF 75591 la nchini Zambia, lililokuwa limebeba madini aina ya salfa likitokea Dar es Salaam kwenda Zambia.


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI NA UCHUKUZI**
**TAASISI YA TEKNOLOJIA YA UJENZI**

**TANGAZO LA KOZI MAALUM YA MAOPARETA WA MITAMBO YA KAZI ZA UJENZI (GRADER OPERATOR' COURSE)**

**1. Utangulizi**
Taasisi ya Teknolojia ya Ujenzi "Institute of Construction Technology" (ICoT) ni Taasisi iliyo chini ya Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi yenye makao makuu katika Mkoa wa Morogoro kilipokuwa Chuo cha Ujenzi. Taasisi inawatangazia wananchi wote kuwa inatarajia kuendesha kozi maalum ya Maopareta wa Mitambo "Grader Operators' Course" ya Kazi za Ujenzi na Matengenezo ya Barabara kama ifuatavyo: -

| | Jina la kozi | Muda wa Mafunzo | Mafunzo yatafanyika |
|---|---|---|---|
| 1 | Kozi Maalum ya Maopareta wa Greda (Motor Grader Operators' Course). | Wiki Kumi (10) 28/11/2022 – 03/02/2023 | Mkoani Morogoro (ICoT – Morogoro) |

**2. Masomo Yatakayofundishwa**
Washiriki watajifunza moduli mbali mbali zinazohusu uendeshaji na utunzaji wa mitambo kama ifuatavyo: -
i. Kudumisha na kuweka usalama wa Mitambo na mahali pa kazi;
ii. Uendeshaji na Utumiaji wa Greda katika kazi za Ujenzi na Matengenezo ya Barabara;
iii. Kufanya Ukaguzi na Matengenezo ya awali ya Mitambo; na
iv. Kuweka kumbukumbu za Utunzaji wa Mitambo.

**3. Njia za Ufundishaji**
Mafunzo yatafanyika katika awamu mbili; awamu ya kwanza itakuwa ni mafunzo ya nadharia (Darasani) kwa muda wa wiki tatu (3) na awamu ya pili itakuwa ni mafunzo ya vitendo ('Site') kwa muda wa wiki saba (7).

**4. Lugha ya Mafunzo**
Lugha itakayo tumika katika kozi maalumu ya Maopareta wa Greda (Motor Grader Operators' Course) itakuwa ni ya mchanganyiko wa lugha ya Kiingereza na Kiswahili.

**5. Malengo ya Kozi**
Kozi hii inalenga kumpatia mshiriki uwezo na ujuzi wa kutumia Greda (Motor Grader) katika kufanya kazi za Ujenzi na matenegenzo ya Barabara na mwisho wa kozi tunatarajia Mshiriki atakuwa na uwezo wa: -
i. Kutumia Greda (Motor Grader) katika kufanya kazi ya ujenzi na matengenezo ya barabara;
ii. Kuhakiki usalama mahala pa kazi na utunzaji wa mtambo (Greda);
iii. Kufanya matengenezo ya awali pindi inapotokea hitilafu na kutunza kumbukumbu za mtambo - Greda.

**6. Sifa za Muombaji**
Muombaji anatakiwa kuwa na cheti cha kidato cha nne (Form IV) pamoja na leseni ya udereva.

**7. Gharama za Mafunzo**
Gharama za kushiriki mafunzo ni shilingi za Tanzania Milioni Moja (1,000,000) tu ambazo zitagharamia ada ya ushiriki, Vitini pamoja na vifaa vya mafunzo, chai ya asubuhi na chakula cha mchana. Mshiriki atajitegemea huduma nyingine zote muhimu ili kuweza kushiriki mafunzo kikamilifu.

**8. Namna ya Kutuma Maombi**
Kwa Tangazo hili, Wale wote wenye sifa zilizoanishwa hapo juu na watakao hitaji kupata mafunzo haya watume maombi yao katika Taasisi ya Teknolojia ya Ujenzi ICoT Makao Makuu – Morogoro au Tawi la Mbeya (ICoT – Mbeya) kwa kutumia anuani ya Posta, barua pepe, au kwa kupiga simu kwa namba zilizotolewa hapa chini. Malipo ya Ada yalipwe kabla ya wiki mbili ya kuanza kozi kwa kutumia 'control number' itakayotolewa kwa mshiriki yeyote atakayehitaji kupata mafunzo.

**WASILIANA NASI**
**MKUU WA TAASISI**

| Institute of Construction Technology ICoT, S.L.P 1957, MBEYA. | Institute of Construction Technology ICoT, S.L.P 963, MOROGORO. |
|---|---|
| Simu: 025 295 7484/5; 0764775354/0769317404 | Simu: 023- 2935229/023- 2935226; 0787059555 /0786384062/0629782068 |
| Nukushi: 025 295 7486 | Nukushi: 023-2935227 |
| Barua pepe: attimbeya@mow.go.tz, attimbeyafrica@gmail.com | Barua pepe: mwti@morogoro.net |

217141402

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Mkutano wa COP 27 unahusu Watanzania

**MKUTANO** wa 27 wa Nchi Wanachama wa Mkataba wa Kimataifa wa Mabadiliko ya Tabianchi (COP 27) ulioanza Novemba 6, mwaka huu, unaendelea jijini Sharmel El Sheik, nchini Misri, ukiwakutanisha wakuu wa nchi zaidi ya 100, mashirika na sekta binafsi 35,000 wakijadili namna ya kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi.

Mkutano huo unaofanyika kwa wiki mbili na kwa mara ya kwanza unafanyika barani Afrika, ajenda kuu ikiwa ni namna ya kuzisaidia nchi za Afrika kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi yaliyosababishwa na hewa ukaa inayozalishwa na nchi zinazoendelea.

Afrika ikiongozwa na mwenyekiti wake, Ephraim Shitima kutoka Zambia, imekwenda katika mkutano huo na ajenda sita muhimu za kulisaidia kukabiliana na athari hizo ikiwamo utekelezaji wa ahadi ya Dola za Kimarekani bilioni 100 za Mfuko wa kukabiliana na athari hizo, iliyotolewa mwaka 2009 na nchi zilizoendelea.

Nyingine ni uwezeshwaji wa teknolojia nafuu ili izisaidie nchi hizo kuendeleza miradi yenye uwezo wa kuhimili athari za mabadiliko ya tabianchi katika sekta mbalimbali ikiwamo kilimo, ufugaji, nishati ili zijikwamue kiuchumi kwa njia salama kwa mazingira.

Ajenda nyingine ni jitihada za kudhibiti ongezeko la joto ambalo sasa ni nyuzi 1.09 na kwa mujibu wa Jopo la Umoja wa Mataifa linaloundwa na serikali mbalimbali kuhusu mabadiliko ya tabianchi (IPCC), likifika nyuzi joto 1.5 hali itakuwa mbaya.

Vilevile kutajadiliwa uzalishwaji wa jesi joto, kwamba mpaka sasa ni kiasi gani cha gesi hiyo kinakwenda angani, madhara yake yakoje na namna ya kupunguza kasi ya uzalishaji ukizingatia kuwa kasi hiyo imeongezeka ukilinganisha na miaka 100 iliyopita.

Mkutano huo ni muhimu kwa Watanzania kwa kuwa madhara ya athari za mabadiliko ya tabianchi yanaendelea kuonekana nchini ikiwamo kutonyesha mvua kwa wakati na hata zinaponyesha zinakuwa chini au juu ya kiwango hali inayoathiri shughuli za kilimo.

Mfano hai ni uhaba wa maji unaendelea kulikumba taifa unaotokana na ukame uliosababishwa na kutonyesha kwa mvua za kutosha na kusababisha mgawo wa maji hasa kwa mikoa ya Dar es Salaam na Pwani.

Aidha, maeneo ya ukanda Kaskazini kunakosifika kwa shughuli za mifugo, kumeathirika kutokana na mifugo kufa kwa kukosa chakula na maji, wanyama wakali wakivamia makazi ya watu na kuwadhuru wakati wakitafuta maji ambayo pia ni matokeo ya athari hizo.

Aidha Kijiji cha Sindeni, kilichopo Halmashauri ya Wilaya ya Handeni wafugaji wanalazimika kuhamishia mifugo yao vijiji vya jirani kufuatia ukame uliosababisha upatikanaji wa majani na maji ya kulisha mifugo kuwa wa shida.


Tanzania kupitia Makubaliano ya Paris, iliweka Mikakati ya Kitaifa ya Kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi kufikia mwaka 2030 na utekelezaji wake utahitaji takribani Sh. trilioni 14.3, kutoka kwenye mfuko wa kukabiliana na athari hizo.

Moja ya mikakati ni kuzuia uzalishwaji wa hewa chafu kupitia uchumi kati ya asilimia 30 hadi 35 ifikapo mwaka 2030 pamoja na kuongeza matumizi ya vyanzo vya nishati mbadala kutoka mwaka 2015 hadi 2025.

Akihutubia katika mkutano huo Novemba 7, mwaka huu, Rais SamiaSuluhu Hassan, alisema nchi hiyo imedhamiria kuongeza matumizi ya vyanzo vya nishati mbadala kutoka asilimia 60 mwaka 2015 hadi asilimia 80 mwaka 2025 na kuhifadhi ekari milioni 48 za misitu ambayo ni 55 ya ardhi yote ya nchi.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji:** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253 676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# Jamii ishiriki vita ya kukomesha mauaji ya ndugu zetu wenye ualbino

Na Sabato Kasika

**HIVI** karibuni kumekuwapo na taarifa za watu wasiojulikana, wanaodaiwa kumuua Joseph Mathias (50), mwenye ulemavu wa ngozi, mkazi wa kijiji cha Ngula, kata ya Ngula, Wilaya ya Kwimba mkoani Mwanza.

Inadaiwa kuwa, watu hao wamvamia nyumbani kwake usiku wa kuamkia Novemba 2, mwaka huu na kumkata mkono wa kulia, kitendo kilichochangia damu kutoka kwa wingi, hata kusababisha kifo chake.

Vitendo hivyo ambavyo miaka ya nyuma vilishamiri, lakini serikali ikavidhibiti, vinataka kuanza kujirudia, hali inayosababisha watu wenye ulemavu huo kuishi maisha ya hofu kwa kutokuwa na uhakika kwa kuishi.

Nadhani ni vyema jamii sasa ikasimama kulaani vitendo hivyo na kushiriki katika vita ya kukomesha mauaji ya albino ikiwamo kuelimishana kuhusu ulemavu huo, pia kutoa taarifa za viashiria vya vitendo hivyo.

Katika tatizo hilo, jamii inatakiwa kukumbishana kuwa watu wenye ualbino ni sawa na wengine wote, wala ngozi yao haina uhusiano na jambo lolote, hivyo wasiwe wepesi kuamini hujuma za waganga wa kienyeji.

Baadhi ya waganga wa kienyeji wamekuwa wakituhumiwa kuwaagiza watu kuwadhuru binadamu wenzao, kwa ajili ya viungo hivyo, jambo ambalo kimsingi si jema katika jamii iliostaarabika.

Mauaji ya Joseph yaliwashtua wadau wa haki za binadamu, Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC) na Chama cha Watu Wenye Ualbino Tanzania (TAS), na kutoa tamko la kulaani mauaji hayo.

Ninaungana na wadau hao kwa kujitokeza hadharani kukimea mauaji hayo, kwani kwa mtu yeyote anayethamini utu wa mtu hawezi kuua binadamu mwenzake kutokana na ukweli kwamba uhai ni utajiri mkubwa kuliko mali.

Vyombo vya dola vinafanya sehemu yake katika kudhibiti mauaji hao, lakini jamii haina budi kushiriki kukamilifu katika vita hiyo, ili kusaidia kukomesha mauaji ya watu wasio na hatia.

Lakini, pamoja na hayo, watu wenye ulemavu huo hawana budi kuendelea kuchukua kila aina ya tahadhari, kwa ajili ya usalama wao ikiwamo kutoa taarifa kwenye vyombo vya dola wanapoona viashiria vya ukatili huo.

Viashiria hivyo, ni kumuona mtu katika maeneo yao wanayemtilia mashaka na kutoa taarifa kwa vyombo vya dola ili vifuatilie nyendo zake kujua kama ni raia mwema au ndio hao wanaotafuta watu wenye ualbino na kuwaua.

Wanaondekeza vitendo hivyo, ni vyema wakatambua kuwa hakuna njia ya mkato ya kupata mafanikio katika maisha, kwani wote ambao wanaamini katika kuua watu wenye ulemavu wa ngozi, ili wanufaike, wanakosea.

Mauaji ya wenye ulemavu wa ngozi, ni ukatili usio na mfano, hivyo suala la ulinzi wao lisiwe la serikali tu, bali jamii nzima inatakiwa kuhusika kwa kuzingatia kwamba umoja ni nguvu.

Ni muhimu pia, kuweka utaratibu wa kuwalinda wenye ulemavu wa ngozi dhidi ya tishio la kutekwa na kuuwawa. Elimu kwa umma ni muhimu. Wanaofanya matendo hayo wapo ndani ya jamii yetu.

Ikiwezekana, sote weanajamii tukajiwekea utaratibu wa malipo kwa wasamaria wema wanaotoa taarifa kuhusu wahusika wa viungo vya albino, huku watoa taarifa hao wakilindwa kwa ajili ya usalama wao.

Ninatambua kuwa, tatizo hilo ni la kisheria, lakini pia ni la imani za ushirikina na uchawi ndani ya jamii. Hivyo ni muhimu kuyakabili mambo haya mawili kwa ushirikiano, ili kusaidia wenye ulemavu huo kuishi kwa amani katika nchi yao.

Baadhi ya watu wenye ualbino, wamekuwa wakikabiliwa na tatizo la saratani ya ngozi, lakini wanaongezewa na lingine la kuwinda uhai wao kana kwamba hawana haki ya kuishi. Ukweli ni kwamba hilo halipendezi!

Ikumbukwe kuwa, dunia ilishaatenga siku Juni 13 ya kila mwaka kuwa ya maaadhimisho ya Siku ya Walemavu wa Ngozi Duniani (albino), hatua inayoonyesha jinsi jamii inavyotakiwa kuwathaminiwa kama binadamu wengine.

# NMB yapiga jeki kituo cha afya, shule

**Na Mwandishi Wetu**

SHULE ya Sekondari Doda na Kituo cha Afya cha Mkinga mkoani Tanga vimenufaika na msaada wenye thamani ya zaidi ya Shilingi milioni nane kutoka Benki ya NMB ikiwa ni moja ya sera ya benki hiyo kurejesha faida kwa jamii.

Shule hiyo imepokea msaada wa mabati 120 kwa ajili ya kuezeka majengo kadhaa katika shule hiyo huku Kituo cha Afya cha Mkinga kikipokea mashuka 100 pamoja na vitanda viwili vya kulazia wagonjwa.

Akizungumza katika hafla ya kukabidhi msaada huo, Meneja wa NMB Kanda ya Kaskazini, Dismas Prosper, alisema benki hiyo imekuwa ikitenga asilimia moja ya faida yake kwa ajili ya kurejesha kwa jamii huku ikiamini kuwa kupitia jamii hizo benki inapata faida inayojitengenezea, hivyo kurejesha kwa jamii ni jambo la muhimu sana kwao.

"Pamoja na makubwa yanayofanywa na serikali, sisi kama wadau tunao wajibu wa kuunga mkono juhudi hizi za maendeleo kwa kusaidia jamii kwani jamii hizi ndizo zimeifanya NMB kuwa hapa ilipo kuwa kubwa kuliko benki yoyote hapa nchini," alisema.

"Tulipopata maombi haya ya kuchangia maendeleo ya elimu na afya katika Wilaya ya Mkinga, tulifarijika na kuamua mara moja kuja kushirikiana nanyi ili kuwa chachu ya maendeleo ya sekta hizi muhimu kwa jamii yetu," aliongeza.

Akizungumza wakati wa kupokea misaada hiyo Mkuu wa Wilaya ya Mkinga, Kanali Maulid Surumbu, alipongeza NMB kwa kuendelea kuzikumbuka jamii zenye changamoto kwa kuwa kwa kufanya hivyo wanazidi kujiongezea imani kwa wateja jambo ambalo litazidi kuwafanya wapate faida kubwa zaidi.

Mkuu huyo wa wilaya huyo aliwasihi watumishi watakaosimamia vifaa hivyo kuhakikisha weledi katika matumizi unazingatiwa ili misaada hiyo ikatumike na watu wengi zaidi.

Mganga Mkuu wa Wilaya ya Mkinga, Dk. Joseph Ligola, alisema awali walipata changamoto ya kulaza wagonjwa katika kituo cha afya cha Mkinga kutokana na sababu ya upungufu wa vitanda lakini msaada kutoka NMB utapunguza tatizo hilo na wagonjwa watakuwa wakihudumiwa vyema.

# Kesi ya kupinga mikutano ya hadhara yakwama kusikilizwa

**Na Grace Gurisha**

KESI ya kikatiba iliyofunguliwa na Chama cha NCCR-Mageuzi ya kupinga zuio la mikutano ya hadhara ya vyama vya siasa, imeshindwa kusikilizwa kwa sababu mawakili wa jamhuri katika shauri hilo wapo Mahakama ya Afrika Mashariki kwenye kesi nyingine.

Kesi hiyo namba 27, 2021 iliyofunguliwa katika Mahakama Kuu, Masjala Kuu, Dar es Salaam inasikilizwa na jopo la majaji watatu Jaji John Mgetta, Jaji Leila Mgonya na Jaji Edwin Kakolaki.

Kutokana na hali hiyo, upande wa jamhuri uliomba ahirisho na kesi ikapangwa Novemba 29, 2022 kwa kusikilizwa mbele ya jopo hilo.

Pia, katika upande wa majaji, majaji wawili hawakuwepo mahakamani hapo kutokana na majukumu mengine. NCCR-Mageuzi imefungua kesi hiyo dhidi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali (AG), Inspekta Generali wa Polisi (IGP).

Mdaiwa mwingine katika kesi hiyo ni Kamanda wa Polisi wa Kanda Maalum ya Dar es Salaam (RPC), ambapo chama hicho kinaiomba Mahakama kuondoa zuio hilo wakidai ni kinyume cha sheria.

Pia NCCR -Mageuzi inaomba Mahakama ielekeze watu waliozuia Kikao cha Kamati Kuu mwaka 2021, kinyume cha sheria, walipe fidia ya gharama zilizotumika kukiandaa kikao hicho.



Mwongoza watalii wa Kampuni ya Afrika Miles Safari Co. Ltd, Serafino Lanzi (kulia), akitoa maelezo kuhusu wanavyohudumia wateja wanaotaka kufanya utalii wa ndani, katika maonyesho ya utalii karibu kusini 2022, yaliyofunguliwa mjini Iringa jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Tanzania, Norway zashirikiana kukabili tabianchi

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Dk. Selemani Jafo, jana alikutana na Waziri wa Mambo ya Nje na Maendeleo ya Kimataifa wa Norway, Anne Veathe Tvinnereim, jijini Sharm El Sheikh, nchini Misri na kujadili namna ya watakavyoshirikiana kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi.

Mazungumzo hayo yalifanyika katika banda la maonesho la Tanzania kwenye Mkutano wa Nchi Wanachama wa Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Mabadiliko ya Tabianchi unaoendelea nchini humo.

Katika mazungumzo yao, mawaziri hao walikubaliana kuendeleza ushirikiano katika masuala ya maendeleo, hususan kufadhili miradi ya hifadhi ya mazingira na ili kuisaidia nchi hiyo kuhimili mabadiliko ya tabianchi.

Dk. Jafo alisema Serikali ya Tanzania na Norway zimekuwa na ushirikiano wa muda mrefu katika sekta mbalimbali na kusisitiza kuwa kwa sasa ushirikiano wao wanaulekeza zaidi katika uhifadhi wa mazingira, ili kuisaidia nchi hiyo kukabiliana na athari zinazoendelea kuathiri Watanzania.

Aidha, aliishukuru serikali ya Norway kwa kuendelea kuwashika mkono katika mambo mbalimbali kiuchumi kwa Tanzania, kuwa nchi hiyo iko tayari kushirikiana na serikali hiyo kwa maslahi mapana ya nchi na maendeleo ya Taifa kwa ujumla.

Alisisitiza kuwa ajenda ya mabadiliko ya tabianchi ni changamoto kubwa duniani na inahitaji ushirikiano na ufadhili wa nchi zilizoendelea na zinazoendelea, ili kutimiza mipango ya kitaifa ya kukabiliana na athari hizo kupitia makubaliano ya Paris.

Waziri wa Mambo ya Nje na Maendeleo ya Kimataifa wa Norway, Anne Tvinnereim, alisema Norway itaendelea kushirikiana na kufadhili miradi ya mabadiliko ya tabianchi nchini Tanzania kwa lengo la kusaidia wananchi walio katika hatari kubwa ya kuathiriwa na athari hizo.

## KABWELA



# Nyati yajenga kituo cha daladala Kigamboni

**Na Frank Monyo**

KAMPUNI ya Saruji ya Nyati imekabidhi Kituo cha Daladala wilayani Kigamboni kilichogharimu Sh. milioni 46 kwa Mkuu wa Wilaya hiyo, Fatma Nyangasa.

Akizungumza wakati wa kukabidhi kituo hicho jana, Mkurugenzi Mkuu Mtendaji wa Kampuni ya Nyati, Biswajeet Mallik alisema dhamira ya kampuni hiyo ni kuhakikisha kampuni yake inaunga mkono serikali katika kusogeza huduma kwa wananchi.

Mallik alisema mbali na kusaidia kutengeneza kituo hicho, pia wamekuwa wakisaidia katika sekta za afya, elimu na miundombinu.

"Katika Sekta ya Afya tumesaidia ujenzi wa Kituo cha Afya Kimbiji, na kwa upande wa elimu tumekarabati madarasa katika Shule ya Golani na Shule ya Sekondari Kimbiji pia tumesaidia saruji katika ujenzi wa Ofisi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) Kigamboni".

Akizungumzia miundombinu ambayo wanatoa huduma, mkurugenzi huyo alisema saruji ya kampuni hiyo inatumika katika ujenzi wa Mradi wa Reli ya Kisasa (SGR) pamoja na ujenzi wa mradi wa Bwawa la Kufua Umeme wa Maji la Julius Nyerere (JNHPP-MW2115) kwenye Bonde la Mto Rufiji.

Mkuu wa Wilaya ya Kigamboni, Fatma Nyangasa akizungumza baada ya kukabidhiwa kituo hicho, alitaka kituo hicho kiwe fursa kwa wakazi wa Kigamboni kujiletea maendeleo ya mtu mmoja mmoja na taifa kwa ujumla.

"Sasa Nyati Cement wametusaidia hapa, tunakaribisha na tunawaomba wadau wengine, tutaendelea kuwapitia na kuwatafuta waendelee kushirikiana nasi, ili waweze kuendeleza miradi hii kwa manufaa ya wananchi wetu na kwa manufaa ya wana Kigamboni.

"Stendi yetu tumeipokea, tunashukuru na tutaendelea kuiangalia kwa jicho la kipekee, kwa Manispaa hili jambo lipo mikononi mwenu manispaa kuiangalia na kuhakikisha kwamba inafanya kazi vizuri, wekeni utaratibu mzuri na uangalizi mzuri ili kuwapo utaratibu mzuri kwa maendeleo ya wana Kgamboni." aliagiza.

Aliongeza kuwa Wilaya ya Kigamboni ipo tayari kushirikiana na wadau wote, ili kuhakikisha wanapata mabadiliko chanya ya haraka na yanayoleta maendeleo yenye tija kiuchumi na kijamii kwa wananchi wa Kigamboni.

Alitoa maelekezo kwa Manispaa ya Kigamboni kutumia mapato ya ndani kuhakikisha inaboresha eneo la stendi hiyo ili kufikia malengo ya kuwa na stendi kubwa Kigamboni.

Alisema anaamini itakuwa stendi ya kipekee kwa Kigamboni na washirikiane mpaka eneo hilo la stendi lianze kufanya kazi kwa ufanisi.

Aliongeza kuwa uongozi wa madereva wa daladala wanapaswa kusimamia utaratibu wa matumizi ya stendi hiyo watumie wale waliopewa kibali.

"Tutaweka utaratibu mzuri kama tulivyoshauriwa ili kuwabana wale ambao hawatakuja hapa, kwa sababu eneo linalotumika kwa sasa sio eneo rasmi kwa ajili ya stendi, eneo lile tunataka tuwaachie wenye eneo lao ili na wao waendelee na uwekezaji mwingine," alisema.

Ofisa Mfawidhi wa Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA), Rahim Kondo alisema wameshaanza kutengeneza kibali cha kuanzia katika stendi hiyo ambayo imekabidhiwa.

"Tunaamini kwa kuwapo hii miundombinu kutawezesha magari kufanya kazi vizuri, hivyo lazima washirikiane kupanga utaratibu mzuri. Pia tunawaomba wamiliki na madereva wa magari wachukulie kwa uzito mabadiliko yatakayowekwa ili kuweza kuifanya stendi hiyo kukidhi vigezo vyake," alielekeza.

Diwani na Naibu Meya wa Manispaa ya Kigamboni, Stephano Waryoba aliishukuru Kampuni ya Nyati kwa kutengeneza stendi kwenye kata yake kwa ajili ya kurahisisha usafiri kwa wakazi wa kata hiyo na watumiaji wa stendi hiyo kwa ujumla.



Madaktari Bingwa wa Upasuaji Ubongo na Mishipa ya Fahamu wa Hospitali ya Taifa Muhimbili- Mloganzila, Dk. Raymond Makundi (kulia) na Dk. Alvin Miranda (katikati), pamoja na mtaalamu kutoka Marekani, Prof. Dilantha Ellegala (kushoto), wakifanya upasuaji mkubwa wa kuondoa uvimbe kwenye tezi ya Pituitari kwa kupitia pua bila kupasua fuvu la kichwa, hospitalini hapo, mkoani Dar es Salaam jana ambapo upasuaji huo ulitumia muda wa takribani saa nne. **PICHA: MNH**

## Madiwani walia na panya waharibifu

**Na Hamisi Nasri,** MASASI

MADIWANI wa Halmashauri ya Masasi wameiomba serikali kuwasaidia wananchi kukabiliana na panya waharibifu wa mazao ambao wanaongezeka kwa kasi.

Wakizungumza wakati wa kikao cha Baraza la Madiwani hivi karibuni, walisema uwapo wa panya hao unatishia uwepo wa baa la njaa, ikiwa hatua hazitachukuliwa kwa haraka.

Wakizungumza kwenye kikao hicho, madiwani hao walisema hali ya mashamba ya wakulima kwenye kata zao kwa sasa sio mzuri kwa sababu ya kuwapo kwa mlipuko wa makundi ya panya waharibifu wa mazao ambao wamevamia mashamba ya wakulima na kula mazao yanayoendelea kupandwa.

Walisema iwapo serikali haitachukua hatua stahiki za kuwadhibiti panya hao wakulima hawatafanikiwa kuvuna chochote kutoka kwenye mashamba.

Diwani wa Lupaso, Douglas Mkapa, alisema kata hiyo ni miongoni mwa zile zilizokumbwa na mlipuko wa panya hawaribifu wa mazao shambani na kwamba tayari mazao mengi yaliyokuwa yamepandwa kwenye mashamba yameharibiwa na panya hao.

Alisema tayari uongozi wa kata umeshatoa taarifa ngazi ya wilaya kuomba kupatiwa msaada wa kuchukua hatua za kuwadhibiti panya hao ili kunusuru hali ya mazao ya wakulima na kwamba kama hatua hazitachukuliwa kuna uwezekano mkubwa wa kukumbukwa na baa la njaa.

"Tunaiomba serikali kutupatia sumu ya kuwaua panya hawa kwani hali ni tete kwenye mashamba ya wakulima kwa sehemu kubwa tayari mazao ya wakulima yameshaharibiwa panya hawa wapo takribani wilaya nzima kwa sasa tunaomba hatua za haraka zichukuliwe ili kudhibiti panya hawa," alisema Mkapa.

Naye Diwani wa Mijerejere, Radhamani Pole, alisema wakulima wanapoteza mazao yao huku hawajui nini cha kufanya kukabili hali hiyo.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Masasi ambaye ni Diwani wa Mpeta, Ibrahimu Chiputula, alimwomba Mkuu wa Wilaya ya Masasi, Claudia Kitta, kuchukua hatua za haraka kudhibiti panya hao.

## Familia zenye mapacha kupewa msaada kuadhimisha siku yao

**Na Sabato Kasika**

TAASISI isiyo ya kiserikali Eden Twins Foundation, inayohudumia familia zenye watoto mapacha zisizo na uwezo, inatarajia kusheherekea Siku ya Mapacha kwa kutembelea familia hizo na kuzipa msaada wa hali na mali.

Mwenyekiti wa taasisi hiyo, Diana Mbena, aliliambia gazeti hili jijini Dar es Salaam jana, kuwa Siku ya Mapacha ni Novemba 11 ya kila mwaka, na wanaichukulia ni ya kipekee, kwa mara ya kwanza waliadhimisha, mwaka jana.

"Mwaka huu tunataka tofauti, badala ya maadhimisho, kwa kukusanya watu uwanjani, tutatembelea baadhi ya familia zenye watoto hao ambazo hazina uwezo kiuchumi na kuzisaidia chochote," alisema Diana.

Aliomba wadau mbalimbali waungane naye kwa hali na mali, ili aweze kutimiza lengo lake la kusaidia familia hizo, katika mikoa ya Dar es Salaam na Pwani kwa kuzipa chakula, mavazi na huduma nyingine.

"Ukifuatilia sana utagundua kuwa familia nyingi zenye watoto mapacha ni zile zilizo na uwezo mdogo kiuchumi, hali inayosababisha zishindwe kuwahudumia kuanzia matibabu, lishe na hata mavazi," alisema.

Alisema mazingira hayo ndio yaliyomsukuma kuanzisha taasisi hiyo kwa lengo la kuhamasisha jamii kutambua vikwazo hivyo, ili ikiwezekana, kuwapo na ushirikiano katika kuvitatua.

"Haitakiwi kuishia kumpongeza mtu aliyejifungua mapacha, badala yake kinachotakiwa ni kuangalia mazingira na vikwazo anavyokutana navyo katika kuwahudumia watoto wake," alisema.

Diana alisema huo ndio ujumbe wake kwa jamii, hasa wakati huu wa Novemba 11 wa maadhimisho ya siku hiyo, na kwamba ipo haja ya kuwatambua kuwa nao ni kundi linalohitaji kusaidiwa.

"Lakini pia niiombe serikali iangalie uwezekano wa kuwapa bima, kwani kutegemea kwa watoto wadogo wanatibiwa bure, wengi wao hukosa matibabu wanapokwenda hospitali na kuambiwa hakuna dawa," alisema.

Alisema wakiwa na bima hata wakienda hospitali yoyote wanaweza kupata matibabu, na katika maisha, Mungu anaweza akampa mapacha mtu mwenye uwezo kiuchumi na asiye nao cha muhimu ni kufuatilia ili kujua wazazi au walezi wenye changamoto na kuwasaidia.

Alisema baadhi ya wanaume huwakimbia wake zao wanapojifungua mapacha, wakidai kuwa ni uchuro, na kusababisha wawe na hali ngumu ya maisha.

HABARI KITAIFA

# Waziri avunja ukimya uchangiaji elimu

**Na Joseph Mwendapole**

WAZIRI wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolph Mkenda, amesema ingawa serikali inatoa elimu bure, haijakataza wananchi kuendelea kuchangia maendeleo ya shule zao kwa hiari.

Prof. Mkenda aliyasema hayo juzi wakati wa ufunguzi wa nyumba sita za walimu katika Shule ya Msingi Msinune iliyoko Chalinze mkoani Pwani.

Nyumba hizo zimejengwa kwa ushirikiano baina ya Taasisi ya Flaviana Matata na Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA) kwa gharama ya Sh. milioni 150.

Alisema kama ilivyo kawaida ya watu kuchangia harusi na sherehe mbalimbali, basi wananchi wana wajibu wa kuona umuhimu wa kuchangia maendeleo ya elimu.

"Serikali kutoa elimu bure haimaanishi kwamba wananchi hawaruhusiwi kuchangia maendeleo ya shule kama ujenzi wa miundombinu na lishe ya wanafunzi. Mkikubaliana kwa hiari changieni," alisema.

**Miradi iliyofadhiliwa ni yenye thamani ya Sh. milioni 550 na katika mwaka wa fedha wa 2022/23 ufadhili wa miradi yenye thamani ya Sh. milioni 964.4 utatolewa.**

Pia alisema serikali inawahimiza wazazi kuchangia kwa hiari maendeleo ya shule lakini aliwahakikishia kwamba hakuna mwanafunzi yeyote atakayefukuzwa kwa kutokuchangia.

Sambamba na hilo, aliwataka Watanzania kujenga utamaduni wa kurudi kwenye shule walizosoma na kutoa michango ya kukarabati shule hizo ili zifanye vizuri kitaaluma kama wanavyochanga kwenye mambo mengine, zikiwamo harusi.

"Kama Flaviana anafanya shughuli zake nchi za nje lakini ameona umuhimu wa kuja kuchangia Shule ya Msingi Msinune kwa nini ninyi wakazi wa hapa mshindwe kuchangia? Serikali haijawakataza kuendelea na michango ya hiari kwa maendeleo ya watoto wenu," alisema.

"Kama tunavyofurahi na kushangilia timu zetu zinavyofanya vizuri kitaifa na kimataifa basi mtu ajisikie fahari kuona shule aliyosoma inafanya vizuri na ili shule ifanye vizuri kitaaluma lazima iwe na miundombinu mizuri na wanafunzi waishi kwenye mazingira rafiki shuleni na wapate chakula," alisema.

Waziri Mkenda alisema Rais Samia Suluhu Hassan anawahimiza viongozi wa serikali kufanya kazi na sekta binafsi, hivyo aliwaomba wadau wengine kujitokeza kushirikiana na serikali.

Mkurugenzi Mkuu wa TEA, Bahati Geuzye, alisema fedha zilizotolewa na Mfuko wa Elimu kwa ajili ya gharama za ujenzi wa mradi ni Sh. milioni 150 na Taasisi ya Flaviana Matata imechangia Sh. milioni 100 na Mfuko wa Elimu wa Taifa umechangia Sh. milioni 50.

Alisema tayari nyumba nne zimekamilika na nyumba mbili zimefikia hatua ya kupauliwa na kwamba TEA inaendelea kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Chalinze kuhakikisha nyumba hizo zinakamilika haraka ili zikabidhiwe rasmi kuwezesha walimu kupata makazi bora.

Alisema katika miaka matatu iliyopita yaani 2020/21 hadi 2022/23 mkoa wa Pwani umepata ufadhili wa miradi ya elimu yenye thamani ya Sh. bilioni 1.7 na katika mwaka wa fedha wa 2020/21 miradi iliyofadhiliwa ilikuwa yenye thamani ya Sh. milioni 695.

Katika mwaka wa fedha 2021/22, alisema miradi iliyofadhiliwa ni yenye thamani ya Sh. milioni 550 na katika mwaka wa fedha wa 2022/23 ufadhili wa miradi yenye thamani ya Sh. milioni 964.4 utatolewa.

Alisema miradi hiyo inatekelezwa katika halmashauri za wilaya ya Chalinze, Bagamoyo, Mkuranga, Kibiti, Rufiji na Mafia ikihusisha ujenzi wa nyumba za walimu, vyumba vya madarasa, matundu ya vyoo, mabweni na miundombinu kwa wanafunzi wenye mahitaji maalum.



Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolph Mkenda (katikati), akikata utepe kuzindua nyumba sita za walimu kwa Shule ya Msingi Msinune, Halmashauri ya Wilaya ya Chalinze, mkoani Pwani juzi, zilizojengwa kwa pamoja baina ya Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA) na Taasisi ya Flaviana Matata kwa Sh. milioni 150. Wengine ni Mkurugenzi Mkuu wa TEA, Bahati Geuzye (wa tatu kushoto) na Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Ridhiwan Kikwete (wa pili kulia). **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Waonywa visingizio ukusanyaji wa mapato

**Na Thobias Mwanakatwe,** IKUNGI

BARAZA la Madiwani la Halmashauri ya Wilaya ya Ikungi mkoani Singida limetaka watendaji kuacha kutoa visingizio visivyo na maana katika ukusanyaji wa mapato badala yake washirikiane na madiwani kufikia malengo yaliyowekwa na halmashauri.

Walisema hayo juzi kwenye kikao cha baraza hilo huku wakibainisha kuwa baadhi ya watendaji wamekuwa wakitoa visingizio vinavyosababisha kutofikiwa kwa malengo ya ukusanyaji wa mapato ambavyo vingi havina uhalisia wa kuwa sababu ya kushindwa kukusanya mapato.

Taarifa za ukusanyaji wa mapato kwa kila kata zilizosomwa na madiwani kwenye kikao hicho ambazo ziliandaliwa na watendaji wa kata na baadhi ya visingizio vilivyoelezwa ni pamoja na baadhi ya wafanyabiashara kusafirisha mazao usiku wakikwepa kulipa ushuru.

Alisema suala la ukusanyaji mapato liwe la kufa na kupona kwa kuhakikisha viongozi kuanzia ngazi za vijiji na kata wanasimamia na si kuruhusu visingizio visivyokuwa na tija.

Naye Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri, Justice Kijazi, alisema halmashauri inawategemea sana madiwani katika kufikia malengo ya ukusanyaji wa mapato kwa kuwa wao wapo kwenye vyanzo vya mapato.

"Mapato ya halmashauri ndiyo moyo wa halmashauri kwa hiyo waheshimiwa madiwani kwenye vikao vya Kamati za Maendeleo ya Kata (WDC) mtusaidia kuweka msisitizo katika suala la ukusanyaji mapato," alisema.

Kijazi alisema hata hivyo Halmashauri ya Wilaya ya Ikungi imepiga hatua kubwa katika suala la ukusanyaji mapato kwani katika kipindi cha miaka mitano iliyopita bajeti ya mapato ilikuwa Sh. milioni 900 tu lakini sasa bajeti imefikia zaidi ya Sh. bilioni mbili.

# Uchunguzi saratani sasa kufika vijijini

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

WATU 24,000 wanaoishi katika maeneo ya vijijini mkoani Morogoro, watafanyiwa uchunguzi wa bure wa awali wa viashiria vya saratani na Hospitali Rufani ya Good Samaritan Cancer(GSCH) iliyoko Kilombero ambayo ni ya kwanza Tanzania kwa kutoa huduma ya mionzi tiba.

Hospitali hiyo ambayo inashika pia nafasi ya tatu Afrika kwa kutoa huduma hiyo, imekusudia kuwafikia wananchi hao wa vijijini kutokana na wengi wao kushindwa kuzifikia huduma hizo kwa sababu ya ugumu wa maisha na gharama zake.

Akizungumza kwenye harambee ya kukusanya zaidi ya Sh. milioni 300, Bingwa wa Uchunguzi na Utambuzi wa Saratani, Dk. Salvatory Mlaga, alisema uchunguzi wa awali utahusisha saratani ya shingo ya kizazi, tezi dume na saratani ya matiti. Alisema zaidi ya watu 1,000 watakaobainika wataokolewa kwa kuanzishiwa huduma za matibabu kutokana na hospitali hiyo kuwa na vifaa tiba vya kisasa.

Dk. Mlaga alisema hospitali hiyo imeweka malengo yake katika mpango mkakati wa kupeleka huduma ya uchunguzi wa awali wa saratani katika ngazi ya vijiji kutokana na upungufu wa hospitali zinazotoa huduma hizo nchini, hivyo kusababisha ongezeko la wagonjwa wa saratani.

"Tunafahamu liko tatizo la wananchi kushindwa kuzifikia huduma za uchunguzi wa saratani kwa sababu hospitali ni chache na gharama za kuzifikia ni kubwa kutokana na ugumu wa maisha au sababu zingine za kijamii, hivyo tumeamua kuwafikia wananchi hasa wa vijijini," alisema Dk. Mlaga.

Naye Mkurugenzi Mtendaji wa GSCH, Father Shibin James, alisema hospitali hiyo ambayo iko chini ya Wamisionari wa Shirika la Huruma kwa kushirikiana na Kanisa Katoliki Jimbo la Ifakara, ina lengo la kusaidia kutoa uchunguzi na tiba kwa wagonjwa wa saratani na magonjwa mengine.

Alisema hospitali hiyo imekuwa ikifikiwa na wagonjwa ambao tayari saratani imekuwa imekomaa, hivyo wameona kuanza mpango huo wa kuwafanyia uchunguzi wa awali ili kupunguza watu wanaougua saratani.

Naye Mwenyekiti wa Chama cha Wafanyabiashara, Wenye Viwanda na Kilimo (TCCIA) Mkoa wa Morogoro, Mwadini Myanza, alisema hospitali hiyo iliwasilisha wazo hilo kwao na kama wadau, waliamua kushirikisha wafanyabiashara mbalimbali waliochangia katika harambee hiyo kusaidia uchunguzi wa awali wa saratani.

Akizungumza kwa niaba ya Mkuu wa Mkoa wa Morogoro, Fatuma Mwasa, katika harambee hiyo, Mkuu wa Wilaya ya Morogoro, Albert Msando, alisema serikali ya mkoa inatambua ukubwa wa tatizo la saratani na watu wengi hupoteza maisha kutokana na kuchelewa kufanyiwa uchunguzi wa awali ili kubainika kama kuna saratani.

Uwapo wa Hospitali hiyo kubwa ya kibingwa ya GSCH, alisema umeanza kuonyesha mafanikio kwa kutatua tatizo hilo si kwa Watanzania tu bali hata nje ya nchi kutokana na kutoa huduma kubwa kwa wagonjwa wanaotoka nchi mbalimbali zikiwamo Malawi na Zambia.

# Serikali yapiga marufuku walalamikaji kuwagharamia watuhumiwa kesi usafiri

BUNGE limeelezwa kuwa kitendo cha mlalamikaji kulazimishwa kugharamia usafirishaji wa mtuhumiwa au mahabusu kwenda na kurudi rumande ni kukiuka sheria na kanuni zilizoko.

Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Jumanne Sagini, alibainisha hayo jana bungeni alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Muleba Kaskazini (CCM), Charles Mwijage.

Mbunge huyo, katika swali lake, alihoji kwa nini katika tarafa ya Kamachumu mlalamikaji hulazimishwa kumgharamia mahabusu kwa kumsafirisha kwenda na kurudi rumande.

"Mwaka jana Oktoba, bibi yangu Juliana Gaisha aliitwa kituo cha polisi na kupelekwa mahakamani Kamachumu. Hakimu alimweleza mlalamikaji kwamba bibi huyu apandishwe pikipiki na mlalamikaji akalipa fedha. Bibi yangu na watu wawili wakafungwa mshikaki kwenye pikipiki wakaenda Muleba kufungwa magereza. Lini itaundwa tume ya kitaifa kuchunguza hili?" alihoji.

Sagini akijibu swali hilo, alisema kitendo hicho kinapaswa kuachwa mara moja huku akisema tukio hilo halihitaji kuundiwa tume.

"Kwa mujibu wa Sheria ya Polisi Sura ya 322 iliyofanyiwa marejeo mwaka 2002 na Kanuni 353 na 354 ya Kanuni za Jeshi la Polisi zinazosimamia watuhumiwa au mahabusu walioko kwenye vituo vya polisi, utaratibu wa kuwasafirisha watuhumiwa au mahabusu kwenda mahakamani hutekelezwa na Jeshi la Polisi," alisema.

Pia alisema jukumu la kuwasafirisha watuhumiwa au mahabusu kutoka rumande gerezani kwenda mahakamani ni jukumu la Jeshi la Magereza kwa mujibu wa Kifungu cha 75 cha Sheria ya Magereza Sura ya 58 ya mwaka 1967 iliyofanyiwa marejeo mwaka 2002.

"Wizara imefanya mawasiliano na wakuu wa vyombo vyetu, yaani Mkuu wa Jeshi la Polisi na Mkuu wa Jeshi la Magereza ili wawaelekeze wasaidizi wao ngazi za mikoa na wilaya kuzingatia sheria," alisema.




Habari na Augusta Njoji

## Masuala wenye ulemavu yawekewa mwongozo

SERIKALI imeingiza masuala ya kamati za watu wenye ulemavu kwenye mwongozo kabambe wa upangaji wa mipango na bajeti ya huduma za ustawi wa jamii kwenye halmashauri na utekelezaji wake utaanza mwaka ujao wa fedha.

Pia imesema itaendelea kufuatilia watendaji wa vijiji au mtaa ili kuhakikisha kamati hizo zinaanzishwa katika maeneo yao. Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Ajira, Vijana na wenye Ulemavu, Patrobas Katambi, alisema hayo jana bungeni alipokuwa akijibu swali la msingi la Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Stella Ikupa.

Katika swali lake, mbunge huyo alihoji ni mikoa mingapi, wilaya, vijiji na vitongoji ambavyo vimeunda kamati za watu wenye ulemavu.

Katambi alisema uundwaji wa kamati hizo ngazi ya mkoa, wilaya, vijiji na vitongoji ni kwa mujibu wa Sheria ya Watu wenye Ulemavu namba 9 ya mwaka 2010 kifungu cha 14 (1) ambacho kimeelezea juu ya uundwaji wa kamati za watu wenye ulemavu katika ngazi ya kijiji, mtaa, wilaya, mkoa pamoja na majukumu ya kila kamati.

Alisema serikali ya Tanzania imetekeleza kwa kiwango kikubwa uundwaji wa kamati hizo.

Alisema katika kuhakikisha na kufuatilia vijiji na mitaa yote inaunda kamati hizo serikali imeandaa mikakati mbalimbali ikiwamo kuingiza masuala hayo kwenye mwongozo huo.



Mbunge wa Segerea, Bonnah Kamoli, akichangia kuhusu mapendekezo ya mpango wa maendeleo wa Taifa unaokusudiwa kutekelezwa na serikali kwa mwaka wa fedha 2023/2024, kwenye kikao cha Bunge, jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

## Bilioni 13.1/- kuimarisha TAZARA

KATIKA mwaka fedha 2022/23, serikali imetenga Sh. bilioni 13.1 kwa ajili ya kuboresha miundombinu ya Mamlaka ya Reli ya Tanzania na Zambia (TAZARA).

Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Atupele Mwakibete, alisema hayo jana bungeni mjini hapo alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Njombe Mjini (CCM), Deodatus Mwanyika.

Katika swali lake, Mwanyika alihoji serikali ina mkakati gani wa kukarabati reli ya TAZARA.

Akijibu swali hilo, Mwakibete alisema serikali imeendelea kuchukua hatua mbalimbali katika kuboresha miundombinu ya reli hiyo na katika mwaka fedha 2022/23, Sh. bilioni 13.1 zimetengwa kwa ajili ya ununuzi wa mataruma ya mbao kwa ajili ya kufanya ukarabati madaraja 172 yaliyoko upande wa Tanzania.

Pia alisema ununuzi wa mtambo wa kisasa wa kushindilia kokoto kwenye reli na ununuzi wa mtambo wa kuvunjia kokoto kwa ajili ya kuongeza kokoto za aina mbalimbali zinazotumika katika kufanya matengenezo ya njia ya reli kati ya Dar es Salaam –Tunduma na Msolwa - Kidatu.

Aidha, alisema fedha hizo pia zitatumika kukarabati mabehewa 21 ya treni za abiria za Udzungwa na treni za abiria za mjini jijini Dar es Salaam.

## Kitengo chaundwa kusimamia afya kwa wazee

WIZARA ya Afya imesema katika kuimarisha huduma za afya kwa wazee, kwa mwaka huu, imepitishiwa muundo mpya wa kuanzisha kitengo ndani ya kurugenzi ya tiba inayoshughulika na huduma zao za utengamao na tiba shufaa.

Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu, alisema hayo bungeni jana alipokuwa akijibu maswali ya Mbunge wa Lushoto (CCM), Shaban Shekilindi.

Mbunge huyo alihoji serikali kwa nini isibadili mfumo kwa kuhakikisha wazee wanakuwa na bima za afya badala ya utaratibu wa sasa wa kutumia dirisha la wazee katika kupata huduma za afya.

"Kwa kuwa mfumo huu wa kutumia dirisha la wazee unaonyesha una upungufu mkubwa, je, serikali haioni kuwa ipo haja sasa ya kubadili mfumo huu na ikiwezekana wazee wapewe kadi za bima ya afya kuliko ilivyo sasa?

Akijibu maswali hayo, Waziri Ummy alisema bima ya afya kwa wote ndiyo mkombozi kwa wazee kupata huduma bora za afya.

Ummy alisema serikali inaendelea kuimarisha huduma za afya za wazee na kwa miaka mingi wazee wamekuwa wakipatiwa huduma mahsusi kwa kupitia madirisha maalum ya huduma za afya kwa wazee yaliyotengwa katika vituo vya kutolea huduma chini ya kitengo hicho, alisema uratibu wa huduma au afua mbalimbali za afya ya wazee utafanyika na maboresho ya huduma za afya kwa wazee yatapokelewa na kuchakatwa na kupatiwa majawabu kwa wakati.

# Mradi ufufuaji zao la kahawa wapata ruzuku

**Na Mwandishi Wetu,** SIHA

MRADI wa ufufuaji wa zao la kahawa katika Wilaya ya Siha, mkoani Kilimanjaro, umeanza kupata mafanikio chanya, baada ya Kampuni ya USADF ya Marekani kuipatia fedha za ruzuku zaidi ya Sh. milioni 200, Chama cha Msingi cha Ushirika cha Siha Kiyeyo.

Chama cha Msingi cha Ushirika cha Siha Kiyeyo chenye wakulima zaidi ya 1,000, USADF na ADC, vilitiliana sahihi jana, mkataba wa uendeshaji wa mradi huo unaolenga kuchochea ongezeko la uzalishaji wa kahawa.

**Hatutasita kuwachukulia hatua za kisheria, watu watakaofanya ubadhirifu wa fedha hizi zilizotolewa kwa lengo la kuboresha zao la kahawa, kupitia Siha Kiyeyo.**

Jana, Msimamizi wa Ruzuku za USAD-Tanzania, Eileen Mwakisese, baada ya kuingia makubaliano alisema wameifuata Siha Kiyeyo kuamsha ari ya uzalishaji wa zao hilo na kujenga uwezo kwa wakulima wa kahawa kurejesha imani ya kustawisha tena zao hilo lenye tija kubwa kiuchumi.

"Ruzuku hiyo itatumika kufanya mambo mbalimbali kama kutoa mafunzo ya kilimo bora cha kahawa ili liwe kwenye mnyororo wa thamani, kununua pikipiki za wataalamu na kununua guta, kwa ajili ya usafirishaji wa zao hilo," alisema.

Ruzuku hutafsiriwa kama pesa au mtaji aliopewa mtu binafsi, chama, taasisi au biashara kwa sababu maalum.

Kabla ya utiaji sahihi mkataba huo, Mkuu wa wilaya hiyo, Thomas Apson, ambaye aliwakilishwa na Ofisa Tarafa ya Siha Kaskazini, Asteria Alfred, alionya kuwa serikali itaweka nguvu katika usimamizi wa fedha hizo kwa kuzuia mchwa wanaopanga kutafuta ruzuku hiyo kwa kujinufaisha binafsi.

"Hatutasita kuwachukulia hatua za kisheria, watu watakaofanya ubadhirifu wa fedha hizi zilizotolewa kwa lengo la kuboresha zao la kahawa, kupitia Siha Kiyeyo.

"Naelekeza fedha hizi zitumiwe kwa malengo yaliyokusudiwa na si vinginevyo. Nimelazimika kusema hivyo kwa sababu kuna baadhi ya vyama vya msingi vya ushirika, vimejaa watu ambao si waaminifu na linapokuja suala la fedha, wao kazi yao ni kupiga tu."

Baada ya kutia saini makubaliano ya fedha hizo, Katibu wa Chama cha Msingi cha Ushirika wa Siha Kiyeyo, Victor Mmari, aliahidi kuusimamia na kufanya vizuri kwa mradi huo, huku akiwaomba wanachama kuzingatia ushauri wa wataalamu wa kilimo ili mazao yazalishwe kwa kiwango kinachotakiwa na kupata soko la kimataifa.

## 40% ya watoto wametelekezwa na wazazi wao

**Na Oscar Assenga,** TANGA

MKOA wa Tanga, unatajwa kuwa na asilimia 40 ya watoto waliotelekezwa na wazazi wao vijijini na kukimbilia mijini kutafuta riziki, huku wanaharakati wakieleza kuwa jambo hilo linachochea kasi ya ongezeko la matukio ya ukatili wa kijinsia.

Ofisa Uhamasishaji wa Jamii kupitia Mradi wa Vijana Balehe dhidi ya visa vya ukatili, Suleiman Msey, alisema kuwa utelekezaji huo wa watoto unaathiri familia nyingi za mkoa huo kwa sasa.

Msey alikuwa akizungumza jana katika Jiji la Tanga, wakati wa mdahalo wa wadau wa haki za binadamu, uliokuwa ukishajihishwa na kaulimbiu ya jukumu la vyombo vya habari katika ulinzi wa watoto na vijana balehe dhidi ya visa vya ukatili.

"Maeneo ya vijiji kuna visa vingi vya ukatili ambavyo vinachochewa na baadhi ya babu na bibi ambao wameachiwa kulea watoto, kutotambua sheria.

"Sasa tafiti zetu zinaonyesha kuwa wazazi, walezi kushindwa kutimiza wajibu wao wa malezi na kukimbia majukumu hayo, ndicho kiini cha ongezeko la ukatili.

"Huko vijijini, kuna watu tumebaini kwamba wanapokwenda kuchunga mbuzi, wanajaribu na wanapoonja kesho anajaribu kwa mwenzie. Jambo ambalo ni hatari kwao."

Kutokana na ongezeko hilo, Msey alimshauri Mkuu wa Mkoa wa Tanga, Omari Mgumba na Mkuu wa wilaya hiyo, Hashim Mgandilwa, kuanzisha operesheni maalumu za kuwatafuta watu wanaofanya vitendo vya ovyo ikiwamo ushoga.

Wakati wa ufunguzi wa mdahalo huo, Mkurugenzi wa Asasi ya Tanga Youth Talent Association (TAYOTA), George Bwire, alisema hali ya ukatili wa kijinsia kwa Jiji la Tanga hairidhishi kutokana watoto kufanyiwa vitendo vya ulawiti wakiwa na umri mdogo.

Alisema mdahalo huo unakwenda sambamba na kuwajengea uwezo waandishi wa habari kushiriki katika kutokomeza ukatili hapa nchini.

Alisema kabla ya kuanza kutekeleza mradi huo, walifanya utafiti na kupata taarifa za awali kuhusu hali ya ukatili Tanga. Shirika hilo limedai kuwa hali hairidhishi kutokana na watoto kufanyiwa ukatili wa hali ya juu.

Alisema wanaokumbana na mikasa hiyo ni kuanzia miaka minane mpaka 10 na wengine wanafanyiwa na ndugu zao wakiwamo baba wa kambo.




Mkuu wa Polisi Kikosi cha Usalama Barabarani Mkoa wa Arusha, SP Solomon Mwangamilo, akitoa elimu ya usalama barabarani kwa madereva wa vyombo vya moto katika kata ya Meserani, wilayani Monduli, mkoani Arusha juzi. **PICHA: WOINDE SHIZZA**

## Sheria Maktaba kurekebishwa kuendana na kasi utoaji huduma

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

SERIKALI inakuja na marekebisho ya Sheria ya Huduma za Maktaba ya Mwaka 1975 ili kuendana na kasi ya utoaji huduma hizo kitaifa na kimataifa kwa njia ya kielektroniki.

Mbali na kufumuliwa kwa sheria hiyo, pia imepanga kutengeneza Sera mpya ya Huduma za Maktaba nchini.

Akizungumza jana katika mafunzo ya siku tano yanayohusisha Wataalamu wa Maabara za Kisayansi kupitia Shirikisho la Maktaba na Vyuo vya Utafiti (COTUL), Mkurugenzi wa Bodi hiyo, Dk. Mboni Ruzegea, alisema sera hizo zikirekebishwa pamoja na sheria, itatoa wigo mpana wa kazi zinazofanywa na watunzi wa vitabu.

"Tunaamini kwamba mabadiliko hayo yanaweza kutoa taswira ya kutambua kazi nzuri zinazofanywa na watafiti, kutambulika zaidi kupitia maktaba za kielektroniki.

"Wanafuzi kuanzia ngazi za chini hadi vyuo vikuu wataweza kusoma mambo mbalimbali kupitia maktaba hizo, katika viganja vyao vya simu au kompyuta mtandao, sehemu yoyote watakapokuwa wakihitaji kujisomea vitabu au vitu mbalimbali vilivyotungwa na Watanzania na watunzi wengine kimataifa.

"Huduma za maktaba ni bure, lakini tukiungana kwa pamoja na vyuo vikuu mbalimbali, wasomi watasoma vitabu kupitia mfumo wa kielektroniki ambao ni rafiki kwa kila mtu na sheria hii ikirekebishwa pamoja na sera, tutafika mbali kupitia maktaba za kielektroniki."

Naye Kaimu Mkuu wa Chuo cha Uhasibu Arusha (IAA), Dk. Cairo Mwaitete, alisema endapo vyuo vikuu vikiungana kwa pamoja na mfumo huo wa kielektroniki ukianza kazi, watu mbalimbali watasoma vitabu ikiwamo utafiti wa wahadhiri na maprofesa na kupata ufumbuzi wa jambo husika.

Alisema endapo COTUL na Wizara ya Elimu zikiungana, gharama za uchapishaji vitabu zitapungua ikiwamo kila vyuo kuwa na maktaba za kisasa, ili kuongeza wanachuo, wanafunzi na watu mbalimbali kusoma vitabu kwa ajili ya manufaa yao.

Awali, Mkuu wa Wilaya ya Arumeru, Richard Ruyango, alisisitiza Watanzania kupenda kusoma vitabu, ili kujifunza mbinu mbalimbali za kimaisha ikiwamo wanafunzi na wanachuo katika vyuo mbalimbali.

Ruyango, alisema maabara hiyo ya kielektroniki, itasaidia watunzi wa vitabu kujulikana ndani na nje ya nchi, kutokana na utunzi wa vitabu vitakavyosomwa kwa njia ya kielektroniki.

# Wawili waliofariki ajali Precision Air kuzikwa leo

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

MIILI ya abiria wawili kati ya 19 waliofariki kwenye ajali ya ndege Precision Air mkoani Kagera imewasili mkoani hapo, kwa ajili ya maziko yatakayofanyika leo, Wilaya ya Arumeru.

Marehemu hao ni Aneth Kaaya na Zaituni Mohamed, ambao wamepokewa na Serikali ya Mkoa wa Arusha kwa kushirikiana na familia zao katika Hospitali ya Rufani ya Mount Meru na Hospitali ya Seliani.

Akizungumza katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Arusha Mount Meru, baada ya kupokea miili hiyo, Kaimu Mkuu wa Mkoa wa Arusha ambaye ni Mkuu wa Wilaya ya Arumeru, Richard Ruyango, alisema mwili wa Zaituni Mohamed, umehifadhiwa katika Hospitali ya Seliani, huku Aneth Kaaya ukihifadhiwa Hospitali ya Mount Meru.

**Tunaendelea kushukuru Mungu miili hiyo imefika salama ikiongozwa na Katibu wa Chama Cha Mapinduzi Kagera.**

"Tunaendelea kushukuru Mungu miili hiyo imefika salama ikiongozwa na Katibu wa Chama Cha Mapinduzi Kagera," alisema.

Naye Katibu wa CCM Mkoa wa Kagera, aliyeongoza miili hiyo kufika katika Mkoa wa Arusha, Christopher Pallangyo, alisema wamesafirisha miili mitatu na mmoja umeachwa Wilaya ya Kondoa mkoani Dodoma kwa ajili ya mazishi.

"Miili miwili ni hii ambayo ni ya dada zetu hivyo tunashukuru Mwenyezi Mungu tumesafiri salama kwani hatujapata tatizo lolote tukiwa njiani," alisema Pallangyo.

Kaka wa marehemu Aneth ambaye alikuwa anaenda ukweni kutambulishwa, Frank Lameck alishukuru serikali kwa kufanikisha mwili wa ndugu yao kufika nyumbani.

Aidha, alisema marehemu dada yake alikuwa anajishughulisha na biashara ya uuzaji wa duka la vipodozi Dar es Salaam.

"Kitu alichokuwa anakifuata Bukoba akijafikia lengo lake, lakini hayo yote ni mapenzi ya Mwenyezi Mungu na ikiwa tu tumewasiliana kwa njia ya jumbe za whatsapp tukitaniana tu kwa wiki mbili zilizopita kweli alikuwa ni mtu wa watu sana," alisema Lameck.



Mkuu wa Wilaya ya Simanjiro, mkoani Manyara, Dk. Suleiman Serera (wa pili kushoto), akiongoza kikao cha kamati ya ushauri cha wilaya (DCC), kilichofanyika juzi. Wengine ni Mwenyekiti wa CCM wa Wilaya hiyo, Kiria Laizer (kushoto), Mwenyekiti wa Halmashauri ya wilaya hiyo, Baraka Kanunga (kulia) na Kaimu Katibu Tawala wa Wilaya, Mussa Waziri. **PICHA: GIFT THADEY**

# Shinini asema ana deni kuwatumikia wanawake

**Na Cynthia Mwilolezi,** SIMANJIRO

MWENYEKITI wa Jumuiya ya Umoja wa Wanawake wa CCM Tanzania (UWT), Wilaya ya Simanjiro mkoani Manyara, Anna Shinini, amesema ana deni kubwa la kuwatumikia wanawake wa wilaya hiyo, waliomchagua kwa kura nyingi hivi karibuni.

Shinini aliyasema hayo jana wakati akizungumza kwenye kikao cha Baraza la Wanawake wa UWT wa wilaya hiyo kilichofanyika Mji Mdogo wa Orkesumet.

Alisema uchaguzi umeshafanyika na hakuna haja ya kuwa na kambi, anahitaji kuwalipa utumishi uliotukuka kwa kumpa heshima kubwa mno.

Aidha, alisema ana malengo makubwa ya kutumikia jumuiya hiyo, akishirikiana na wanawake wote, wanapaswa kujifunga mikanda katika kutumikia nafasi walizoziomba.

"Twendeni wote kwa pamoja na tukisema tukimbie tunapaswa kukimbia wote na tukisema tusimame, basi tusimame wote ila atakayebaki nyuma tutamuacha," alisema Shinini.

Kwa mujibu wa Shinini, hivi sasa wanawake wamepata moyo wa kuwatumikia wananchi, kwa kuwa Rais Samia Suluhu Hassan ni mwanamke wanapaswa kwenda naye sambamba.

"Hivi sasa tupo juu kupitia Rais Samia hivyo tusimwangushe na kumshusha chini tumuunge mkono kwa kutimiza wajibu wetu ipasavyo," alisema Shinini.

Pia alisema atawatumikia wanawake wa Simanjiro, kwa kuwa ameshaacha alama kwa wasichana kwa kuwasomesha na hivi sasa ni wasomi wakiwamo madaktari na wanasheria.

Mbunge wa Viti Maalum wa Mkoa wa Manyara, Regina Ndege, alimpongeza kwa kuchaguliwa kuwa Mwenyekiti wa UWT Wilaya ya Simanjiro.

Mwenyekiti wa Madiwani wa Viti Maalum wa Wilaya ya Simanjiro, Bahati Partison, alisema mwenyekiti huyo ni hazina ya uongozi, wanawake wanapaswa kumpa ushirikiano wa kutosha.

"Miaka ya nyuma nilipochaguliwa kuwa Mwenyekiti wa UWT wa Wilaya ya Simanjiro, kipindi hicho kati ya nafasi tatu nilizokuwa nazo, moja nilimchagua Shinini kuwa mjumbe wa kamati ya utekelezaji," alisema Bahati.

# Waridhia watumishi 2 kufukuzwa kazi utovu wa nidhamu

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

BARAZA la Madiwani Halmashauri ya Jiji la Arusha limeridhia kufukuzwa kazi kwa watumishi wawili kwa utovu wa nidhamu, huku mmoja akiamriwa kurudishwa kazini baada ya kubainika tuhuma zake hazina mashiko.

Watumishi waliofukuzwa kazi ni mlinzi wa jiji hilo, Zalgano Gabriel na Ofisa Mtendaji wa Mtaa wa Kambi ya Chupa na Sorenyi Kata ya Kimandolu Methew Jackson.

Mtumishi atakayerudishwa kazini baada ya kubainika tuhuma zake hazikuwa na ukweli ni mkusanya mapato wa jiji hilo, Jacob Joseph.

Akizungumza jana katika Baraza la Madiwani, Mstahiki Meya wa Jiji la Arusha, Maximilian Iranghe, alisema watumishi hao kabla ya kufukuzwa kazi walijadiliwa idara ya utumishi na baadaye Baraza lilijigeuza kama kamati na kutoa uamuzi huo.

Alisema ni vizuri watumishi wanapokuwa kazini, kuzingatia miiko ya kazi na kuepuka utoaji wa lugha zisizofaa kwa wananchi.

"Pia naomba tushirikiane wote na tupendane ili kuharakisha maendeleo kwa jiji letu kwa manufaa pia ya wananchi na taifa hili," alisema.

Alisema hatua hiyo imechukuliwa pia ili kutoa mafunzo kwa wengine wenye tabia za utovu wa nidhamu kazini.

Aidha, alitoa pole kwa waathirika wa ajali ya ndege ya Precision Air iliyotokea Novemba 6 na kusababisha vifo vya watu 19.

Pia alitoa pole kwa waganga wa ajali ya gari wilayani Koteto mkoani Manyara iliyosababisha vifo vya watu saba watumishi wa Halmashauri ya Kiteto.

Naye Mkurugenzi wa Jiji la Arusha Hargeney Chitukulo, alitoa pole kwa familia mbili tofauti zilizopoteza wapendwa wao kutokana na uzembe na lugha chafu za wauguzi.

Alisema hivi karibuni alipata taarifa za uwapo wa vifo vya wazazi wawili katika Kituo cha Afya Osunyai na Murieti kutokana na utovu wa nidhamu wauguzi wa vituo hivyo.

Chitukulo alitoa wito kwa watumishi wote wa maeneo ya umma kufanya kazi kwa wito na kuzingatia nidhamu kazini.

"Naelekeza ofisa utumishi na nafahamu kuna Chama cha Wauguzi shirikianeni ili kuchukua hatua zaidi dhidi ya waliohusika na matukio haya," alisema.

# ama

ALHAMISI NOVEMBA 10, 2022

AFYA NA MAZINGIRA



Ukurasa 14

**Ukuaji teknolojia elektroniki, utandawazi sasa unageuka shida kwa afya ya akili**



**Minamata, ugonjwa uliojificha ukiwanyemelea wachimba dhahabu wadogo waliopo Chunya**

Ukurasa 16

# Kampuni inayowekeza katika urafiki tabianchi

**Na Halfani Chusi**

MABADILIKO ya tabianchi, ni janga katika nchi nyingi, ikiwemo Tanzania inayokaribisha ushuhuda wa kuwa na maafa makubwa, ikiwamo kusababisha njaa, mafuriko pamoja na ukame.

Ni taifa linalohitaji watu wenye uthubutu kukabiliana na hali hiyo pindi linapotokea, na si suala la kuiachia serikali pekee, bali ushiriki wa wadau katika kukabiliana na hilo.

Hapo ndipo Kampuni ya Bia ya Serengeti (SBL), inaungana na serikali kukabili hilo ikipanda miti ambayo ni babu kubwa ya kupatikana mvua na kuondoa ukame, pia janga la njaa.

Mkurugenzi wa Mahusiano, John Wanyancha, katika mazungumzo yake na waandishi wa habari, anaanika wanavyoshiriki kupanda miti kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi.

Anasema kampuni yao inategemea sana mazao kutengeneza vileo ikiwamo mahindi na mtama, lakini bidhaa hiyo kuna muda haipatikani kwa wakulima, kutokana na ukame ambao muda mwingine husababishwa na mabadiliko ya tabianchi.

Anaendelea kwamba, kampuni imelazimika kupanda maelfu ya miti, ikiamini uwapo wake ni nyenzo ya kukabiliana na magumu hayo.

“Kuna mikoa ambayo tayari tumeshaanza zoezi la upandaji miti kama wilaya ya Same mkoani Kilimanjaro, mkoa wa Dodoma katika wilaya ya Kongwa na tunafanya hivyo kwa kushirikiana na taasisi mbalimbali wakiwamo wanahabari, ‘ki projekti’ iliyoko Moshi, ambayo inashujishughulisha na upandaji wa miti



Wafanyakazi wa kampuni ya bia Serengeti, wakishiriki tukio la upandaji miti, ikiwa ni sehemu ya wajibu wao kwa jamii, kupanda miti na kuchimba visima vya maji. **PICHA: HALFANI CHUSI.**

‘Sisi tuna hela, lakini hatuna miti. Kwa hiyo, ambacho huwa tunakifanya tunanunua miti kwao, halafu tukishapanda tunashirikiana pamoja katika kuitunza, ili ikue, maana mti ukishaupanda kama hutauhudumia sawasawa na hujafanya kitu utanyauka” anasema Wanyancha.

NINI WAMELENGA?

Wanyancha anasema lengo la kampeni ni kuhakikisha miaka ya baadaye Tanzania haikumbani na adha ya mabadiliko ya tabia ya nchi kama ilivyo kwa sasa.

“Ukiangalia sehemu nyingi hapa nchini, kumekuwa na ukame mkubwa. Hii yote ni kutokana na kutokuwa na miti ya kutosha. Ukiangalia wilaya ambazo tayari tumeshapanda miti kama Same na Kongwa, utagundua kidogo kuna hali nzuri na ukame umeanza kupungua.

‘Lengo letu ni kuona watu wa wilaya hizo wanaendeleza utamaduni huo, ambao sisi tunaamini kama wilaya zingine zitaiga mfumo huo kwa pamoja, tunaweza kukabili madhara yanayotokana na mabadiliko ya tabianchi, ikiwamo njaa muda mwingine hata mlipuko wa magonjwa.

“SBL inachukulia miti kama sehemu muhimu sana ya mazingira. Miti inasaidia kuhifadhi vyanzo vya maji, ni makazi kwa wanyama na wadudu mbalimbali, ina vuta hewa chafu ya kaboni na kuzalisha hewa safi, pia miti ni chanzo cha dawa,” anafafanua.

SIMULIZI YA NDUGAI

Katika upandaji wa miti mkoani Dodoma wilayani Kongwa mwaka 2019, aliyekuwa Spika wa Bunge, Job Ndugai, akaishukuru kampuni ya SBL kwa kuunga mkono jitihada za upandaji miti na kuongeza nafasi ya kipikee kwa maisha ya watu, kwani pasipo miti hakuna maisha.

Anaeleza ukataji miti holela ni kati ya sababu za mabadiliko ya tabianchi, yanayosababisha vikwazo vingi kwa binadamu, ikiwa na athari kwenye uzalishaji chakula, upatikanaji maji, afya ya viumbe na binadamu.

Katika kampeni hiyo, pia Ndugai akawataka Watanzania kujenga utamaduni wa kupanda miti kila mara, kwa maelezo kwamba si suala la kuiachia serikali pekee yake .

“Wapo wanaokata miti kwa shughuli mbalimbali za kijamii ikiwamo kuchoma mkaa. Hilo

Inaendelea Uk. 15

AFYA

# Ukuaji teknolojia elektroniki, utandawazi sasa unageuka shida kwa afya ya akili



Wanafunzi wa shule ya msingi jijini Mwanza wakimsikiliza aliyekuwa Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, John Mongella, alipotembelea shule hiyo, Machi mwaka juzi. Ni kada inayopaswa kulindwa kupitia elimu saikolojia, isitumbukie katika athari za mitandao. **PICHA: MTANDAO.**

**Na Neema Emmanuel, MWANZA**

UKATILI wa kimtandao ni miongoni mwa mambo yanayoshamiri kwa kasi katika jamii, hali kadhalika madhara yake ni makubwa, hususani kwa mabinti na vijana.

Mwarobaini wake unatajwa uko katika wazazi kufuatilia mienendo ya watoto wao, bila kusahau kutoa elimu ya matumizi sahihi ya mtandao.

Gervas Evodius, Mkurugenzi wa shirika la Haki Zetu Tanzania, anaieleza Nipashe kwamba, ukatili wa kimtandao sasa wanafanyiwa watu wengi na umekuwa na madhara makubwa, hasa katika afya akili, eneo la saikolojia.

Anafafanua kwamba, hali hiyo inachangia kumharibia mtu malengo yake na moja ya sababu kuu ni umma kupokea teknolojia, ikiwa haijajipanga vyema katika matumizi yake, hata wanashindwa kukabili mahitaji na yasiyohitajika kutoka kwenye mtandao huo.

"Ukiangalia sasa hivi kwenye mambo ya utandawazi, kuna vitu ambavyo watu wanaiga kwenye mataifa mengine, wanaona labda ndio mtindo wa maisha.

"Wanaamua kuishi katika mtiririko huo, mfano unakuta binti mdogo picha zake za utupu zimesambaa katika mitandao. Hali hiyo inaweza kusababisha kujifungia katika kupata fursa mbalimbali na hatoweza kuajirika kwenye taasisi au ajira nyingine.

"Pia, baadae atahitaji kuwa mzazi kama mama watoto wake watakuwa wataona, kwa sababu kitu kikiwekwa kwenye mtandao, maana yake kitaendelea kuwepo kwa muda mrefu," anaeleza Gervas

Anafafanua sababu ya hisia hizo kusailojia, ni kwamba wenye ushawishi mkubwa kwenye jamii wamechangia kuwepo mmomonyoko wa maadili kimtandao, kwani wapo wanaotaka kuwa maarufu kwa kuiga ya mtandaoni.

"Watu maarufu kama wamefanya halafu watu wakaona hajachukuliwa hatua kali, jamii inaona kama kitu cha kawaida basi na mwingine anafanya, hata ukiangalia maoni(comments) ya watu kuwa ukitaka kuwa maarufu achia video yako.

"Tunatakiwa tuchambue maudhui ambayo yapo mitandaoni, tutatambua sisi kwa jamii yetu tunataka maudhui gani, kwani video hizo za utupu zinaweza kuwa nzuri katika nchi nyingine na zisiwe nzuri kwetu, ingawa serikali yetu imejitahidi kuzifunga saiti (mitandao yenye maudhui ya ngono)," anafafanua Gervas.

Hata hivyo, anasema sheria pekee yake haijawahi kufanya kazi ikafanikiwa na ndio maana watu wanatahadharishwa kutii sheria, lakini wanaendelea kukiuka.

Kwa maoni yake, Gervas anasema jambo linaloweza kuwa mwarobaini wa kudumu kukabili upungufu huo wa kijamii, ni kutolewa elimu stahiki, hata umma ukabadilika kimtazamo, pale wanapojua madhara yake, daima hawatafanya kitendo hicho, kwa sababu tayari wana uelewa.

"Sheria inaweza kuwepo na vitendo vikawepo, sasa tuendelee kutoa elimu na tuwaonyeshe madhara ya picha au video zisizo na maadili, hasa kwa watoto walio shuleni na vijana ambao bado wapo vyuoni.

"Kwa sababu watoto wadogo ni rahisi kuonewa ambao bado wako shuleni au mtaani ni rahisi kurubuniwa, wakiwa katika mapenzi akiambiwa nitumie video zako na yeye akatuma tu," anaeleza Gervas.

Vilevile anashauri hatua nyingine sahihi, ni kwa umma unatakiwa kufundishwa kwamba mtu hapaswi kumuamini yoyote, maana mara nyingi wanaowafanyiwa ukatili ni wale watu wanaowaamini na kutuma hizo video.

Gervas anafafanua mikasa hiyo ya kisaikolojia, kwamba wanaowaamini ndio wanakuwa wasambazaji wa hizo video, wanapaswa kufunzwa kutomuamini mtu yeyote, kwani anaweza kuwa ulingo wa maovu dhidi yake.

Mwanasaikolojia huyo anasema, jamii inapaswa kufunzwa hata pale wanapokuwa wamehifadhi video kwenye kompyuta mpakato (laptop), simu na nyenzo zingine za kielektroniki vinaweza kupotea na watu wasio wema wakaokota, hata wakavisambaza.

"Kwa hiyo tuwafundishe, kwa sababu sheria ipo, lakini mtu ataiba simu yangu atasambaza kama kuna video hizo. Sheria itaniadhibu mimi, lakini aliyesambaza ni mtu mwingine, hivyo tuwaambie wasihifadhi hizo video wala picha, ndio itakuwa mwarobaini wa tatizo, kwani sheria pekee haiwezi kumaliza changamoto hiyo," anashauri Gervas.

Pia, anataja nyenzo nyingine ya kinga, ni kwa familia ikae na kuchunguza mienendo ya watoto wao vitu wanavyovipenda kwenye mitandao na runinga kuanzia utotoni, hata inapofika umri mkubwa anakuwa kaathirika.

**USTAWI JAMII**

Ofisa Ustawi wa Jamii Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela, Christiana Mwambola, anasema utandawazi umewafikishia simu watoto na vijana shuleni, wanatumiana picha chafu, tofauti na zamani waliandikiana barua.

Mwambola anasema, ingawa sheria hairuhusu mtoto mdogo kumiliki simu, baadhi ya wazazi wanawapa simu na ndio unakuwa mwanzo wa mitandao kuathiri saikolojia zao, ingawa walakini huo, pia unawafikia hata watu wazima.

"Lengo la mtandao ni mawasiliano, lakini jinsi inavyotumika kwa jamii zetu ni vibaya, hasa kwa watu wazima na watoto, kila mtu anatumia tofauti, hali inayoongeza ukatili sana mtaani, kwa sababu watu wanapata uelewa wa namna ya kufanya vitendo vya ukatili kutoka kwa watu wengine," anasema Mwambola.

Anaeleza kuwa, pale sheria zinaposimamiwa kwa umakini na kwa vitendo zitasaidia, akitoa mfano pale watoto wanapotumiana picha 'chafu', vivyo hivyo kwa watu wazima, kati ya wapenzi au mke na mume, udhibiti ukiwa bora unakuwa na mchango katika kusaidia kumaliza ukatili wa kimtandao.

Ofisa Dawati la Jinsia na Watoto katika Hospitali ya Rufani Sekou-Toure (one stop center) Gift Msowoya, anasema, huwa wanapokea kesi nyingi za ukatili wa kimtandao, akikiri unagusa watoto na watu wazima.

Anasema, mhusika anapowajia na uthibitisho kwamba amerekodiwa, huwa wanachukua maelezo ya mlengwa, wanampa ushauri nasaha na kisha wakimaliza kumhoji wanamshauri namna ya kufungua kesi.

"Kuna wengine wanaogopa kuwa wakifungua kesi, inaweza kusambaa zaidi, lakini tunamueleza kuwa watalifikisha mbele ya sheria na litabakia mikononi mwa sheria, huku wakichukua hatua ya kudhibiti kwa kuwachukulia hatua wale watu ambao wamefanya hivyo, ili video isiendelee kusambaa," anaeleza .

Pia, anasema wamekuwa sehemu ya kuupa umma elimu, kwani siyo wote wanaorekodiwa wanayanajua madhara husika, baadhi wakihisi wapo kwenye starehe, pasipo kujua wanaweza kugombana hivyo na mtu akaamua kusambaza.

"Tunaendelea kuwapa elimu watu wote siyo wahanga pekee, hata ambao hawajatendewa vitendo hivyo, ili wasijiingize kwenye kundi au vitendo vya kuchukuliwa video za utupu na kisha kusambazwa kwenye mitandao.

"Uzuri sheria zipo wazi, tunaendelea kuelimisha watu ili wajue imetungiwa sheria maalum ya matumizi mabaya ya mtandao na wanapokuja tunawasaidia," anaeleza Msowoya.

MAZINGIRA

# Hatimaye mradi wa maji uliosuasua miaka tisa, washikiwa 'bango' utimie

**Na Gideon Mwakanosya, NAMTUMBO**

NI hadithi mpya katika kipengele cha kusambaza maji wilayani Namtumbo, mkoani Ruvuma. Mnamo Oktoba mwaka 2013, chini ya Wakala wa Usambazaji Maji Safi na Salama Vijijini (RUWASA) wilayani Namtumbo, kulitiwa saini mkataba wa kujenga mradi wa maji kuwafikishia wakazi 7, 927, lakini ukagota miaka minne.

Pale, utekelezaji wake ulipoanza kwa matarajio ya kukamilika Desemba mwaka 2019, nao ukakwama kutokana na madai ya kuyumbishwa na mkandarasi.

Meneja wa Ruwasa wilaya ya Namtumbo David Mkondya, anaiambia Nipashe kwamba ni mradi unaowalenga wakazi wa vijiji viwili , Litola na Kumbara, ambao tangu uhuru hawajawahi kufikiwa na maji ya bomba.

Anasema, hadi sasa serikali imeshatenga zaidi ya Sh milioni 423 kukamilisha ujenzi wa mradi wa maji wa Litola-Kumbara wilayani Namtumbo.

Mkondya anaeleza fedha hizo zitatumika kununua mabomba ya chuma yatakayosambazwa kutoka kwenye chanzo cha maji hadi kwenye tenki umbali wa km 17.76.

Kwa mujibu wa Mkondya, utekelezaji wa kwanza ulishindwa kukamilika baada ya mkandarasi aliyekabidhiwa kazi hiyo ya kiufundi, kushindwa kuikamilisha.

Anasema, hivi sasa kazi hiyo inakamilishwa chini ya mkandarasi mpya na hadi sasa, kazi zilizotekelezwa zinajumuisha matenki mawili yenye ujazo wa lita 100,000 na lita 75,000, huku ujenzi wa chanzo cha kukusanya maji na uchimbaji mtaro na kulaza mabomba ya kusambaza maji umbali wa kilomita 22 ukiendelea.



Tangi la maji ambalo linajengwa kwenye mradi huo.

Kazi nyingine anazitaja ni kuchimba mtaro na kulazwa bomba kuu kutoka chanzo, umbali wa kilomita 11 kati ya kilomita 17.76, pia ujenzi wa vituo 32 vya kuchota maji na kujenga mifumo ya mfano ya uvunaji maji ya mvua.

Kwa mujibu wa Mkondya, mradi huo unakamilishwa na Ruwasa kwa njia ya inayoitwa 'Force Account' ambayo msingi wake ni akaunti kwa ajili ya jambo maalum, ambako sekta ya maji hutumia mara nyingi.

Meneja Mkondya, anasema waliamua kutia saini mkataba huo katika eneo la mradi, ili wanufaika wa mradi wawe mashuhuda, hata wakarudishiwa matumaini yaliyotoweka, hasa mradi huo ulipoanza kutekelezwa muda mrefu, pasipo mafanikio.

**DC NA KINACHOJIRI**

Hivi karibuni akipokea mabomba ya chuma yaliyokusudiwa kumaliza kero tajwa ya maji vijijini Litola na Kumbara, Mkuu wa Wilaya ya Namtumbo, Dk. Julius Ningu, anasema RUWASA inatakiwa kukamilisha mradi huo kama ilivyokusudiwa , ili kuwamalizia kero ya maji wananchi hao.

Dk. Ningu anafafanua, sababu ya mradi kuchelewa ni kutokana na kuchelewa utengenezaji mabomba ya chuma yaliyotakiwa kutumika katika kutekeleza mradi huo, ambao ulisimama kwa miaka mitano toka 2017 mpaka 2022.

Anaeleza matarajio ya serikali kusimamia matengenezo na upatikanaji mabomba hayo ya chuma, itamaliza kilio cha muda mrefu cha wananchi wa vijiji vya Kumbara na Litola, ambao kila mara wamekuwa wakilalamika serikali kutokamilisha mradi huo wa maji.

Pia, anatumia fursa hiyo kuelekeza kwamba, utekelezaji wa miradi yote ya maji inayofanyika wilayani Namtumbo, ofisi yake ifahamishwe, hata kusaidia kufuatilia utekelezaji wake.

Mkondya katika taarifa yake kwa Mkuu wa Wilaya, anataja kazi zilizofanyika katika mradi ni ujenzi wa matenki mawili yaliyoainishwa, chanzo cha kukusanyia maji, uchimbaji na kulaza mtandao wa mabomba ya usambazaji maji na vituo 32 vya kuchota maji katika kijiji.



Mafundi wa mabomba wakiwa kazini. **PICHA ZOTE: GIDEON MWAKANOSYA.**

Pia, anataja kazi ambazo hazijafanyika ni ununuzi na ulazaji wa bomba kuu kutoka katika chanzo, umbali wa mita 7000 (kilometa saba), kujengwa chemba katika bomba kuu na chanzo, baada ya kulaza mabomba ya chuma.

Yusta Nikata, mkazi wa kijiji cha Kumbara, anasema kupokewa kwa mabomba hayo ya chuma, kunawapa imani kuwa sasa mradi huo wa maji uko katika hatua ya kukamilika.

Tofauti na hali ya awali, inaelezwa wameamini kwamba mradi huo umetelekezwa ambao matarajio ya wananchi juu yake yalikuwa yanatia shaka, hata imani kupungua.

Mabomba ya chuma yaliyopokelewa ni yenye jumla ya urefu wa mita 4,698 kati ya mita 7000 zinazohitajika yakiigharimu serikali shilingi milioni 499.557, ambayo ni malipo ya awali.

Awali, Serikali ilitia saini mkataba na kampuni ya Tanzania Steel Pipes, kwa ajili ya kutengeneza mabomba ya chuma yatakayotumika kusambaza na kufikisha huduma ya maji karibu na makazi ya wananchi.

Meneja wa Ruwasa Mkoa wa Ruvuma, Rebman Gansonga, anasema, katika kutatua kero ya maji kwa wananchi wa vijiji hivyo na maeneo mengine mkoani Ruvuma, wameshirikiana na viongozi wa serikali kuanzia ngazi ya vijiji, kata, wilaya hadi mkoa.

Hivyo amewataka wananchi kuhakikisha wanatunza mradi na miundimbinu yake ili uweze kudumu na kuharakisha maendeleo yao kama ilivyokusudiwa

Anasema, mradi wa maji Litola - Kumbara, sasa umeshindwa kukamilika kwa wakati, kutokana na changamoto mbalimbali, ikiwemo mkandarasi wa awali kushindwa kutekeleza kazi hiyo na hivyo wizara ya maji kulazimika kuvunja mkataba wake.

***Mwandishi wa makala anapatikana kwa simu: +255 754 928752***

# Kampuni inayowekeza katika urafiki tabianchi

**INATOKA UK. 13**

sio sawa, kwa sababu wengi huwa hawakumbuki hata kupanda miti mingine," akaeleza Ndugai, ambaye ni mbunge wa Kongwa.

**MNUFAIKA ANENA**

Machicha Malolela, mkazi wa wilayani Kongwa, anashuhudia namna miti iliyopandwa na SBL ilivyochangia kuleta mabadiliko chanya katika kilimo.

"Wilaya yetu ni moja kati ya wilaya ambazo zilikuwa zinakabiliwa na ukame kwa miaka mingi lakini tangu 2019 walipokuja kupanda miti hapa kumekuwa na mabadiliko makubwa.

"Kwanza, mwaka huu mvua imenyesha kwa wingi, tofauti na miaka mingine, licha ya sehemu nyingi kukabiliwa na ukame, lakini kwetu hapa kumekuwa na neema ya kipekee.

"Kwenye kilimo, watu wamepata mahindi, ufuta, na mtama kwa wingi jambo jingine tunapata hewa safi pamoja na maeneo mazuri ya kupumzika nyakati za jua kali kwa hiyo kipekee sisi wakazi wa wilaya hii tunashukuru kwa jitihada za dhati za kuungana na sisi katika zoezi zima la upandaji miti"

Alipoulizwa, namna gani wamekuwa wakiendeleza juhudi hizo?, akajibu wao wana mpango wa kuongeza miti 1000 katika sehemu zenye, upungufu wa miti akizitaja Msagali na Barabara ya Mpwapwa.

**AGIZO LA WAZIRI MKUU**

Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, akiwa Dodoma katika uzinduzi wa upandaji miti katika Mji wa Serikali Mtumba, aliambatana na Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira Dk. Selemani Jafo pamoja na viongozi mbalimbali wa Kitaifa na Mkoa.

Alisema, serikali kupitia Ofisi ya Rais kwa kushirikiana na Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira imeendelea kuratibu utekelezaji wa kampeni ya kitaifa ya upandaji na utunzaji miti, inayotekelezwa nchini kwa kila halmashauri kupanda miti milioni 1.5 kila mwaka.

"Suala la kupanda miti na kuitunza ni la muhimu kwa ustawi wa Mazingira ya Taifa letu hatua inayokwenda sambamba na uhimili wa mabadiliko ya tabianchi lakini pia unawezesha mazingira ya miji yetu kuwa ya kijani na mandhari nzuri ya kuvutia.

Pia akaagiza Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira, timu ya wataalamu pamoja na Wakala wa Huduma za Misitu kusimamia kikamilifu ujenzi wa mji wa serikali pamoja na programu ya upandaji miti pamoja na kuelimisha jamii juu ya upandaji bora wa miti kwa kuzingatia hali ya hewa ya eneo husika ili upandaji uwe na tija.

AFYA

# Minamata, ugonjwa uliojificha ukiwanyemelea wachimba dhahabu wadogo waliopo Chunya

**Na Grace Mwakalinga, CHUNYA**

"TANGU nianze shughuli hii ya uchenjuaji dhahabu, kwa kutumia kemikali ya zebaki sijawahi kupata madhara yoyote ya kiafya, ikiwa ni zaidi ya miaka kumi sasa."

Ni kauli ya mchimbaji mdogo wa madini aitwaye Lucia Mpanda, mkazi wa kijiji cha Itumbi, katika kata ya Matundasi wilayani Chunya, wakati akizungumza na Nipashe.

Lucia anasema, shughuli ya uchimbaji na uchenjuaji dhahabu ndiyo kubwa na anayoitegemea kuendesha maisha yake, kwa maana ya kukidhi hata mahitaji mbalimbali ya wanawe.

Hapo Lucia anasimulia cha ziada kwamba, katika kuendesha shughuli zake za madini, hulazimika kutumia kemikali kama vile zebaki wakati wa kile anachokitafsiri 'kuikamata' na utakatishaji wa dhahabu kabla ya kwenda kuuza.



Baadhi ya wachimbaji wa madini, eneo la Itumba Kata ya Matundasi wilayani Chunya Mkoa wa Mbeya, wakiendelea na uchenjuaji wa dhahabu bila vifaa vya kujikinga na kemikali. **PICHA ZOTE: GRACE MWAKALINGA**

Kimsingi, ni hoja inayoibua kitendawili cha kiafya kwamba, kukiwapo maelezo madhara yatokanayo na matumizi ya kemikali hiyo, huonekana taratibu kwa watumiaji na si ajabu kutoonekana muda mrefu.

Mwenyekiti wa Chama cha Wachimbaji wa Madini Mkoa wa Mbeya, (MBELEMA), Leonard Manyesha, anasema baadhi ya wachimbaji wadogo wa madini wilayani Chunya, hulazimika kutumia mikono kuchenjua dhahabu bila ya kuvaa vifaa vya kujikinga na madhara ya kemikali, kutokana na ukosefu wa fedha za kuvinunua.

Anasema, vifaa kinga kwa wachimbaji wadogo wa madini vinauzwa kwa bei ghali, kiasi cha kuwafanya baadhi yao kushindwa kuvinunua na kuna wakati huwa havipatikani katika maeneo yao ya uchimbaji.

Manyesha anasema, hata gharama za ununuzi wa mitambo ya uchenjuaji dhahabu ni kubwa, hali inayowalazimu wachimbaji wengi wa madini kutumia zana duni, pasipo kujali madhara ya kiafya wanayoyapata.

Kwa mujibu wa Manyesha, miundombinu ya kusaidia uchimbaji madini kama vile umeme na maji pia sio rafiki kwao wachimbaji, hali inayochangia baadhi ya wachimbaji kuathirika kiafya, pasipo kujua.

"Wilaya ya Chunya ina uhaba mkubwa wa maji, hali inayosababisha shughuli za uchimbaji na uchenjuaji kukwama. Baadhi ya wamiliki wa migodi hulazimika kutumia gharama kununua maji, ili kufanikisha kazi zao. Tunatamani kuwa na mitambo mikubwa, lakini vikwazo kama hivi vinakwamisha kufikia malengo yetu.

"Miongoni mwa mambo yatakayosaidia kuachana na matumizi ya nyenzo duni za kuchimbia na kuchenjulia dhahabu ni pamoja na serikali kutusaidia kupata mikopo yenye riba nafuu, ili itusaidie kununua mitambo rafiki na ambayo itatuwezesha kuachana na matumizi ya kemikali ya zebaki kwenye shughuli zetu," anasema.

### MAONI YA KITAALAMU

Mkurugenzi wa kampuni ya Apex Resource, Shigongo Kimongele, anasema utafiti uliofanywa mwaka 2012 unaonyesha kuwapo teknolojia ya kuwasaidia wachimbaji wadogo kupata madini ya dhahabu mara tatu zaidi ya ile wanayoipata kwa kutumia kemikali ya Zebaki.

"Zebaki inapowekwa kwenye maji hutumika kutenganisha dhahabu na mchanga, lakini kutokana na elimu duni juu ya madhara yatokanayo na zebaki kwenye mwili wa binadamu, hakuna tahadhari yoyote inayotolewa na wataalamu wa afya kwa wachimbaji wadogo," anasema Kamongele.

Anashauri, hatua za makusudi zinahitajika kuwanusuru wachimbaji hao walio hatarini kupata magonjwa ya ngozi, kama vile kansa, kwa sababu wanaweza kula na kuvuta mvuke wa kemikali hiyo wakati wa kuchoma dhahabu.

Kamongele anaongeza, hatari hiyo ipo hata inapogusana na ngozi, wachimbaji wanakuwa hatarini kudhurika zaidi, kutokana na kuvuta vumbi la mgodi lililochanganyika na kemikali unaoingia moja kwa moja kwenye mfumo wao wa hewa.

### MKEMIA MKUU ANENA

Mkemia Mkuu wa Serikali, Kanda ya Mbeya, Gasper Mushi anasema wachenjuaji hao wa madini, pia wana hatari ya kupata ugonjwa wa Minamata, unaosabishwa na masalia ya kemikali yanayopatikana kwenye udongo, maji na vyakula.

Anasema, pale kemikali hiyo inapokuwa ndani ya udongo, mimea inayomea kwenye ardhi hiyo nayo huchukua kemikali hiyo, hata kumfikia mwanadamu alaye chakula chenye kemikali iliyopo kwenye mmea huo.

Mushi anazitaja baadhi ya dalili za ugonjwa huo, kuwa ni kupoteza kumbukumbu, mwili kutetemeka, kansa kwenye figo, kongosho, ini na damu.

Kwa mujibu wa mkemia huyo wa serikali, endapo wachenjuaji dhahabu hawatatumia vifaa vya kisasa kwenye shughuli zao, wako hatarini kupata ugonjwa huo wa minamata.

Anafafanua, mpaka sasa ugonjwa huo haujawahi kuripotiwa nchini, ingawa historia inaonyesha kuwa mwaka 1953 ugonjwa huo uliripotiwa kulipuka nchini Japan.

Pia, anaeleza pale kemikali hiyo inapoingia kwenye maji ya mito, ziwa au bahari, huwaingia viumbe hai wanaopatikana mahali hapo, wakiwa samaki na pale wanapokuwa mlo kwa binadamu, wanaweza kupatwa na ugonjwa minamata.

"Tumekuwa tukifanya ukaguzi wa mara kwa mara kwenye migodi huko wilayani Chunya. Tumeona kwa kiasi kikubwa, hakuna vifaa vya kisasa vinavyotumika kufanya shughuli za uchenjuaji wa dhahabu. Tumebaini wapo wachimbaji wanaotumia mikono kufanya shughuli hizo jambo ambalo ni hatari kwa afya zao," anasema Mushi.

Anasema, utafiti walioufanya wamebaini baadhi ya wachimbaji hawataki kutumia vifaa, kwa madai inawapotezea muda, pia imani potofu kwamba wakivaa mipira ya mikononi huharibu ubora wa dhahabu.

Mushi anaeleza kuwa, madhara ya matumizi ya zebaki yamechukua muda mrefu kugundulika, hivyo ni muhimu kwa wachimbaji wakachukua tahadhari, kwani ni madhara yanayoathiri vizazi na vizazi.

Athari zinazoweza kujitokeza kwa watu wanaokabiliana na matumizi ya kemikali hasa wanawake, ni pamoja na kujifungua watoto wenye ulemavu wa viungo, watoto kupata degedege na magonjwa mengine kama vile kansa ya ngozi na ugumba kwa mwanaume au mwanamke.

"Nawakumbusha wamiliki wa viwanda vya kuchenjua dhahabu, kuwasisitiza wafanyakazi wao kutumia vifaa vya kujikinga na kemikali," anasema Mushi.

"Pia, kuzingatia matumizi sahihi ya zebaki wakati wa kuchenjua dhahabu kwa vile madhara hutokea kwa njia ya mvuke hasa wakati wa uchomaji wa dhahabu, pia mtu anaweza kupata madhara kwa njia ya ngozi pale anapogusa kemikali hiyo," anahitimisha.



AFYA

# Namna elimu ya VVU haijazama kwa kina waliko wanafunzi shule

**Na Augusta Njoji, DODOMA**



Mwakilishi wa Mkurugenzi Afya, Ustawi na Lishe kutoka Ofisi ya Rais(TAMISEMI), Amina Mlakia, akifafanua jambo katika mdahalo wa wadau wa utekelezaji shughuli zinazohusu UKIMWI kwa wawakilishi wa Baraza la Watu Wanaoishi na Maambukizi ya Virusi vya UKIMWI (NACOPHA). **PICHA: AUGUSTA NJOJI.**

TAKWIMU zinaonyesha vijana wanachangia maambukizi mapya ya Virusi Vya Ukimwi (VVU) kwa asilimia 40 kila mwaka.

Sababu kubwa ya kasi hiyo kwa vijana, inatokana na kukosa elimu ya kina kuhusu afya ya uzazi, stadi za maisha, ukatili jinsia, umaskini, mila na desturi, hata wakajihusisha na ngono au ndoa za umri mdogo.

Ni hali inayotajwa kuufanya UKIMWI uendelee kuwa tishio kwa ustawi wa nchi, kwa kuathiri shughuli za uzalishaji na maendeleo ya kijamii.

Katika takwimu hizo, vijana wa kike wanatajwa kuchangia asilimia 80 na kiume asilimia 20. Sasa kuna jitihada za kusaidia vijana wanaoishi na VVU, ambao wanakutana na vikwazo wanapokuwa kwenye mfumo wa elimu kuanzia msingi hadi chuo kikuu.

**UHALISIA ULIKOEGEMEA**

Tume ya Taifa ya Kudhibiti Ukimwi (TACAIDS) kwa kushirikiana na Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Watoto (UNICEF), kupitia mradi wa 'Dreams' unataka kuanza kuchukua hatua, ikiwamo mjadala wa upatikanaji huduma za Virusi vya Ukimwi na UKIMWI, katika mazingira ya kutoa elimu na njia bora za kuhudumia, bila kuathiri upatikanaji elimu kwa vijana.

Akiwasilisha taarifa ya utafiti mdogo uliofanywa kuhusu huduma za VVU na UKIMWI kwenye baadhi ya shule nchini iliyofanywa na UNICEF na Kituo cha Utafiti wa Magonjwa (NIMR), Mshauri Mwelekezi Dk. Andrew Kigombola, anasema bado kuna tatizo la upatikanaji huduma, kukosekana ushirikiano kati ya wazazi au walezi na walimu.

Anasema, baada ya kubaini hayo walifanya tathmini kujua kinachoathiri utoaji huduma kwa ngazi ya wizara, mikoa na wilaya.

Dk. Kigombola anasema takwimu zinaonyesha vijana balehe wenye umri kati ya miaka 10 hadi19 wanaoishi na VVU ni 99,000 wakiwa katika mgawanyiko 57,000 ni wasichana, akitaja sababu wanaanza ngono katika umri mdogo.

"Unakuta mtu mwenye miaka 40 ameshazunguka nchi nzima ametembea na huyu na huyu na matokeo ana maambukizi anatembea na kijana mwenye umri mdogo na hii inachangia kwa kiasi kikubwa maambukizi ya wasichana yanakuwa yapo juu," anasema.

Mtaalamu huyo anafafanua ni utafiti wao waliofanya katika mikoa ya Njombe, Mbeya na Songwe kwa kupitia nyaraka mbalimbali na kuhoji watu,kuanzia ngazi ya wizara, hadi shuleni walikopata ufafanuzi.

Anaeleza: "Sera ya elimu imezungumza umuhimu wa kuwajengea uwezo kwenye huduma za uzazi, sera imelenga vyuo, shule na vyuo vya ualimu. Tulipofanya mahojiano, walisema sera zipo zinajitosheleza, lakini kuna shida kwenye utekelezaji wa pamoja bado haupo vizuri."

Kwa mujibu wa mtafiti huyo, Wizara ya Afya inapaswa kutoa huduma za afya shuleni, lakini hakuna taarifa kuhusu suala hilo. Anaendelea: "Mitaala ipo inazungumzia umuhimu wa kujumuisha elimu ya afya, HIV, afya ya uzazi na asilimia 79 walikubali mitaala ipo, lakini changamoto ni ufundishaji."

Kuhusu waliohojiwa, anasema walionyesha kwenye masomo ambayo wanapaswa wanafunzi kufundishwa kuhusu, afya, HIV na masuala ya jinsia walimu hawafundishwi na wengine wanafundishwa kwa ufupi, kwa kuwa masuala hayo hayachukui nafasi kwenye mitihani yao.

"Kuna jitihada mbalimbali za kujengea uwezo walimu ambao wanajengewa kwa sasa wamefikia takribani 10,000. Hivyo ni muhimu kuwafikia wengi zaidi, ili kupata elimu ya kufundisha masuala hayo kwa wanafunzi," anasema.

Pia, anasema kwenye mikoa kuna shughuli zinazofanyika, lakini kuna kilio haziwafikii vilivyo vijana balehe na waratibu wa UKIMWI kwenye shule kwa kutumia rasilimali zilizopo.

"Ni muhimu kutumia wadau kutumia rasilimali zilizopo kufikia vijana balehe kwenye shule ili kuwajengea uwezo vijana wanaoishi na maambukizi na wasio na maambukizi," anasema.

**WADAU WATAALAMU**

Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa TACAIDS, Jumanne Issango, akifungua mjadala uliohusisha Vijana na Wawakilishi wa Baraza la Watu Wanaoishi na Virusi vya UKIMWI (NACOPHA), anafafanua uhalisia uliopo ni kwamba, kabla mtu kuanza maisha kujitegemea, vijana wote nchini lazima wapite kwenye mfumo wa elimu.

"Wakati wakiwa kwenye mfumo wa elimu wanapatiwa elimu ya afya ya uzazi, stadi za maisha, elimu ya VVU na UKIMWI kama somo la hiari na baadhi wanamaliza bila kuwa na elimu hii," anasema.

Pia, anataja pamoja na kuwapo nafuu hiyo, vijana wengi wanaoishi na maambukizi ya VVU wameendelea kukutana na vikwazo wanapokuwa katika mfumo wa elimu.

"Hali inakuwa tofauti kwa vijana ambao wapo shule za bweni kutokana na kuwa mbali na wazazi au walezi, mazingira haya husababisha wengi wao kuwa katika hatari ya kupata unyanyapaa na ubaguzi, kukosa lishe bora na mazingira rafiki," anasema.

Dk. Mastidia Rutaihwa kutoka Mpango wa Taifa wa Kudhibiti UKIMWI (NACP) anaeleza kuhusu huduma za VVU kwa vijana balehe Tanzania, kuna kasoro ya huduma rafiki za afya kwa vijana, ikiwamo matumizi madogo ya kondomu.

Anashauri wazazi na walezi kuwaambia ukweli vijana na watoto kuhusu hali zao kiafya, ili wawe wafuasi wa dawa stahiki.

"Usiri unaofanywa na wazazi unasababisha wasiwe wafuasi wa dawa, mwingine anamwambia ulipokuwa unazaliwa ulikunywa maji machafu, matokeo yake mtoto anapokuwa shule bweni anakosa usimamizi wa kuzingatia matumizi ya dawa," anasema.

Katika hilo,Mwakilishi wa Mkurugenzi wa Idara ya Afya Ustawi na Lishe kutoka Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Amina Mlaki, anasema watoa huduma ngazi ya jamii wamekuwa wakisaidia kwenye utekelezaji wa afua za VVU ikiwamo kutoa elimu kwa vijana.

**NENO KUTOKA UNICEF**

Ofisa wa kitengo cha VVU na UKIMWI wa shirika la UNICEF, John George, anasema idadi ya watoto na vijana wanaoishi na VVU ni kubwa, hivyo ni vyema kuwa na hatua zinazowalenga zaidi kuzuia maambukizi na kuwasaidia wanaoishi na VVU.

Anasema sera, mipango mikakati ya elimu ya afya shuleni nayo bado ina tatizo, kuhusu uelewa wa dhana hiyo.

"Utafiti unaonyesha vijana wanaoishi na VVU ambao wapo shuleni wana changamoto ya kupata elimu ya UKIMWI kwa wasio na VVU, lakini wenye VVU wanapata changamoto ya kukosa ruhusa kuchukua dawa, unyanyapaa unafanya wasijitambulishe," anasema.

Anaeleza kuwapo vijana waliojiweka wazi, wakiwa nyumbani wanatumia vizuri dawa na wakienda shule hawazingatii.

"Vijana kati ya umri wa miaka 15 hadi 19, ufuasi wao wa kutumia dawa ni mdogo, ikilinganishwa na walio na umri wa miaka 10 hadi 14, kutokana na kutokuwa kwenye himaya ya wazazi," anadems,akishauri vyema kukawekwa mikakati ya kuangalia namna ya kuhudumia kundi hilo.

"Mwongozo wa WHO unataka shughuli za afya ya UKIMWI ihusishwe na masuala ya afya ya uzazi, hivyo muhimu shughuli hizi kuunganishwa pamoja," anasema.

Mwenyekiti wa Mtandao wa Vijana wanaoishi na Maambukizi ya Virusi vya UKIMWI, Pudensia Mbwiliza, anahitimisha kwa kusema ipo haja ya wadau kuunganisha nguvu kutatua vikwazo vinavyowakabili.

AFYA

MIAKA 28 YA AZIMIO ...

# Bosi UNFPA: Ajenda ni 'sifuri' katika vifo watoto, uzazi hatari, ukatili jinsia

**Na Yasmine Protace**

MARK Bryan Schreiner, ni mwakilishi wa Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulika na Idadi ya Watu (UNFPA), anayetafsiri afya ya uzazi ni haki ya wanawake na ili watu wote wapate huduma ya kina katika afya ya uzazi, hapo inajumuisha mpango wa mimba salama na huduma za uzazi salama.

Schreiner anayatamka hayo jijini Dar es Salaam, akisema

Mkutano wa Kimataifa wa Idadi ya Watu na Maendeleo, unaojulikana kama ICPD uliofanyika mwaka 1994 jijini Cairo, Misri ulipitisha mpango wa utekelezaji ulioazimia mambo kadhaa, ikiwamo "afya ya uzazi na haki za wanawake kuwa kitovu cha maendeleo.'

Anasema watu wote wanapaswa wapate huduma ya kina ya afya ya uzazi,ikiwa ni pamoja na uzazi wa mpango wa hiari, mimba salama na huduma za uzazi.

Kikao cha ICPD pia kinatambua afya ya uzazi na uwezeshaji wa wanawake ni jambo muhimu kwa maendeleo ya jamii, huku Schreiner akisema, UNFPA ilipewa uongozi kusaidia nchi kutekeleza Mpango wa Utekelezaji wa ICPD.

Mwakilishi huyo wa UNFPA anaendelea:"tunakutana miaka 25 baada ya kongamano la awali la Kimataifa la Idadi ya Watu na Maendeleo ili kukagua maendeleo, Mkutano wa Kilele wa Nairobi kuhusu ICPD25 ulifanyika mwaka wa 2019."

Anasema mkutano huo wa mwaka 2019 ulisababisha kinachojulikana 'Ahadi za Nairobi', zaidi ya ahadi 1,300 za hiari zilitolewa na zingine za kiserikali 140 na washirika, kuhusu afya na haki za wanawake.

Schreiner anaongeza kuwa Mkutano wa Nairobi uliungwa mkono ili kufikia matokeo matatu ya mageuzi, ndani ya miaka 10 akizitaja ni: Kufutwa vifo vya uzazi vinavyozuilika; mpango uzazi usiokamilika; na kufutwa ukatili wa kijinsia na mila hatarishi, ikiwamo ndoa za utotoni.

Mwakilishi huyo wa UNFPA, anakiri kutambua hatua za kiserikali nchini kufuta madhila hayo kiafya, kijamii na kisaikolojia na anaahidi kuchukua hatua zaidi.

"Tunasisitiza kwamba UNFPA inalenga kuunga mkono serikali ya Tanzania, ili kuharakisha maendeleo kuelekea ahadi hizi," anaeleza Schreiner, akitaja furaha yake ya Zanzibar kushirikishwa.

Anaeleza, wiki hii Zanzibar itashirikishwa wakikusanyika kupeleka ahadi za kimataifa kuhusu afya ya uzazi na haki za ngono, ni wajumbe wa Tume ya Ngazi ya Juu ya Mkutano wa Kilele wa Nairobi wa Ufuatiliaji wa ICPD25.



Mwakilishi Mkazi kutoka UNFPA, Mark Bryan Scheiner, akizungumza na waandishi wa habari, pichani hawapo. **PICHA: YASMINE PROTACE.**

Anaongeza kuwa tume ya ngazi ya juu ina jukumu la kufuatilia, kuripoti na kutoa mapendekezo kuhusu maendeleo ya ahadi za ICPD25. Wanawasilisha ripoti ya pili ya mwaka ya ufuatiliaji wa ahadi za Mkutano wa Nairobi.

Schreiner anasema, Wenyeviti Wenza wa Tume ya Ngazi ya Juu ni: Rais Mstaafu Jakaya Kikwete na Michaelle Jean, Gavana Mkuu wa zamani na Kamanda Mkuu wa Canada.

Anafafanua kwamba tume hiyo ya ngazi ya juu, itafanya ziara Zanzibar katika hospitali, vitengo vya afya, vituo rafiki kwa vijana, kushuhudia hali ya mabadiliko nchini katika maisha, hasa kwa wanawake na wasichana.

Anaongeza kuwa tafsiri za maendeleo zilibainishwa kwenye baadhi ya ahadi za mkutano wa Nairobi, lakini ndani yake kuna hali ya kurudi nyuma kwa jumla katika afya ya ngono na uzazi na haki duniani kote.

"Hatua za kina zinahitajika ili kufikia haki ya kujamiiana na uzazi kwa wote, hasa kwa wanawake na wasichana," anasema mwakilishi huyo wa UNFPA nchini.

### MTAALAMU ANAAINISHA

Felister Bwana, ni mtaalamu wa masuala ya afya ya uzazi mama na mtoto kutoka UNFPA, anasema Tanzania imejipanga ifikapo mwaka 2030 kuongeza upatikanaji wa huduma za dharula wakati wa uzazi.

Anasema, umeshapatikana mtaala utakaosaidia kufundisha wakunga kwa undani zaidi, masuala ya uzazi salama na anaongeza kuwapo huduma za dharura zitakazowasaidia wananchi, pale wanapotaka kujifungua.

Mtaalamu huyo, anaeleza kwamba kuwa na wakunga wenye sifa, wana nafasi ya kuwapunguzia mama na mtoto vifo kwa asilimia 60. Anasema, Dira ya Mpango wa Uzazi Kitaifa unatakiwa usonge kwa kuzuia asilimia 50, kutoka asilimia 30 za sasa.

### MAAZIMIO YA CAIRO

Ramadhan Hangwa, Mchambuzi wa Idadi ya Watu na Maendeleo kutoka UNFPA, anasema Mwaka 1994, mataifa 179 ikiwamo Tanzania yalikutana nchini Cairo na wakaibua Mpango wa Miaka 20, ambao mwanamke aliwekwa katika mpango kazi akitakiwa aangaliwe.

"Mpango kazi wa Cairo, ulitaka mambo matano yapewe msisitizo kutokana na kutokuwa na usawa katika dunia," anatamka, akiwa na ufafanuzi kwamba masuala yote ya kutokuwa na usawa, pia nchi zikuze uchumi kufikia hatua za maendeleo.

Katika hilo, mchambuzi anasema walijikita katika kuangalia elimu wakimuona mtoto wa kike aelimishwe, hasa katika ukanda nchi za Kusini mwa Jangwa la Sahara, ambako kuna changamoto ya ulipaji afya ya uzazi na kusababisha vifo.

Anasema mwaka 2019 walikutana jijini Nairobi, walikofanya tathmini miaka 25, baada ya mkutano wa Cairo, akisema tathmini ilionyesha watoto wengi wameanzishwa shule na kuongezeka shule za sekondari za kata.

Hata hivyo, Hangwa anaweka angalizo kwamba katika tathmini hiyo tajwa, bado kuna nchi zenye vifo vya kinamama vinavyotokana na uzazi vipo juu hasa katika ukanda Kusini mwa Jangwa Sahara.

Anasema, kuna mikasa ya watu wanaotoa mimba kwa njia isiyo salama, pia mimba za utotoni bado zipo na kuna

vijana wanaopata maambukizi ya Ukimwi, pia mimba zisizotarajiwa.

MAZINGIRA

SAFARI ILIYOKWISHAANZA KABLA....

# Mwekezaji nyumbani anaposafiri na ajenda tabianchi anayoitetea Rais mkutanoni Misri




Mkuu wa Mkoa wa Singida, Peter Serekumba, akizindua mradi wa kisima cha maji kijiji cha Kihanjo wilayani Itigi, mkoa Singida kilichofadhiliwa na SBL na Water Aid. Waliomzunguka ni viongozi, watendaji wa SBL na wadau wengine kwenye tukio hilo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU.**

**Na Frank Monyo**

HIVI sasa dunia inakabiliwa na changamoto ya mabadiliko ya tabianchi. Huko Sharm el-Sheikh nchini Misri, unaendelea Mkutano wa 27 wa nchi wanachama wa mkataba wa mabadiliko ya tabianchi, COP 27.

Katika siku ya pili ya mkutano huo ulioanza juzi na unatarajiwa kuhitimishwa Novemba 18 mwaka huu, Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa Antonio Guterres aliwakumbusha viongozi wa dunia wanaohudhuria mkutano huo, kwamba suluhu ya changamoto ya tabianchi iko mikononi mwao, hivyo ni wakati wa kuchukua hatua, hakuna muda wa kusubiri.

Pia, juzi usiku, Rais Samia Suluhu Hassan, naye alipopata fursa kuwasilisha mada kwa niaba ya nchi nyingine za dunia ya tatu, amegusa kwa mifano baadhi ya mambo na mifano inayogusa moja kwa moja maisha ya Kitanzania, maudhui yanayogusa kwa kifupi maeneo matatu makuu: Uwezeshwaji wa wanyonge kukabili adha hiyo ya tabianchi; kulinda vyanzo vya maji, na namna ya kufanikisha upatikanaji nishati mbadala katika hatua hiyo.

Ni ajenda ambayo ikiangaliwa kwa kina na kurejewa hatua zinazochukuliwa nchini na Kampuni ya Bia ya Serengeti kuhitimisha hayo matatu, imeshaanza siku nyingi kutekelezwa, katika sura inayojibu kilio cha mkuu wa nchi mkutanoni, aliyepaza sauti akiwaachia wajumbe kiulizo, alipowahoji:

"Swali la kujiuliza ni kuwa nchi kama Tanzania itapata wapi kiasi hiki cha fedha kwa ajili ya kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi?"

Ni hatua iliyofikiwa nchini kukiwepo pia sera na sheria inayoziweka taasisi binafsi na umma kushirikiana kwa maslahi mapana, inayojulikana kama PPP.

Vilevile, kabla ya kuelekea mkutanoni Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Dk. Seleiman Jafo, akatoa ufafanuzi wa Tanzania inakosimama, akishuhudia mabadiliko ya tabianchi yanavyoleta athari za moja kwa moja katika sekta za kilimo, ufugaji na upatikanaji majisafi na salama.

Katika hilo, anarejea uhalisia unaotawala wa sasa kuwapo mgawo wa maji sehemu mbalimbali, ikiwamo mikoa ya Dar es Salaam na Pwani ambako yeye ni mbunge, chanzo kikuu kikiwa kupungua kina cha maji katika Mto Ruvu.

Kwa mujibu wa Mamlaka ya Hali ya Hewa nchini (TMA), kuna tahadhari ya kuwepo upungufu wa mvua kwa mikoa 14 inayonyeshewa mara moja kwa mwaka katika mikoa ya Ruvuma, Mbeya, Rukwa, Njombe, Iringa, Lindi, Mtwara, Songwe, Katavi, Kigoma, Singida, Tabora, Dodoma na baadhi ya maeneo Kusini mwa mkoani Morogoro.

Uhalisia huo ndio unafungua tafsiri pana na iliyoanza siku nyingi kwa kinachofanywa na SBL, kutetea hifadhi ya rasilimali misitu na vyanzo vya maji, ambavyo hadi sasa imeshachimba jumla ya visima 24 katika mikoa kadhaa.

Anaitaja kuwa ni Iringa, Singida Kilimanjaro, Mwanza, Tanga, Ruvuma, Dar es Salaam, Pwani, Dodoma na Mara, ambako wameanza kuwasaidia wakazi wa maeneo hayo.

Mkurugenzi wa Mahusiano kwa Umma wa SBL, John Wanyancha, anasema katika kuiunga mkono serikali katika kukabili vita ya mabadiliko ya tabianchi na upatikanaji maji, imeshawezesha Watanzania zaidi ya milioni mbili wanaoishi katika sehemu zenye changamoto ya upatikanaji maji, wakipata ahueni.

Wanyancha, anasema katika mkutano wa mkataba wa mabadiliko ya tabianchi, COP 27unaoendelea hivi sasa nchini Misri, wao SBL wanaungana na serikali katika vita hivyo, wakipita katika mistari, ajenda na kanuni za kitaifa za kukabili athari mabadiliko ya tabianchi, kunusuru maisha ya umma, vilevile mtaji wa mwajiri mkuu kitaifa na sekta ya kilimo na mifugo.

Vilevile, anasema ni sehemu ya utekelezaji wajibu wa msingi wa wawekzaji wote kitaifa, kurejeshea umma sehemu ya faida inayopatikana kupitia huduma, inayojulikana kama 'corporate social responsibility'.

Wanyancha anafafanua kwamba ajenda ya kampuni yake imeyapa uzito majisafi na salama kama hitaji muhimu kwa maendeleo ya watu kupitia 'Corporate social responsibility' na ndio sababu iko mstari wa mbele kushirikiana na serikali na wadau kusaidiana.

Hapo anafafanua kwa vielelezo: "Ukiwa mkoani Singida, unagundua uhaba wa maji uliokuwa unaukabili mkoa huo kwa kipindi kirefu umepungua, unapojaribu kuwahoji wenyeji wanakwambia ni kwa sababu ya msaada wa visima vilivyochimbwa na SBL.

"Hii inanipa taswira kwamba, kama wadau wa maendelao pamoja na makampuni mbalimbali zikiungana kuisaidia serikali kuna uwezekano mkubwa nchi yetu ikaondokana na kero za maji, hata itakapotokea kuna mabadiliko ya tabianchi, pasina shaka hakutokuwa na madhara makubwa."

Kimsingi, ni hatua inayoshikamana na kauli ya hivi karibuni ya Waziri Mkuu Kassim Majaliwa alipozindua mradi wa visima saba vya maji vilivyopo Kisarawe II Kigamboni, akiielekeza Wizara ya Maji kushirikiana na sekta binafsi kuanzisha miradi ya uzalishaji maji, ili kukabili uhaba wa maji unaosababishwa kwa kiasi na mabadiliko ya tabianchi.

Rais Samia akiwa mkutanoni Misri, anasema Tanzania imepanga kupanda miti milioni 200 kila baada ya miaka mitatu, ambayo ikiangaliwa kwa kina ina uhusiano wa moja kwa moja na ustawi wa vyanzo vya maji, hali kadhalika, ubunifu na ulinzi wa mahitaji muhimu kwa binadamu, wanyama na mimea-maji.

**SAFARI IENDAKO**

Anasema kuwa moja ya kazi ya kampuni hiyo ni kuhakikisha watu wanapata maji safi na salama, na kazi yao ni kukarabati visima vilivyokufa pamoja na kuchimba vipya ikiwa ni juhudi za kupambana na uhaba wa maji ambao huchangiwa na mabadiliko ya tabia ya nchi.

Wanyancha anasema kuwa katika kipindi cha miaka 10 SBL imetumia zaidi ya shilingi bilioni 1.5 kufadhili miradi ya maji zaidi ya 23 sehemu mbalimbali hapa nchini.

"Hii miradi inaanzia ukarabati wa mabwawa, ujenzi wa visima na katika Wilaya ya Handeni tumejenga mabwawa matatu ambayo yanategemewa na wakazi wa vijiji vitatu.

"Lakini, mwaka 2020 kulitokea mafuriko na kingo za mabwawa hayo zilivunjika, wanakijiji walituomba tukarabati mabwawa hayo na sasa hivi tunaendelea na ukarabati mvua zikija maji yaweze kuingia," anasema Wanyancha.

Anasema kwa kunukuu taarifa ya taasisi ya Water Org inayowafanyia kazi ya upatikanaji maji na usafi wa vyoo, kwamba zaidi ya asilimia 57 ya Watanzania sawa na watu milioni 25 kati ya milioni 57, wanaweza kupata maji kupitia vyanzo vilivyoboreshwa, huku asilimia 30 tu wanaweza kuwapa huduma ya vyoo safi.

## JICHO LA MKUTANONI COP27...

# Vigogo waja na uamuzi wenye faraja kwa mazingira ya dunia

## • China na yake, vigogo tisa nao...

**Na Mwandishi Wetu**

CHINA ikiwa ni taifa kigogo nchini, sasa imeweka mpango mpya wa kudhibiti gesi aina ya methane, huku ikisisitiza haja ya kuwa na matumizi ya teknolojia mpya mbadala.

Hali kadhalika, nchi hiyo imeanika njia za kuifadhili katika juhudi za kupunguza ongezeko la gesi hiyo chafu, inayonasa joto mara 80 zaidi ya gesi ya kaboni.

Ofisa Mkuu wa Mazingira wa nchi hiyo, Xie Zenhua akizungumza pembezoni mwa Mkutano wa Umoja wa Mataifa wa Mazingira wa COP27 katika mji wa mapumziko wa Sharm El-Sheikh, amesema mpango huo mpya utaleta hatua madhubuti za kupunguza utoaji gesi ya methane kutoka kwenye nishati, kilimo na takataka.

Ni namna anayoitaja ya kukabiliana na gesi ya methane, ikiwa ni sehemu kuu ya juhudi za dunia za kudhibiti ongezeko la nyuzi joto 1.5 kutoka kwenye kilimo, huku takribani nchi 40 zikitarajiwa kuanika mipango yake ya kuidhibiti gesi hiyo, katika kikao hicho kikubwa katika historia ya harakati za kukabili mazungira na hali ya hewa duniani, huko jijini Sharm El-Sheikh.




**MATAIFA MAKUBWA**

Wakati China inachukua hatua hiyo mataifa tisa makubwa duniani nayo yamejiunga katika umoja wa kuzalisha nishati kwa njia ya upepo wa bahari.

Katika orodha hiyo, kuna nchi zilizojitambulisha; Uingereza, Ujerumani, Marekani na Japan, zikitangaza kujiunga na muungano wa uendelezaji nishati ya upepo wa mawimbi ya bahari, kwa jina la GOWA.

Ni muungano ulioasisiwa kwa lengo la kuondosha vikwazo vya kupata nishati. Awali, ulianzishwa na Shirika la Kimataifa la Nishati Jadidifu (IRENA) Denmark na Baraza la Nishati ya Upepo Duniani.

Mataifa mengine yaliyojiunga na muungano huo Jumatatu wiki hii ni Ubelgiji, Colombia, Ireland, Norway na Uholanzi.

IRENA na Shirika la Nishati Duniani (IEA) zinatabiri kwamba kufikia mwaka 2050, nishati itokanayo na upepo bahari itakuwa maradufu kwa kiwango cha jigawati 2000 kutoka 60 za sasa, hatua inayotajwa itasaidia kuzuia kupanda kwa joto kwa zaidi ya nyuzi 1.5 za kabla ya zama za viwanda.

**MAKUBWA YA ULAYA**

Mjumbe wa Mabadiliko ya Tabianchi wa Ujerumani, Jennifer Lee Morgan, ambaye nchi yake ni ya tatu kwa kuzalisha nishati hiyo duniani, anafafanua kuna mipango ya kuongeza pakubwa utowaji wa nishati ya upepo wa mawimbi ya bahari.

"Bahari ya Kaskazini itageuka kuwa mtambo mkubwa kabisa na endelevu wa kuzalisha umeme na kuchukua nafasi ya gesi na mafuta kwa haraka," anasema Waziri wa Nishati wa Ubelgiji, Tinne Van der Straeten.

**UINGEREZA & MKOPO NAFUU**

Katika hatua nyingine, Uingereza inasema inapanga kutoa mikopo mipya kuzisaidia nchi zilizoathirika zaidi kwa majanga yatokanayo na mabadiliko ya tabianchi.

Wizara ya Fedha ya Misri, mwenyeji wa mkutano, inasema taarifa yake ya sasa ni kwamba mikopo hiyo itajumuisha kipengele kinachowaruhusu wakopeshwaji kuacha kulipa madeni yao endapo nchi zitakuwa zimekumbwa na majanga hayo.

Shirika la Ukopeshaji Nje wa Uingereza (UKEF), ndicho chombo kilichokabidhiwa jukumu la mikopo hiyo, inayotolewa kwa mataifa yenye kipato cha chini, pia himaya ya visiwa vidogo.

Wizara ya Fedha ya Uingereza inasema kwamba, taarifa za kina juu za mpango huo zitatolewa kwenye mkutano huu wa COP27 unaoendelea sasa.

"Nina fahari kusema kwamba, Wakala wa Ukopeshaji wa Nje wa Uingereza, ndiyo wa mwanzo kabisa duniani kutoa mikopo ambayo itasitisha malipo ya huduma ya madeni kwa nchi zinazokumbwa na majanga ya tabianchi na ya kimaumbile," anaeleza Naibu Waziri wa Fedha wa Uingereza, James Cartlidge.

Shirika la Mazingira barani Ulaya (EEA) linasema kuwa mabadiliko ya tabianchi yamegeuka kitisho kikubwa, kwa afya na mustakabali wa binadamu, ukitaja kiwango kikubwa cha joto, mafuriko na moto unaowaka misituni, kugeuka uhalisia wa maisha ya sasa.

Katika taarifa yake iliyotolewa kwenye siku ya tatu ya mkutano wa sasa wa tabianchi unaoendelea nchini Misri, shirika hilo linasema kulikuwapo idadi kubwa ya vifo kwenye majira ya kiangazi ya mwaka huu barani Ulaya, vilivyotokana na kuongezeka joto.

"Idadi hii inaweza kuongezeka endapo hakutakuwa na hatua za uhakika kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi," linatamka shirika hilo, katika taarifa yake.

***Kwa mujibu wa taarifa za kimataifa.***


---

Dondoo: Kulia
1. Nairobi ni mji wake mkuu
3. piga ramli 5. Shikwa
9. eleza 11.mzazi wa kiume
12.tengeneza kitu
13.nyuzi zinazotokana na viwavi vya nondo 15.idadi ya watumishi inayohitajika katika idara
17.funga nikaha 19.daima
21.desturi 23.kauli aitoayo mtu juu ya mali zake kabla ya kufa
25.kauka kwa nguo iliyofuliwa
26.Ijapokuwa

Chini:
1. kinyume cha dada
2. tarakimu
3. heshima 4. karo ya shule
6. pengine 7. fedheheka 8. tarabu
10.zao la mti itumikayo kujengea
13.kasirika ghafla 14.madhubuti
16.Mwanaume wa kwanza
18.vunja kanuni za nchi
20.alka mtu kwako
22.omba ruhusa ya kuondoka
24.yenye kuishi

**CHEMSHABONGO NA -00 20 00-**


Na Felix Magezi
felixmagezi@gmail.com




Kamilisha jedwali kwa kujaza maneno yafuatayo:

UTAKATIFU
THAMANI
DAMU
MBABANE
AGUA
ANWANI
GAIDI
KUJIKWAA
MTUMWA
DHANA
UHABA
LIBERIA
ANGUKIA
IDADI

DUA
JUA
BIA
MKUU
MAMA



Majibu toleo lililopita





# Washauriwa kupanda mazao yanayostahimili ukame

**Na Grace Mwakalinga,** SONGWE

WAKULIMA wa Wilaya za Momba na Songwe, wameshauriwa kupanda mazao kama maharagwe na mtama ili kukabiliana na hali ya ukame.

Kauli hiyo ilitolewa jana na Katibu Tawala Msaidizi Idara ya Kilimo, Vanscar Kulanga, alipozungumza na wakulima wa wilaya hizo ikiwa ni sehemu ya maandalizi ya msimu mpya wa kilimo.

Alisema miongoni mwa mazao wanayopaswa wakulima wasiyapuuze ni maharagwe na mtama ambayo kwa kiasi kikubwa yanahimili mabadiliko mbalimbali ya hali ya hewa na yanasaidia kukidhi mahitaji yao ya kila siku.

Alisema kwa sasa dunia inakabiliwa na tatizo la mabadiliko ya tabianchi na kusababisha ukame na hatari ya njaa.

"Hali ya kiangazi inaweza kusababisha baa la njaa katika jamii, mbali na kupanda mazao kama vile mahindi, mpunga lakini mazao kama alizeti, maharagwe na mtama ambayo yanahimili hali zozote za hewa ni muhimu yakapandwa," alisema Kulanga.

Aliongeza kuwa katika kuhakikisha msimu wa kilimo wakulima wanapata taarifa za kupanda mazao na matumizi sahihi ya pembejeo, amewasisitiza maofisa ugani katika kila kijiji kuwatembelea ili kuwapatia elimu ya kilimo bora.

Athuman Kalago mmoja wa wakulima katika kijiji cha Kilimampimbi, alisema kukosekana kwa mvua za uhakika katika ukanda huo kumeleta hofu kwa jamii lini waanze kupanda.

Aidha, aliwasisitiza wakulima wenzake kuendelea kufuatilia taarifa za utabiri wa hali ya hewa ili kujua ni lini muda sahihi wa kupanda mazao yao pamoja na kuzingatia ushauri wa wataalamu wa maofisa ugani.

Hivi karibuni, Mkuu wa Mkoa wa Songwe Waziri Kindamba, aliwataka wananchi kutouza chakula chote kutokana na tishio la ukame.

# Zaidi wanafunzi 300 hawakufanya mtihani wa darasa la saba Rungwe

**Na Grace Mwakalinga,** RUNGWE

WANAFUNZI 337 kati ya 7,404 wa shule za msingi wilayani Rungwe, hawakufanya mtihani wa kuhitimu darasa la saba mwaka huu kutokana na sababu mbalimbali zikiwamo mimba na utoro.

Kwa mujibu wa Diwani wa Viti Maalum Kata ya Kyimo, ambaye ni Mwenyekiti wa Kamati ya Elimu na Afya, Emmy Masseta, wamebaini hali hiyo baada ya kufanya ufuatiliaji wa maendeleo ya wanafunzi shuleni.

Alisema miongoni mwa sababu zilizochangia idadi hiyo ya utoro na mimba ni usimamizi hafifu wa walimu wakuu wa shule pamoja na kutowajibika ipasavyo katika kufuatilia mienendo ya wanafunzi wao.

Aidha, wazazi na walezi wametupiwa lawama kuhusika na tatizo hilo ikielezwa kuwa wamejikita zaidi kwenye shughuli za uzalishaji mali na kusahau kufuatilia maendeleo ya watoto wao shuleni.

**Tusimamie misingi ya ufundishaji ili wilaya yetu ifanye vizuri, wasiwapo watoto wanaoishia njiani, kama kuna kikwazo ofisi yangu iko wazi njoo tuyajenge.**

"Tayari hatua mbalimbali zimechukuliwa ikiwamo kutengua uteuzi wa baadhi ya wakuu na wengine kuwahamisha vituo vya kazi na kuwaandikia barua za onyo ili kuondokana na hali hiyo," alisema Masseta.

Naye Diwani Kata ya Kiwira, Saimon Michael, alisema tatizo lingine linalochangia utoro na mimba kwa wanafunzi ni baadhi ya walimu kujiingiza kwenye masuala ya vita ya kisiasa baina yao na wazazi wa wanafunzi badala ya kuzingatia Sera ya Elimu inavyoelekeza.

"Waheshimiwa madiwani kundi la watoto ambao hawajahitimu elimu ya msingi ni kubwa ni jukumu letu kusimamia imara kuwa na mikakati ya pamoja kufuatilia walimu ambao hawafanyi kazi kwa wito na kujiingiza kwenye masuala ya kisiasa," alisema Michael.

Diwani wa Kata ya Bujela, Abraham Mwankenja, aliiomba serikali kujenga shule maalum kwa ajili ya elimu kwa watu wasiojua kusoma na kuandika kutokana na kuwapo na kundi kubwa mitaani.

Alisema hatua hiyo itasaidia kundi hilo kupata elimu na maarifa ambayo yatawasaidia kuepukana na vitendo mbalimbali vya uhalifu.

Mkuu wa Wilaya ya Rungwe, Dk. Vicent Anney, aliwataka walimu kurejea kwenye sera ya elimu na kuweka mikakati ya kuhakikisha idadi ya wanafunzi wanasajiliwa wanahitimu elimu ya msingi kwa mwakani.

"Tusimamie misingi ya ufundishaji ili wilaya yetu ifanye vizuri, wasiwapo watoto wanaoishia njiani, kama kuna kikwazo ofisi yangu iko wazi njoo tuyajenge," alisema Dk. Anney.



Wakazi wa Kijiji cha Luteba, Halmashauri ya Busokelo, wilayani Rungwe, mkoani Mbeya, wakishuhudia kufukuliwa kwa kaburi lililokuwa na mwili wa Neema Mlomba, aliyefariki kwa matatizo ya uzazi. **PICHA: GRACE MWAKALINGA**

# Wahitimu vyuo vikuu Katoliki waonywa kujihusisha ushoga

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

ASKOFU Mkuu wa Jimbo Kuu la Mwanza, ambaye ni Mwenyekiti wa Baraza la Wadhamini wa Vyuo Vikuu vya Katoliki nchini, Renatus Nkwande, amewashauri wanafunzi wa elimu ya juu kutojiingiza kwenye vitendo vya ushoga na tabia nyingine zinazohatarisha maisha yao na badala yake wazingatie masomo na kumcha Mungu.

Nkwande alitoa kauli hiyo jana alipofungua mwaka mpya wa masomo 2022/23 na kubariki majengo ya Chuo Kikuu Kishiriki cha Kikatoliki Mbeya (CUCoM).

Alisema ni vyema wanafunzi hao wakaepuka tabia hatarishi kwa mustakabali wa maisha yao kama vile ushoga ambao kwa sasa umezidi kushamiri duniani badala yake waishi maisha ya kumcha Mungu na kujikita kwenye masomo ili kufanikisha ndoto za maisha yao.

"Tunashuhudia vijana wetu wakiharibikiwa kutokana na mambo haya ya ushoga, mtindo wa maisha umechangia vitendo hivyo kushamiri bado tunayo nafasi ya kukomboa kizazi hiki kwa kuwafundisha maisha ya kumcha Mungu pamoja na elimu ya dunia, lakini nawasihi vijana wangu epukeni kuiga maisha ya mtu ukitambua umekuja chuoni kufanya nini basi hautakuwa mtu wa makundi," alisema Nkwande.

"Suala la ushoga limekuwa la kawaida vijana hawaogopi tena tofauti na enzi zetu tulikuwa tukisikia hata hilo neno tunakimbia, mtindo wa maisha umechangia vitendo hivyo kukua na kuenea kwa kasi, naamani bado tunayo nafasi ya kumuomba Mungu atuepushe na tabia hii.

Kwa upande mwingine Askofu Nkwande aliwapongeza watumishi wa Chuo cha CUCoM kwa jitihada za kuhakikisha wanawapatia wanafunzi elimu ya kiroho na darasani kwa ajili ya kutimiza malengo waliyojiwekea.

Alisema ni miaka tisa sasa tangu kuanzishwa kwa chuo hicho mkoani Mbeya na mambo mengi yamefanyika ikiwamo kukuza uchumi wa wakazi wa jiji hilo lakini kuwawezesha vijana nchini kutimiza ndoto za maisha yao kupata elimu.

Alisema jitihada hizo zinaunga mkono nia ya serikali ya kuwapatia elimu wananchi wake katika maeneo mbalimbali nchini ikiwamo kuwajengea ujuzi na maarifa ili kukabiliana na soko la ajira ndani na nje ya nchi.

Makamu Mkuu wa Chuo cha CUCoM, Prof. Romuald Haule, alisema wamejipanga kuwafundisha na kuwaandaa wanafunzi kukidhi mahitaji ya soko la ajira.

Alisema katika kufanikisha hayo chuo hicho kimekuwa na utaratibu wa kufanya tathmini na kutoa semina elekezi kwa wahadhiri ili kukumbushwa mambo ya msingi kwa ajili ya kutoa elimu kwa wanafunzi wapya waliodahiliwa.

Aliwahakikishia viongozi wa Kanisa Katoliki nchini kuwa chuo hicho kitakuwa miongoni mwa vyuo vikuu nchini vinavyotoa elimu bora ambayo inawaandaa wanafunzi kujiajiri na kuajiriwa.

Aliwataka wanafunzi wote kujitambua na kuzingatia kilichowapeleka chuo kikuu na kamwe wasiingize kwenye tamaa za kidunia ambazo mwisho huharibu ndoto zao.

"Hapa chuoni tunalo bomu, usikubali hilo bomu likulipukie wewe kwa sababu tu umeshindwa kujitambua na kufuata mambo yasiyokuhusu," alisema Prof. Haule na kuongeza kuwa chuo hicho kina wanafunzi wa aina zote ambao wametimiza miaka 18 na ambao bado hawajatimiza.





# Maofisa maendeleo watakiwa kuchochea kasi ya maendeleo

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

MAOFISA Maendeleo ya Jamii wametakiwa kujipanga kwenda na kasi ya serikali ili kuchochea maendeleo ya jamii sambamba na sera, mikakati, sheria na miongozo mbalimbali.

Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Dk. Dorothy Gwajima, aliyasema hayo juzi jijini hapo alipokuwa akifungua kikao kazi cha maofisa hao wa sekretarieti za mikoa na Wakuu wa Idara za Maendeleo ya Jamii wa Mamlaka za Serikali za Mitaa.

Dk. Gwajima alisema, serikali ina matumaini makubwa na mchango wa kada hiyo na itahakikisha inafanya uwezeshaji ili kwenda na kasi iliyokusudiwa.

"Rais Samia Suluhu Hassan anatambua umuhimu wa Sekta ya Maendeleo ya Jamii katika kuiwezesha jamii kushiriki kujiletea maendeleo kwa kutumia rasilimali mlizonazo hivyo kuwa kitovu cha maendeleo.

**Maofisa Maendeleo ya Jamii, muda wa kuambiana umepita kila mmoja asimame vyema fanyeni kazi na wadau, kila mnachopanga mpange na wadau.**

"Na ndiyo maana amechukua hatua ya kuunda wizara mama ya sekta hii na mambo mengi mazuri yanakuja," alisema Dk. Gwajima.

Akielezea umuhimu wa kada ya maendeleo ya jamii kwenye sekta zote aliwapongeza kwa kazi nzuri wanayofanya katika kuwezesha mapambano ya kutokomeza ukatili wa kijinsia kwa watoto.

Aliwakumbusha Maofisa Maendeleo ya Jamii masuala yanayotekelezwa na serikali na kuyasimamia ikiwamo majukwaa ya uwezeshaji wananchi kiuchumi, utekelezaji wa ahadi za nchi kupitia Jukwaa la Kizazi Chenye Usawa Tanzania ikiwa kinara wa eneo la haki na usawa wa kiuchumi, pamoja na programu ya malezi na makuzi ya watoto kwa kutoa mafunzo ya malezi chanya kwa wazazi na walezi.

Katibu Mkuu wa wizara hiyo, Dk. Zainab Chaula, aliwataka maofisa hao kutimiza majukumu yao kulingana na mipango iliyowekwa na sheria zilizoko.

"Maofisa Maendeleo ya Jamii, muda wa kuambiana umepita kila mmoja asimame vyema fanyeni kazi na wadau, kila mnachopanga mpange na wadau," alisisitiza Dk. Chaula.

Mwakilishi wa Ofisi ya Rais TAMISEMI, Naibu Katibu Mkuu, Ramadhami Kailima alisema, Maofisa Maendeleo ya Jamii ndio wasimamizi na watekelezaji na kuwahimiza watumie mikutano ya mkoa na wilaya kuzungumzia majukumu yao.

Mkurugenzi shirika lisilo la kiserikali la kutetea haki za wanawake na watoto la Kivulini, Yasin Ally, alisema nchi haiwezi kufanikiwa bila kuwekeza kwenye Maendeleo ya Jamii.

Aliwahimiza maofisa hao kuthibitisha uwepo wao kwenye maeneo yao na kuiomba Ofisi ya Rais TAMISEMI kutoa Mwongozo wa Ulinzi na Usalama wa Mtoto na kuwapo mpango kazi utakaowezesha kukutana na makundi maalum.




Waziri wa Mambo ya Ndani, Mhandisi Hamad Masauni (katikati), akizindua Mfumo wa Usajili na Usimamizi wa Jumuiya (RSMIS), jijini Dodoma, jana. Mfumo huo, utasaidia kuwezesha wananchi kuwasilisha maombi ya usajili wa taasisi, vyama na vikundi vyenye sifa ya kusajiliwa kuwa jumuiya bila kulazimika kufika katika Ofisi ya Msajili wa Jumuiya. Wa pili kushoto ni Kaimu Katibu Mkuu wa Wizara, Dk. Maduhu Kazi na (kushoto) ni Msajili wa Jumuiya, Emmanuel Kihampa. **PICHA: WMNN**

# Polisi yaanza msako wanaolawiti wanafunzi

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

JESHI la Polisi mkoani hapa limeanza msako kwa wanafunzi na raia wanaotumika kulawiti watoto ili kukomesha tabia hiyo.

Msako huo umeanza baada ya jeshi hilo kupata taarifa kuhusu mwanafunzi wa miaka (14), kulawiti wenzake ikiwamo kuwaonyesha video za ngono.

Kamanda wa Polisi mkoani Dodoma, Martine Otieno, alisema vitendo hivyo ni haramu hivyo Jeshi la Polisi limeingilia kati ili kukomesha tabia hizo.

"Jeshi la Polisi linahitaji kukomesha tabia hiyo ndio maana tumeanza msako katika maeneo mbalimbali hapa Dodoma," alisema Kamanda Otieno.

Alisema tukio la awali limetokea mtaa wa Mathias ulioko Mailimbili mkoani hapa.

Hivi karibuni Balozi Jackson Kadege wa Mtaa wa Mailimbili, Kata ya Miyuji, aliiomba serikali kuingilia kati suala la watoto kulawitiana katika mtaa huo.

Tukio hilo limetokea juzi jijini hapo baada ya watoto saba kulawitiwa na mtuhumiwa aliyejulikana kwa jina la Musa baada ya kuwakusanya nyumbani kwao huku akiwaonyesha filamu za ngono.

Balozi Kadege alisema baada ya kuhoji watoto waliofanyiwa tukio hilo walisema wamekuwa wakifanyiwa na wao kufanya kwa wengine.

"Tunaomba serikali iingilie kati suala hilo ili kuhakikisha watoto wa kiume wanakuwa salama na suala hilo ambalo ni tishio," alisema Kadege.

Balozi Kadege alisema lengo lao ni kuona jamii inakuwa sawa katika suala hilo ambalo linahitaji ufumbuzi wa haraka.

Aisha Hida, alisema mtaani kwao kumeharibika kutokana na watoto kulawitiana kitendo ambacho ni kinyume na maadili ya kiafrika.

Alisema wanaomba serikali iwasaidie katika hilo kwa sababu vitu hivyo vinaanza wakiwa wadogo na visipokemewa vitaendelea kufanyika kwa jamii.

# Idadi ya watoto waliokosa elimu ya awali yaongezeka

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

IDADI ya watoto waliokosa fursa ya kusoma elimu ya awali katika Mkoa wa Rukwa, Simiyu na Pwani imeongezeka katika vituo vya utayari wa kumwandaa mtoto kwenda shule sababu kubwa ikitajwa ni mwitikio mkubwa wa jamii kwenye mpango huo.

Hadi kufikia Novemba 4, 2022, Mkoa wa Pwani una zaidi ya watoto 1,200, Simiyu 1,600 huku Mkoa wa Rukwa ukiongoza kwa kuwa na zaidi ya watoto 2,000 katika vituo vya utayari.

Hayo yalibainishwa na washiriki wa Mafunzo ya SRP kutoka katika mikoa ya Pwani, Rukwa na Simiyu yaliyomalizika juzi, jijini Dodoma.

Ofisa Elimu Taaluma wa Halmashauri ya Wilaya ya Itilima, John Mpamwa, alizitaja sababu za ongezeko hilo kuwa mwitikio mkubwa wa wazazi kwa kuchukua hatua na kuwapeleka watoto katika vituo hivyo ili waweze kuandaliwa kwa ajili ya kuanza darasa la kwanza mwakani.

Mratibu wa shule bora kutoka Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Winfrid Chilumba, alisema ongezeko hilo ni moja ya mafanikio ya awali ya Mpango wa Utayari.

Alisema kuwa sio tu idadi ya watoto imeongezeka, lakini watoto wenye umri zaidi ya miaka sita waliokosa fursa ya kusoma elimu ya awali wamejitokeza kwa wingi katika vituo ukizingatia mpango huo ulilenga hasa watoto wenye miaka minne hadi sita.

Naye Mtaalamu Kiongozi anayesimamia eneo la ujifunzaji na ufundishaji kutoka katika Mradi wa Shule Bora, Vicent Katabarwa, alisema mikoa hiyo mitatu imetumika kama majaribio.

Alisema lengo ni kuona mafanikio yanayopatikana katika mikoa hiyo mpango wa utayari utatekelezwa katika maeneo mengine ambayo shule bora inahudumia.

Kadhalika, alisema tathmini ya utekelezaji wake itafanyika katika ngazi tatu, moja halmashauri husika itafanya ufuatiliaji kuona jinsi watoto wanavyojifunza, pili viongozi wa kitaifa watatembelea vituo vya utayari na kufanya tathmini na tatu ni idadi ya wanafunzi watakaoanza darasa la kwanza mwaka 2023, ambao wamepitia katika mpango huo.





# Kikwete kuzindua ripoti jinsia Afrika

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

RAIS mstaafu, Jakaya Mrisho Kikwete, leo anatarajiwa kuzindua ripoti ya ufuatiliaji wa maazimio ya mkutano uliofanyika Nairobi mwaka 2019 uliojadili mambo mbalimbali ikiwamo udhalilishaji wa kijinsia.

Ripoti hiyo inatarajiwa kuzinduliwa katika hoteli ya Melia Mkoa wa Kaskazini Unguja na kuhudhuriwa na viongozi waandamizi 29, wakiwamo aliyekuwa Gavana Mkuu wa Canada, Michaelle Jean na Prince Mary Elizabeth kutoka Denmark.

Akizungumza na waandishi wa habari jana mjini hapa katika warsha maalum, Mwakilishi Mkazi wa Shirika la Umoja wa Mataifa la Idadi ya Watu (UNFPA), Mark Bryan Schreiner, alisema ripoti hiyo ni sehemu ya ufuatiliaji wa maazimio yaliyofikiwa mwaka 1994 katika mkutano wa Cairo, Misri.

**Mambo mingine yaliyozungumzwa ni mikakati ya kupambana na vifo vinavyotokana na uzazi ikiwamo kuwapo kwa huduma bora za kisasa za afya katika hospitali.**

Alisema katika mkutano wa Nairobi uliohudhuriwa na viongozi wa nchi 173, iliundwa kamisheni kwa ajili ya kufuatilia mambo mbalimbali yaliyokubaliwa katika mkutano wa Cairo ambao ulijadili masuala ya mpango wa kumwezesha mwanamke kupambana na udhalilishaji wa kijinsia na usawa wa kijinsia.

Pia alisema mambo mingine yaliyozungumzwa ni mikakati ya kupambana na vifo vinavyotokana na uzazi ikiwamo kuwapo kwa huduma bora za kisasa za afya katika hospitali.

Alisema kamisheni imeundwa kwa ajili ya kufuatilia mambo yote hayo ambayo yamekuwa kikwazo na kurudisha nyuma juhudi za makundi hayo kupiga hatua kubwa ya maendeleo ikiwamo utashi wa serikali kuwapa nafasi wanawake kushika nafasi za uongozi wa juu.

Akiwasilisha mada kwa waandishi wa habari kuhusu malengo ya Tanzania katika utekelezaji wa ahadi za mkutano wa Nairobi, Ofisa Mwandamizi anayeshughulikia masuala la idadi ya watu, Ramadhan Hangwa, alisema bado utafiti unaonyesha kwamba vifo vya kinamama na watoto vinaendelea kuathiri kundi kubwa la wanawake na watoto pamoja na mimba za utotoni.

"Utafiti wetu unaonesha katika nchi zilizoko kusini mwa Afrika, tatizo la mimba kwa watoto na vifo ni kubwa. Kwa mfano Tanzania katika vizazi hai 100,000 vifo vya watoto ni 5,566 ambapo kwa upande wa mimba kwa wanawake wasichana kati ya wanawake.

Mratibu wa ufuatiliaji wa mkutano huo, Saskia Schellekens, alisema mkutano pia utajadili mambo mbalimbali yanayohusu afya ya uzazi ambayo yamepewa kipaumbele katika ripoti hiyo ili kupunguza idadi ya vifo vya uzazi hadi kufikia asilimia sifuri, ukatili wa kijinsia pamoja na kumwezesha mwanamke.

Alisema kutokana na tathmini iliyofanywa katika mkutano uliofanyika Cairo, vifo vya kinamama vitokanavyo na uzazi bado viko juu huku akibainisha kuwa kwa Tanzania katika kila vizazi hai 100,000, wanawake 556 hufariki dunia kutokana na uzazi.

## Mwinyi ahimiza uhifadhi bahari kukuza uchumi

**Na Mwandishi Wetu,** ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, amesema uhifadhi wa mazingira ya bahari unapaswa kufanyika kwa kuwawezesha wananchi ili kupunguza umaskini na kuleta usawa wa kijamii.

Dk. Mwinyi (pichani chini) alisema hayo juzi katika kongamano la saba la ujumuishi, utu na uwekezaji lililofanyika Hoteli ya Golden Tulip, Zanzibar.

Alisema uhifadhi wa mazingira ya bahari ni muhimu katika kufanikisha dhana ya matumizi bora ya rasilimali za sekta za uchumi wa buluu, unaohusisha utalii, viwanda vya rasilimali za baharini, ufugaji wa samaki, uvuvi, mafuta na gesi asilia.

Alisema ni muhimu katika uhifadhi wa mazingira bahari kufuata miongozo ya ulimwengu kama vile mwenendo wa sera pamoja na mabadiliko ya tabianchi.

Dk. Mwinyi alisema baada ya kuibuka kwa ugonjwa wa UVIKO-19, dunia imeelekeza nguvu katika ukuzaji wa shughuli za kiuchumi wa bahari na hivyo kubadili mandhari ya uchumi wa dunia, ambapo hali hiyo haitokani na msukumo wa washirika wa maendeleo bali kutokana na michango ya mifuko mbalimbali pamoja na sekta binafsi.

Akigusia kaulimbiu ya Kongamano hilo isemayo 'Mjadala Kuhusu Uchumi wa Buluu katika Afrika', alisema inaakisi dhamira ya kutoa msukumo katika kuleta mageuzi ya kiuchumi kupitia sekta ya uchumi wa buluu barani Afrika ili kuwa uwekezaji endelevu.

Rais alisema anaunga mkono mpango huo utakaoshirikisha teknolojia, sera, kinamama pamoja na vijana, kwa kuelewa kuwa ni chachu ya kuleta mabadiliko katika sekta ya uchumi wa buluu na kusema mpango huo ni mwelekeo bora katika kuibadili Afrika ili iwe na uchumi imara.



Alitumia fursa hiyo kuwashajihisha washiriki wa kongamano hilo kutembelea vivutio vya utalii viliopo nchini, baada ya kukamilisha mkutano huo.




Mratibu wa ufatiliaji wa maazimio ya kongamano la kimataifa la idadi ya watu na maendeleo (ICPD 25) kutoka Shirika la Umoja wa Mataifa la Idadi ya Watu Duniani (UNFPA), Saskia Schellekens, akizungumza na waandishi wa habari, jijini Zanzibar jana, kuhusu uzinduzi wa ripoti ya ufuatiliaji wa maazimio hayo uliofanyika Nairobi mwaka 2019 ambao ulijadili mambo mbalimbali ikiwamo idadi ya watu. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

## Ataka elimu zaidi chakula bora

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

NAIBU Katibu Mkuu Wizara ya Kilimo Maliasili na Mifugo, Dk. Omar Ali Amiri, amesema elimu zaidi inahitajika ya ulaji chakula bora (mlo kamili) kwa jamii ili kuondoa tatizo la upungufu wa lishe.

Aliyasema hayo jana katika kikao cha kujadili ripoti ya kitaalamu ya matumizi ya chakula katika hoteli ya Zanzibar Beach Resort, Mazizini mjini hapo.

Dk. Omar alisema Wizara ya Kilimo, Maliasili na Mifugo inasaidia wakulima kulima kilimo chenye tija ambacho kitazalisha chakula chenye lishe kwa kuweka uangalizi wa kitaalamu wakati wa upandaji na uvunaji.

"Tunawawezesha wakulima namna ya uzalishaji bora wa chakula kama serikali ilivyoanza na wakulima wa mpunga kuwapa namna bora ya umwagiliaji ili kupatikana chakula bora," alisema.

Serikali ya Zanzibar, ilisema imewawekea mazingira mazuri ya umwagiliaji wakulima wa mpunga, mboga na matunda ili chakula kitakachopatikana kiwe katika hali ya usalama kwa watumiaji.

Alisema lengo la kikao hicho ni kuangalia takwimu zinazoonyesha hali ya chakula kwa Zanzibar na njia za kufanya ili kuondoa uhaba wa chakula.

Naye mwakilishi kutoka Idara ya Uhakika wa Chakula Zanzibar, Ahmed Gharib Khamis, alisema asilimia 25 ya watu wa Zanzibar wana hali ya chini ya upatikanaji wa chakula, hivyo kupitia kikao hicho wataangalia namna ya kuisaidia jamii kupata chakula kwa kuungana na wadau mbalimbali wa masuala hayo.

Mwakilishi kutoka Shirika la Chakula na Kilimo (FAO), Charles Tulahi, alisema chakula ni afya, hivyo ni vyema jamii ikapewa elimu ya namna ya ulaji wa vyakula ili kupata lishe bora.

Mkurugenzi wa Sera na Mipango Wizara ya Kilimo Tanzania, Obadiah Nyagiro, alisema hali ya udumavu wa lishe nchini ni asilimia 30 katika baadhi ya mikoa, hivyo ni vyema kikao hicho kikaweka mikakati imara itakayosaidia kupunguza au kuondosha kabisa tatizo hilo.





# Walimu wa4 wafukuzwa kazi kwa kughushi vyeti

**Na Mathias Marwa,** TARIME

TUME ya Utumishi wa Walimu (TSC) imewafukuza kazi walimu wanne na wengine watano kupewa onyo wilayani hapo kutokana na makosa mbalimbali ikiwamo kughushi vyeti.

Katibu Msaidizi wa TSC wilayani Tarime, Agutu Christopher, amewataja waliofukuzwa kwa kosa la kughushi vyeti kuwa ni Mary Muniko wa Shule ya Msingi Bisarwi na Magdalena Mwanyika wa Shule ya Msingi Tumaini.

Alisema walimu wengine walifukuzwa kwa makosa ya utoro na kughushi vyeti ambao ni Editha Lusumbo wa Shule ya Msingi Buguti na Tabani Daniel wa Shule ya Msingi Kenyamanyori.

**Walimu wengine wawili walipewa onyo kutokana na makosa ya utoro ambao ni Nyamanche Kulwa wa Shule ya Msingi Kikomori na Phinias Malingumu wa Shule ya Msingi Kemakorere.**

Akizungumza ofisini kwake juzi, Christopher alisema walimu wengine wawili walipewa onyo kutokana na makosa ya utoro ambao ni Nyamanche Kulwa wa Shule ya Msingi Kikomori na Phinias Malingumu wa Shule ya Msingi Kemakorere.

"Walimu watano bado mashauri yao yanasikilizwa likiwamo la Victoria Jonas aliyekuwa Mkuu wa Shule ya Sekondari ya Manga ambaye anakabiliwa na mashtaka ya rushwa na uhujumu uchumi katika Mahakama ya Wilaya ya Tarime.

Christopher aliwataja walimu wengine wa shule za sekondari ambao pia mashauri yao yanaendelea kusikilizwa kuwa ni Meremo Marwa wa Shule ya Kibasuka na Musa Nzugilwa wa shule ya Muriba.

Wengine kutoka shule za msingi katika mabano ni Dorin Mushi (Mangucha), Zephania Magesa (Mturu) na Juma Makuri (Buguti). Alisema mashauri hayo ni ya kati ya Mei 5, 2018 na Septemba 8, mwaka huu.



Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Maendeleo kwa viziwi Tanzania, Kelvin Nyema (kulia aliyesimama), akizungumza katika ufunguzi wa mafunzo ya lugha za alama kwa wanafunzi na wakufunzi wa Chuo cha Afya Sumbawanga, mkoani Rukwa jana, chini ya ufadhili wa Taasisi ya Nos Vies en Partage (NVep) inayofadhiliwa na Rais na Ofisa Mtendaji Mkuu wa Kampuni ya Barrick Gold Corporation, Mark Bristow. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Watakiwa kupaza sauti ushirikishwaji uchimbaji wa madini

**Neema Emmanuel,** MWANZA

WANAWAKE wanaojishughulisha katika uchimbaji mdogo wa madini, wametakiwa kuwa na sauti ya kujisemea ili kuondokana na kizingiti kinachowakwamisha katika shughuli za uchimbaji.

Akizungumza na mwandishi wa habari hii juzi, Meneja Mradi na Utafiti wa Taasisi ya Kuendeleza Uchimbaji Mdogo (FADev), Evans Rubara, alisema kinachohitajika katika kuwa na maendeleo endelevu ni wao kuwa na sauti na kujisemea.

Rubara alisema kikubwa kinachohitajika ni wanawake kuwa na sauti na kujisemea kwa kuwa kinachosababisha wanawake waonekane kuwa ni wachache katika sekta hiyo kwa vile hawawezi kujisemea licha ya kuwapo kwa vyama vya wanawake wachimbaji wa madini.

Alisema mila na desturi hususan katika maeneo hayo ya uchimbaji mdogo Kanda ya Ziwa, wanawake hawapaswi kusema chochote kutokana na kuonekana hawawezi na hawaruhusiwi kuingia kwenye maduara kuchimba madini.

"Bado mwanamke hapewi nafasi inayostahili ili apate uwezo na kipato kwa maana ya mtaji ili aweze kufanya shughuli hizo ambapo anayefahamika ni mwenye mtaji kuliko yule anayefanya kazi kila siku," alisema.

Rubara alisema kitu kingine ambacho kimekuwa kizingiti kwa wanawake kujiendeleza katika sekta ya uchimbaji mdogo wa madini ni kutopata nafasi ya kujiendeleza kielimu.

Pia alisema mambo mengine yanayofanya wanawake kukosa fursa ni pamoja na uwepo wa sera ambazo haziwasaidi wanawake hivyo wakaomba kuwepo sheria za kuwawezesha.

# Wakulima wapewa pembejeo kuboresha kilimo

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

WAKULIMA vijana 71 kutoka kata 12 katika Halmashauri ya Manispaa ya Kahama mkoani Shinyanga, wenye uwezo wa kulima ekari tano na kuendelea za mazao ya chakula na biashara, wamepatiwa pembejeo za kilimo bure ili kuongeza uzalishaji na kujikwamua kiuchumi.

Utoaji wa pembejeo hizo ulianza kutolewa kwa vijana kuanzia mwaka wa fedha 2018/19 kwa lengo la kutengeneza ajira katika sekta ya kilimo na kuondoa wimbi la vijana mitaani. Mpaka sasa wakulima 172 wameshanufaika kwa kupata pembejeo zenye thamani ya Sh. milioni 115.7.

Ofisa Kilimo wa Manispaa ya Kahama, Richard Hegera, aliyabainisha hayo jana wakati akitoa taarifa ya ugawaji wa pembejeo za ruzuku kwa wakulima vijana na wakulima wa mfano walionufaika msimu uliopita.

Pembejeo hizo zilitolewa na halmashauri hiyo ili kuongeza uzalishaji wa mazao ya chakula na biashara kwa kata 12 za pembezoni.

Alisema kila mwaka wa fedha wamekuwa wakitenga fedha kupitia mapato ya ndani kwa ajili ya kununua pembejeo za kilimo na kuzigawa bure kwa wakulima vijana wenye uwezo wa kulima ekari tano na kuendelea na mazao wanayoyapata ni mali yao na si ya halmashauri.

Herege alisema wametoa mbolea mifuko 680, mbegu za mahindi bora kilo 1,500, mbegu za alizeti kilo 300 na lita 225 za viuatilifu kwa wakulima vijana 71 kati ya wakulima 312 walioomba kutoka kata 12 zenye thamani ya Sh. milioni 66.8 na jumla ya ekari 415 za mahindi, mpunga, alizeti na pamba zitalimwa.

Alizitaja kata hizo kuwa ni Isagehe, Iyenze, Mwendakulima, Wendele, Busoka, Kilago, Ngogwa, Zongomela, Kinaga, Nyandekwa, Mhongolo na Mhungula na watakuwa wakisimamiwa ipasavyo na maofisa ugani wa kila kata kwa ajili ya kuwapatia elimu ya namna ya kulima kisasa.

Naye Meya wa Manispaa hiyo, Yahaya Bundala, aliwataka wakulima hao kuacha tabia ya kuuza pembejeo hizo na kutumia fedha katika anasa kama vile ulevi na mambo mengine yasiyofaa na badala yake wajikite katika kilimo chenye tija na kujiongezea kipato.

Alisema, kabla ya serikali kuweka ruzuku, mbolea hizo zilikuwa zinauzwa Sh. 140,000 kwa mfuko fedha ambazo zilikuwa nyingi na wakulima wenye uwezo wa chini walishindwa kumudu gharama hizo.

Martha Mwandiki, mkulima kutoka Kata ya Mwendakulima, alisema pembejeo hizo zitawasaidia katika kulima kilimo chenye tija kwa kuwa awali walikuwa wakilima na kupata mazao machache kwa kutokuwa na uwezo wa kununua pembejeo na ametayarisha shamba la ukubwa wa ekari 20 na atalima mahindi tu.

## Mataifa maskini yaomba msaada COP27

**SHARM EL-SHEIKH, Misri**

MATAIFA maskini yametumia mkutano wa kimataifa wa mazingira wa COP27 kuzilaumu serikali za mataifa tajiri kwa kuchochea ongezeko la joto duniani, huku zikitaka kuongezewa ufadhili katika kupambana na hali ya ukame.

Mkutano huo wa wiki mbili wa Umoja wa Mataifa (UN) unaendelea katika mji wa mapumziko wa Sharm el-Sheikh nchini Misri.

Rais wa Senegal, Macky Sall, aliwaambia wajumbe wa mkutano huo kwamba mataifa yanayoendelea barani Afrika yanahitaji kuongezewa ufadhili kutoka mataifa tajiri ili kukabiliana na hali inayozidi kuwa mbaya ya mabadiliko ya tabianchi.

Rais wa Sri Lanka wakati huo, alisema serikali za magharibi zilichukuwa hatua za haraka kuhamishia fedha kwenye vita vya Ukraine, na kwamba zinajikongoja kwenye matumizi ya kukabiliana na tabianchi.

Naye Rais wa Afrika Kusini, Cyril Ramaphosa, aliwakosoa wafadhili wa kimataifa kwa kuyawekea ngumu mataifa maskini kupata msaada ili yahamie kwenye nishati safi zaidi.

Inaelezwa kuwa Afrika Kusini ambayo inategemea nishati ya makaa ya mawe kwa kiasi kikubwa, ni mmoja wa wachafuzi wakubwa zaidi wa mazingira duniani.

Kulingana na Benki ya Dunia, Afrika Kusini itahitaji walau dola bilioni 500 ili kufanikisha uondoaji wa gesi chafu kufikia mwaka 2050.

**DW**

# Chama cha Marubani Kenya chafuta notisi ya mgomo

**NAIROBI, Kenya**

CHAMA cha Marubani wa Ndege nchini Kenya (KALPA), kimefuta notisi yao ya mgomo kufuatia uamuzi wa awali wa mahakama ya ajira na mahusiano, ambayo iliwaamuru marubani hao kurejea kazini.

Katika taarifa ya KALPA, iliyotolewa usiku wa kuamkia Jumanne, ilieleza juu ya kusitishwa notisi yao ya mgomo na kuwataka wanachama wao warejee kazini jana kuanzia saa 12:00 asubuhi.

Chama hicho kilisema kinajutia usumbufu ambao wateja wamepitia na kuwataka wanachama wao kurejesha hali ya kawaida mara moja.

Marubani hao walianza mgomo huo katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Jomo Kenyatta Novemba tano, wakikaidi agizo la mahakama lililotolewa wiki jana dhidi ya hatua kama hiyo.

Hakimu wa Mahakama ya Mahusiano ya Kazi, Anna Mwaure, juzi aliamuru marubani wa Shirika la Ndege la Kenya Airways warejelee majukumu yao kama marubani bila masharti.

Pia ilielezwa kuwa Shirika la Ndege la Kenya Airways baadaye liliunga mkono uamuzi huo uliotolewa na mahakama.

Waziri wa Uchukuzi wa Kenya, Kipchumba Murkomen, alisema mgomo wa muda mrefu ungesababisha si tu kufungwa kwa shirika hilo ambalo lilikuwa likipoteza zaidi ya Sh. milioni 300 kwa siku, lakini kuathiri vibaya maisha ya zaidi ya watu 18,000 wanaotegemea shirika hilo.

Aidha, inaelezwa kuwa kesi iliyowasilishwa mahakamani na chama hicho cha marubani itaendelea kusikilizwa. ***VOA***



Wanajeshi zaidi ya 5,000 Ufaransa wakisalimiana na vijana baada ya kupelekwa katika eneo la Sahel kukabiliana na wapiganaji wa jihad. . **PICHA: VOA**

# Ukraine yaapa kutorudi nyuma

**KYIV, Ukraine**

RAIS wa Ukraine, Volodymyr Zelenskiy, amesema taifa lake halitaacha hata sentimita moja katika mapambano ya kudhibiti mkoa wa mashariki wa Donetsk, huku mawakala wa Urusi wakisema vikosi vya Ukraine vinaelekea kusini kwa vifaru.

Mkoa wa Donetsk ni moja ya mikoa minne ambayo Urusi ilidai kuinyakua mwishoni mwa mwezi Septemba.

Mapigano yamekuwa yakiendelea katika mkoa huo kati ya jeshi la Ukraine na vikosi vinavyoelemea Urusi tangu mwaka 2014, kipindi ambacho Moscow iliinyakua rasi ya Crimea kutoka Ukraine.

Rais Zelenskiy, alisema kwamba shughuli za vikosi vya uokoaji zinasaidia kwa kiwango cha juu, zikihusisha mashambulizi ya kila siku, huku akibainisha kuwa vikosi hivyo vya Urusi vinakumbwa na hasara kubwa.

"Amri inabaki ile ile kusonga mbele kuelekea mpaka wa utawala wa mkoa wa Donetsk, hatutaachia hata sentimita moja ya ardhi yetu," alisema Zelenskiy.

Pia aliwashukuru aliowaita mashujaa wote wanaosimama kidete kuitetea Donbas.

Meya aliyewekwa na Urusi katika mji wa Snihurivka, mashariki mwa mji wa kusini wa Mykolaiv, alinukuliwa na shirika la habari la RIA akisema kwamba wakazi waliona vifaru na mapigano makali yalikuwa yanaendelea.

Gavana wa Ukraine wa mkoa wa Mykolaiv Vitaly Kim, aliashiria kwamba vikosi vya Ukraine tayari vimewatimua wanajeshi wa Urusi kutoka eneo hilo, akinukuu kilichoonekana kuwa mazungumzo kati ya wanajeshi wa Urusi.

Kwenye uwanja wa mapigano mkoani Kherson, Zelenskiy alisema vikosi vya Ukraine vilikuwa vinachukuwa hatua kwa usahihi kutokana na uelewa wao wa mipango ya Urusi.

MILIONI 4 WAKOSA UMEME

Zelenskiy pia alieleza kuwa karibu watu milioni nne walikuwa hawana umeme katika mikoa 14, pamoja na mji mkuu wa Kyiv mwanzoni mwa wiki hii, na kwamba ni kwa msingi wa udhibiti na siyo dharura.

Inaelezwa kuwa vikosi vya Ukraine vimekuwa kwenye mashambulizi katika miezi ya karibuni, huku Urusi ikijipanga kutetea maeneo ya Ukraine inayoendelea kuyakalia, baada ya kuwaita maelfu ya askari wa akiba katika kipindi cha mwezi mmoja uliyopita.

Mchambuzi wa kijeshi mwenye makao yake mjini Kyiv, Oleh Zhdanov, alisema kwamba wanajeshi 21 wa Urusi walikuwa wamejisalimisha kwa vikosi vya Ukraine karibu na Svatove katika mkoa wa Luhansk.

Ukraine pia imeishtumu Urusi kwa kupora vifaa na kuharibu miundombinu ya nishati na barabara, wakati vikiondoka katika maeneo yanayorejeshwa na Ukraine.

Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa linatarajiwa kupiga kura wiki ijayo kuhusu azimio linalotambua kwamba Urusi inawajibika kuilipa Ukraine fidia, kutokana na majeraha, ikiwamo uharibifu wowote uliosababishwa na matendo yanayotambuliwa kuwa makosa kimataifa.

Robo tatu ya mataifa 193 wanachama wa Baraza Kuu ya Umoja wa Mataifa yalipiga kura mwezi Machi mwaka huu, kulaani uvamizi wa Urusi, na pia mwezi Oktoba walilaani jaribio la Moscow kunyakuwa baadhi ya maeneo ya Ukraine.

***DW***

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA CHETI



**GRANT BARAKAEL ANDERSON** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha sita chenye index namba **S0189-0544** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia **FEZA BOY'S SEKONDARY** mwaka 2018. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha Polisi. Taarifa ya Polisi: **DAR/OST/RB/436382/2022.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**SAMO CHARLES MASSARE,** Anatangaza kupotea kwa kadi ya Gari aina ya **TOYOTA HIACE** yenye usajili namba **T552 BES,** CHASIS NO **LH1821001684,** ENGINE NO **3L3928773.** Yeyote atakaeiona atoe taarifa Kituo chochote cha Polisi. TAARIFA YA POLISI: **DOD/MPW/RB/437075/2022**

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**MOHAMMED ENTREPRISES (T) LTD** anatangaza kupotea kwa kadi ya pikipiki aina ya **BOXER BM 125** yenye usajili namba **MC410 DCR ,** CHASSIS NAMBA: **MD2B15BX7MWF87245** na ENGINE NAMBA: **JVXWMF62187**. Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi . POLISI TAARIFA: **DAR/URA/RB/419260/2022**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**EVARIST THADEO KAPINGA**

ANATANGAZA KUPOTEA KWA KADI YA GARI YENYE NAMBA ZA USAJILI **T957BBR.**

KWA YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI KWA NAMBA - **ARU/ARU/RB/437179**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**HABIB S. MAHADHY** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya **TOYOTA ESTIMA** yenye usajili namba: **T ABC 315 ,** CHASSIS NAMBA: **CXR200105479** na ENGINE NAMBA: **3C812541.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: **WMB/RB/13032/2022**

---

**WIZARA YA ARDHI,NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI**

**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA WILAYA YA MASWA.**

**LILILOPO MASWA.**

**MAOMBI MADOGO NA.853 YA MWAKA 2022**
**(From the decision of Mwanghonoli Ward Tribunal land case No 2 of 2021)**

**KATI YA HAMIS LUCAS NHELE.............MLETA MAOMBI**

**DHIDI YA**

**MALULI LUGALILI MAYUNGA ............MJIBU MAOMBI**

**WITO/TAARIFA**

**Kwa: MALULI LUGALILI MAYUNGA POPOTE ALIPO KATIKA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA.**

Kwa kuwa mwombaji hapo juu amefungua Maombi dhidi yako katika Baraza hili la wilaya ya Maswa,maelezo ya madai yanaweza kupatika hapa Barazani.Unatakiwa kuleta hapa Barazani utetezi wako wa maandishi(WSD)kabla ya tarehe 08.12.2022.
Pia unajulishwa kuwa shauri hili limepangwa kutajwa siku ya tarehe 08.12.2022 saa 2;30 asubuhi mbele ya Mhe.J.T.Kaare Mwenyekiti,Baraza la Ardhi na Nyumba Wilaya-Maswa.
Na pia unafahamishwa kuwa iwapo utakadi wito huu na kushindwa kufika siku iliyopangwa,Baraza litalazimika kusikiliza Maombi haya upande mmoja na kutoa uamuzi dhidi yako.
IMETOLEWA kwa MKONO wangu na MHURI wa Baraza hili leo tarehe 08.11.2022

J.T.KAARE
MWENYEKITI
BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA (W)
MASWA

MWENYEKITI BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA YA MASWA TANZANIA

## TANZANIA TEACHERS UNION

Wanatangaza kupotolewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T. 752 DQG** aina ya **TOYOTA COSTAR** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi kilichopo karibu yake. Taarifa ya polisi. **KAH/TR/RB/740/2022.**

## MAGOTO HUDUMA COMPANY L.T.D

Wanatangaza kupotolewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T. 399 DVQ** yenye Engine No; **43195800438518,** Chassis No; **WDB9342332L498533** aina ya MERCEDS. Yeyote atakayeiona ataoe taarifa kituo cha polisi kilichopo jirani yake. Taarifa ya Polisi. **KAH/RB/746/2022.**

---

**MAHAKAMA YA ARHI NA NYUMBA YA WILAYA YA MBEYA**

**SHAURI No. 262/2020**

**HERMAN JOHN MPEMBWA(Msimamizi wa Mirathiya Marehemu JOHN MPEMBWA.................................MDAI**

**DHIDI YA**

**ERASTO MPEMBWA.............................................MDAIWA**
**FURAHA MUSSA MWASHAMBWA...........................MDAIWA**
**FRANK CHRISTOPHER DEO..................................MDAIWA**

**YAH: KUITWA SHAURINI**

**KWA: FRANK CHRISTOPHER DEO**

Fahamu kwamba HERMAN JOHN MPEMBWA amefungua Shauri dhidi yako katika Baraza hili.
Shauri limepangwa kwa ajili ya Hukumu tarehe 11/11/2022 saa 2.30 asubuhi mbele ya Mh.A.Mapunda Mwenyekiti wa Baraza. Unaamriwa kuhudhuria mbele ya Baraza siku hiyo bila kukosa wewe Mwenyewe au mwakilishi anayeruhusiwa kisheria.Ofisi za Baraza zipo ndani ya eneo la Sabasaba Mbeya mjini.

Tambua kwamba Shauri hili lilisikilizwa upande mmoja dhidi yako.

Amri hii imetolewa kwa mkono wangu na Lakiri/Muhuri wa Baraza hili leo tarehe 07/11/2022

A. Mapunda
MWENYEKITI
07/11/2022

CHAIRMAN DISTRICT LAND AND HOUSING TRIBUNAL Mbeya TANZANIA

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA WILAYA YA UBUNGO LILILOKO – LUGURUNI**

**SHAURI LA MADAI NAMBA 5 YA MWAKA 2017**

**VIOLETH J. MKOMWA NA BEDA A. MLANGWA.........MUOMBAJI**

**DHIDI YA**

1. **KELVIN MROPE**
2. **MICHAEL HASSAN MROPE...........MJIBU MAOMBI**

**KUITWA SHAURINI**
**KELVIN DAVID MROPE NA MICHAEL MROPE – POPOTE ULIPO/MLIPO**

**VIOLETH MKOMWA NA BEDA MLANGWA** amefungua shauri mbele ya Baraza la Ardhi na Nyumba (W) Ubungo lililopo Luguruni. Maombi yamepangwa kusomwa Hukumu tarehe 28/11/2022 saa 14:30 mchana. Hivyo basi unatakiwa wewe mwenyewe au Wakili wako afike siku hiyo bila kukosa. Endapo hautokuwepo/hamtakuwepo Hukumu itasomwa upande mmoja.
AMRI hii imetolewa kwa mkono na LAKIRI ya Baraza hili leo tarehe 09 Mwezi wa 11, 2022.

MWENYEKITI
BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA UBUNGO
DAR ES SALAAM

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**GODFREY AUGUSTINE MAINDE** Anatangaza kupotelewa kwa kadi za gari zenye usajili wa namba **T 402 ANV (MITSUBISHI CANTER) na T 984 AAV (MITSUBISHI FUSO).** Kwa yeyote atakayeziona au kuokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi au apige simu: **0714152193. MOR/MOR/RB/419872/2022.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**MOHAMMED ALI RASHID** Anatangaza kupotelewa kwa kadi ya gari yenye usajili wa namba **T354 DYZ.** Kwa yeyote atakaeiona au kuokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi. **DAR/KIL/RB/436062/2022.**

**OFISI ZA MATANGAZO**

**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**

**PO.BOX 31042,**

**DAR ES SALAAM.**

**MOB: +255 - 745 700 710.**

**E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com**

Kwa Habari Motomoto

usikose Gazeti lako

la Nipashe kila siku

Tupigie

0782253676

Nipashe MWANGA WA JAMII

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# NUH

## NA SABABU KUVAA NGUO ZA KIKE



**Na Mwandishi Wetu**

KATIKA hali isiyo ya kawaida Msanii wa Bongo Fleva, Nuh Mziwanda, amesema aliamua kuvaa nguo za kike na kupiga picha kuziweka kwenye mtandao kwa sababu ya kuvuta tu hisia za watu.

Akizungumza na kipindi cha Planet Bongo cha East Africa Redio, Nuh alisema sababu kubwa ilikuwa kuvuta hisia za watu si vingine.

"Nilikaa na nikawaza nikaamua kuvaa nguo za kike na kupiga picha na kuziweka mtandaoni na lengo ni kuvuta hisia za watu kuhusu EP yangu mpya ya Wonders," alisema Nuh.

Msanii huyo aliibua mjadala mkubwa kwenye mitandao ya kijamii kwa kuvaa nguo hizo za kike huku akionekana amejipodoa na wengi kuanza kumfikiria vibaya.

# NAY: MAMA ANATESEKA POLISI WAKINITAFUTA

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS wa kitaa na mtetezi wa wanyonge kama ambavyo anajiita mwenyewe, Nay wa Mitego, amesema mama yake mzazi anapata shida sana kutokana na misukosuko anayoipitia hasa kukiwa na taarifa za kutafutwa na polisi.

Nay ameomba mashabiki wake wamuombee mama yake hasa katika nyakati kama hizi.



Pia, amelaani wanaompelekea taarifa kama hizo mama yake.

"Nafanya kwa ajiili ya walala hoi wenzangu wasio na sehemu ya kusemea, ambao naamini bila wao nisingekuwa hapa," aliandika Nay kwenye ukurasa wake wa Instagram.

Aliongeza: "Lakini kuna shida kubwa anapata mama yangu hasa akisikia misukosuko ya kutafutwa na polisi pale ninapotoa nyimbo ambazo mamlaka haizielewi.

"Wimbo wangu wa 'Sauti ya Mtaa' umenipa misukosuko mingi kutafutwa polis'i," naamini yatakuwa tu."

# ETI TID HAMJUI ALI KIBA

**Na Mwandishi Wetu**

MSANII wa Bongo Fleva, Khalid Mohamed, maarufu TID, amesema hajawahi kukutana na Ali Kiba na wala hamjui kama ni Mwarabu au Mwafrika.

TID alitoa kioja hicho kwenye uzinduzi wa albamu ya Dimpoz inayokwenda kwa jina la Dedication ambapo mastaa mbalimbali wakubwa walihudhuria akiwamo Rais mstaafu, Jakaya Kikwete.

"Dimpoz ni kijana wangu nimekuwa naye kwa takriban miaka minne tukiimba naye kwenye bendi yangu, anajua kujiongeza kama unavyoona kwenye albamu amewashirikisha wasanii kama Jux na yule dogo Marioo.

"Agalia amemshirikisha Ali Kiba, sijawahi kukutana naye mimi kabisa. Nafikiri ni Mwarabu eeh," alisema TID.



# MABONDIA 30 WAPIMA AFYA KUZICHAPA DAR BOXING DERBY

**Na Saada Akida**

JUMLA ya mabondia 30 wamepima afya jana tayari kwa maandalizi ya mwisho kuelekea pambano la Dar Boxing Derby linalotarajiwa kufanyika Novemba 20, mwaka huu kwenye Uwanja wa Kinesi uliopo Urafiki, Dar es Salaam.

Mabondia watakaocheza pambano hilo ni pamoja na Ally Ngwando wa Manzese ambaye atacheza pambano kuu dhidi ya Ismail Boyka kutoka Gongo la Mboto, Dar es Salaam huku kiingilio kikiwa ni Sh. 5,000 kabla na Sh. 10,000 mlangoni huku kwa VIP kikiwa ni Sh. 15,000.

Wengine ni Karimu Mandonga ambaye amewataka mashabiki wa mchezo huo kujitokeza kwa wingi katika pambano hilo la Dar Boxing Derby huku akisisitiza kuwapo kwa ngumi yake ya ndoige siku hiyo.

"Tayari tumekamilisha zoezi la kupima afya kwa ajili ya maandalizi ya pambano la Dar Boxing Derby na jambo kubwa ni kuhamasisha wadogo zetu siku hiyo mashabiki wanataka kushuhudia ngumi hasa yaani watu wapigane na ngumi ndoige zionyeshwe," alisema Mandonga.

Mratibu wa pambano hilo, Bakari Khatibu, ameliambia gazeti hili jana kuwa wamekamilisha zoezi la kwanza kwa upimaji afya za mabondia kuelekea pambano hilo ambalo linasubiriwa kwa hamu na mashabiki wa mchezo huo.

"Tayari leo (jana), tukiwa kama waandaji tumekamilisha sehemu ya kwanza ya maandalizi kwa kuwapima afya mabondia wote kutokana na kanuni na sheria za mchezo wa ngumi za kulipwa hapa nchini.

"Kitu kikubwa ambacho tunataka kuwaambia mashabiki tukiwa kama waandaji ni kwamba, tumekuwa tukifanya mambo kwa utofauti mkubwa kwa sababu wasitegemee kuona Uwanja wa Kinesi kuwa unavyokuwa kwenye mapambano mengine, tumejipanga kuleta tofauti na hata wale ambao watakuwa wamekata tiketi za VIP basi watapata hadhi ya kuwa katika VIP," alisema Khatibu.

Kwa upande wa upande wa daktari aliyesimamia mchakato huo, Khadija Hamisi, alisema kawaida wamekuwa wakisimamia kuwapima magonjwa matatu kabla ya kupanda ulingoni ambayo ni homa ya ini, kisukuri na ukimwi.

Mabondia wengine watakaopanda ulingoni kwenye pambano hilo ni Gilbert Machupa dhidi ya Juma Kichupa, Joseph Maigwisa na Ibrahim Tamba huku Mudy Pesa akitarajia kucheza na Man Chuga wakati Yuko Kyando akipambana na Hemedi Rashid.

Wengine ni Vigulo Shafii dhidi ya Bakari Dunda, Hamad Furahisha dhidi ya Max Mushi, Paul Magesta akivaana na Haruna Ndaro, Emmanuel Kitimtim na Swahibu Ramadhan wakati Mshamu Mohamed atacheza na James Killian huku Peter Tosh akizichapa na Jackson Malinyingi.

**CHETI...**



Mwenyekiti wa Baraza la Michezo la Taifa (BMT), Leodgar Tenga (kushoto), akikabidhi cheti kwa mshiriki wa mafunzo ya walimu wa michezo wa shule 56, Vicent Yahya, baada ya kufunga mafunzo hayo jana, yaliyofanyika katika Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam. **PICHA: SAADA AKIDA**

## Polisi yaipeleka Simba Ushirika

**Na Adam Fungamwango**

BODI ya Ligi Kuu Tanzania (TPLB), imeufungulia Uwanja wa Ushirika uliopo mjini Moshi mkoani Kilimanjaro, kuendelea kutumika kwa michezo ya ligi baada ya kukaguliwa na kuthibitishwa na Kamati ya TFF ya Leseni ya Klabu.

Kutokana na kufunguliwa kwa uwanja huo, mechi ya Ligi Kuu kati ya Polisi Tanzania na Simba Novemba 27, mwaka huu sasa itapigwa kwenye uwanja huo.

Taarifa iliyotolewa jana na Idara ya Habari na Mawasiliano ya bodi hiyo, imeeleza uwanja huo umefunguliwa baada ya kufanyiwa maboresho kwenye maeneo yote muhimu ikiwamo eneo la kuchezea 'pitch', vyumba vya kuvalia na uzio unaotenganisha mashabiki na eneo la kuchezea.

Hata hivyo, imeeleza uwanja huo utaanza rasmi kutumika kuanzia Novemba 20, ikiwa ni siku 14 tangu ulipokaguliwa na Kamati ya Leseni za Klabu Novemba 5, mwaka huu.

Uwanja huo ambao ulikuwa unatumiwa na Polisi Tanzania kwenye mechi za Ligi Kuu msimu uliopita, haukuweza kutumika tangu kuanza kwa msimu huu, huku timu hiyo ikilazimika kutumia Uwanja wa Sheikh Amri Abeid kwenye mechi za mwanzo za msimu kabla nao haujapigwa kufuli kwa sababu zinazofanana na hizo.

Kwenye mechi iliyopita dhidi ya Singida Big Stars, Polisi Tanzania ililazimika kuipeleka kwenye Uwanja wa Black Rhino, Karatu Arusha Jumapili iliyopita na kuchapwa bao 1-0.

Pamoja na kufunguliwa uwanja huo, Novemba 20, ratiba inaonyesha kuwa Polisi Tanzania haitocheza mechi yoyote ya nyumbani, badala yake itakuwa ugenini Novemba 21 dhidi ya Mtibwa Sugar na itaanza rasmi kuutumia Novemba 27 itakapocheza dhidi ya Simba.

# Hitimana alia nyota wa3 kuikosa Geita Gold

**Na Shufaa Lyimo**

KOCHA Mkuu wa KMC FC, Thierry Hitimana, ameeleza kusikitishwa kwake kwa kuwakosa nyota wake watatu katika mchezo wao ujao dhidi ya Geita Gold utakaochezwa Novemba 11, mwaka huu mkoani Geita.

Akizungumza na gazeti hili jana, Hitimana aliwataja wachezaji watakaoukosa mchezo huo kuwa ni Awesu Awesu, Ibrahim Ame pamoja na Matheo Antony ambao wote ni majeruhi.

"Ninasikitika wachezaji wangu hao wana majeraha ambayo yananifanya nisiwe na uhakika kama wataweza kucheza au laa ila baadhi wanaendelea vizuri," alisema Hitimana.

Alisema baada ya kupoteza michezo miwilii mfululizo aliamua kutowapumzisha wachezaji wake ili kuzidi kuwajenga zaidi kuelekea michezo ijayo.

Akizungumzia kuhusu mechi mbili za kirafiki walizocheza jijini Mwanza, kocha huyo alisema imemsaidia kurekebisha baadhi ya makosa ya wachezaji wake ambayo waliyafanya kwenye michezo iliyopita.

"Mchezo wa kwanza wa kirafiki tulicheza na timu ya Mbao FC na kuwafunga mabao 7-2 na wa pili tulicheza jana (juzi) dhidi ya Pamba FC na kutoka sare ya kufungana mabao 2-2," alisema Hitimana.

Alisema jana walitarajia kuelekea mkoani Geita tayari kwa mchezo wao wa Ligi Kuu Bara dhidi ya Geita Gold, ambao alieza anatajia kuwa mgumu kwa kila upande hasa kutokana na ligi ilivyo kwa sasa.

KMC ipo nafasi ya tisa kwenye msimamo wa Ligi Kuu Bara ikiwa na pointi 13 sawa na Geita Gold inayoifuata nafasi ya 10, baada ya timu hizo kila moja kushuka dimbani mara 10, zikitofautiana tu kwa tofauti ya mabao ya kufunga na kufungwa.

Kabla ya mechi za jana kati ya Singida Big Stars dhidi ya Simba na Azam dhidi ya Dodoma Jiji FC, Yanga ndiyo iliyokuwa kileleni mwa msimamo wa ligi hiyo ikiwa na pointi 20 baada ya mechi nane huku watani wao hao wakifuata kwa alama 17. Azam na Singida Big Stars nazo zilikuwa na pointi 17 kabla ya mechi zao za jana, lakini zenyewe zikiwa mchezo mmoja mbele kutokana na kushuka dimbani mara tisa.

Ligi hiyo inatarajiwa kuendelea leo kwa kupigwa mchezo mmoja ambapo Tanzania Prisons itakuwa nyumbani kuikaribisha Coastal Union katika Uwanja wa Kumbukumbu ya Sokoine jijini Mbeya.

## ZISIKUPITE

### LLORIS ATAFUTIWA MRITHI

KLABU ya Tottenham Hotspur inatafuta mtu wa kuchukua nafasi ya mlinda mlango wa Ufaransa na nahodha wa klabu hiyo, Hugo Lloris mwenye umri wa miaka 35 msimu ujao. ***(TeamTalk)***

### DUBAI WAITAKA LIVERPOOL

Dubai International Capital ina nia ya kutaka kuinunua Liverpool licha ya kushindwa kukamilisha makubaliano wakati wa kujaribu kuinunua klabu hiyo mwaka wa 2007. ***(Arabian Business)***

### ENDRICK ATAKIWA CHELSEA

CHELSEA wamekutana mara kadhaa na mshambuliaji wa Palmeiras mwenye umri wa miaka 16, Endrick lakini wanakabiliwa na ushindani kutoka kwa Real Madrid na Paris St-Germain kuwania saini ya Mbrazil huyo. ***(Evening Standard)***

### CARRASCO LULU ULAYA

KLABU ya Newcastle inataka kumsajili mchezaji anayesakwa sana, Yannick Carrasco, Januari huku Atletico Madrid wakitarajiwa kumuuza winga huyo wa Ubelgiji mwenye umri wa miaka 29. ***(Mundo Deportivo - via Sport Witness)***

### EDWARDS AWANIWA SPURS

KLABU ya Tottenham Hotspur inamtaka kiungo wa kati wa Sporting Lisbon, Marcus Edwards mwenye umri wa miaka 23, ambaye aliwahi kuzichezea timu za vijana katika klabu hiyo ya London. ***(Record)***

### RATCLIFFE HAITAKI LIVERPOOL

BILIONEA wa England, Sir Jim Ratcliffe, amejiondoa katika mbio za kuinunua Klabu ya Liverpool akisema haioni tena thamani ya kununua timu hiyo ya Ligi Kuu ya England. ***(Telegraph)***

### SHAW ATAKIWA EVERTON

KOCHA wa Everton, Frank Lampard, ana nia ya kumleta beki wa kushoto wa Manchester United, Luke Shaw, pale Goodison Park, lakini mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 27, ana matumaini ya kuongezewa mkataba Old Trafford. ***(Football transfers)***

### MUDRYK KUTUA ARSENAL

WINGA wa Shakhtar Donetsk na Ukraine, Mykhaylo Mudryk, mwenye umri wa miaka 21, inasemekana amefanya mazungumzo chanya kuhusu kuhamia Arsenal katika dirisha la Januari. ***(Fabrizio Romano)***

### DIAZ AMULIKWA UNITED

KLABU ya Manchester United inamfuatilia mshambuliaji wa Blackburn na Chile, Ben Brereton Diaz, mwenye umri wa miaka 23, ingawa klabu nyingi za Ligi Kuu England zinataka kumnunua mchezaji huyo katika dirisha la Januari. ***(90Min)***

### DEPAY KUONDOKA JANUARI

MSHAMBULIAJI wa Barcelona, Memphis Depay mwenye umri wa miaka 28, anataka kuondoka katika klabu hiyo Januari, huku klabu za Manchester United na Tottenham zikifuatilia hali inavyokwenda kuhusu mchezaji huyo wa kimataifa wa Uholanzi. ***(Mundo Deportivo - via Express)***

### LIVERPOOL KWA ISAKSEN

LIVERPOOL wameripotiwa kutuma maskauti kumtazama winga wa Midtjylland raia wa Denmark, Gustav Isaksen, mwenye umri wa miaka 21, kwa nia ya kumsajili katika uhamisho wa Januari. ***(Extra Bladset via Express)***

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# MANE AZUA MSHTUKO KOMBE LA DUNIA QATAR

## Kocha asema amepata pigo kwenye kigimbi cha mguu, ni mahali pabaya, inabidi kwanza...

**MUNICH, Ujerumani**

SADIO Mane jana alifanyiwa vipimo vya X-ray baada ya kupata jeraha la kigimbi cha mguu wakati Bayern Munich ikishinda mabao 6-1 dhidi ya Werder Bremen juzi huku Kocha Mkuu Julian Nagelsmann akithibitisha.

Mshambuliaji huyo wa Senegal alichechemea dakika ya 20 kwenye Uwanja wa Allianz Arena, ambapo Serge Gnabry alipiga hat-trick huku viongozi wa Bundesliga wakisonga mbele kwa pointi nne kileleni.

Mane sasa anakabiliwa na kinyang'anyiro cha kuwa fiti kwa mechi ya ufunguzi ya Kombe la Dunia ya taifa lake dhidi ya Uholanzi Novemba 21, huku Bayern ikisubiri kufanyiwa vipimo zaidi ili kujua ameumia kwa kiasi gani.

"Alipata pigo kwenye kigimbi cha mguu," alisema Nagelsmann akiiambia Sky Sport. "Labda, lazima uende kwenye mashine ya X-ray na uone ikiwa kuna kitu hapo.

"Hapa ni mahali pabaya. Natumaini hakuna kitu, lakini sijui haswa."

Bayern walishinda mara tisa mfululizo, huku wakisawazisha rekodi ya klabu kwa kufunga mara nne au zaidi kwa mechi ya nne mfululizo ya ligi ya nyumbani.

Nagelsmann aliipongeza timu yake baada ya kufikisha jumla ya mabao 47 kwenye Bundesliga - zaidi ya timu yoyote katika ligi tano bora za Ulaya - ingawa alihisi ushindi ungekuwa mkubwa zaidi.

"Malengo ndiyo yanafanya soka kuvutia sana," aliongeza. "Baada ya mechi 14, tuna mabao 47 kwenye Bundesliga, hiyo ni ya kushangaza.

"Leo (juzi), tungeweza kufunga mengi zaidi. Tuna ubora mzuri uwanjani na roho nzuri. Tuko kimya sana, tulivu. Tumecheza mchezo mzuri kwa mashabiki."

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!

SUPA JACKPOT KWA 1000/- 1,048,8

MECHI KALI

MANCHESTER UTD
VERSUS
ASTON VILLA

1 | 1.64
X | 3.79
2 | 4.92

KUWEKA PESA:
- PIGA *150*87#,
CHAGUA 4
- WEKA PESA.

tigo pesa
vodacom m-pesa
airtel money
SEND

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#

GBT:0249
18+
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA:
0764115588, 0677115588
0685115588

@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# XAVI ALIA NA DROO YA EUROPA



**BARCELONA, Hispania**

KOCHA wa Klabu ya FC Barcelona, Xavi Hernandez, ameoneshwa kusikitishwa na droo ya michuano ya Ligi ya Europa baada ya kupangwa na Manchester United.

Barcelona walitolewa kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya na kushuka kwenye michuano ya Europa ikiwa ni mara ya pili baada ya msimu uliopita pia kushindwa kufuzu hatua ya 16-bora.

Barcelona chini ya Xavi msimu uliopita ilitolewa na Klabu ya Eincharcht Frankfurt kwenye hatua ya robo fainali ya michuano ya Ligi ya Europa na ndipo kocha wa klabu hiyo anaona mwaka huu pia wamekua wenye bahati mbaya kupangwa na Man United.

Kocha huyo anaamini wanahitaji kupambana na kuonyesha ubora wa hali ya juu kutokana na mpinzani ambaye wamepangwa naye chini ya Kocha Erik ten Hag

Barcelona mara ya mwisho kukutana na Man United ilikuwa hatua ya robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu wa 2018/19 aMbapo waliitoa kwenye michuano hiyo.

Mchezo mwingine ambao kocha Xavi alikuwa pia mchezaji ilikuwa fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya mwaka 2011 ambapo Barcelona walifanikiwa kushinda mabao 3-1 uliopigwa katika Uwanja wa Wembley.

# Phillips matumaini kibao kwenda Qatar

**LONDON, England**

KIUNGO wa Manchester City na Timu ya Taifa ya England, Kalvin Phillips, amejawa na matumaini kibao kabla ya kutajwa kwa kikosi cha England kitakachoiwakilisha nchi hiyo kwenye michuano ya Kombe la Dunia nchini Qatar.

Kiungo huyo ambaye amekuwa akisumbuliwa na majeraha ya bega baada ya kufanyiwa upasuaji wiki kadhaa nyuma, sasa ameshareje mazoezini hivyo anaamini anaweza kufanikiwa kuitwa kwenye kikosi cha Kocha, Gareth Southgate.

Phillips aliyehamia Man City akitokea Leeds United majira ya joto yaliyopita, amekuwa akisumbuliwa na majeraha mara kwa mara huku mpaka sasa akiwa amecheza michezo 14 pekee kwenye michuano yote klabuni hapo.

Jana Phillips alikuwa miongoni mwa wachezaji waliopo kwenye kikosi katika mchezo wa kombe la Carabao.

Bado kiungo huyo ana imani ya kuitwa kwenye kikosi cha England japo pia hana uhakika sana kutokana na kukaa nje ya uwanja kwa muda mrefu.

Lakini wadau wengi wa soka na timu hiyo ya taifa wanaamini nafasi ya kiungo huyo bado ipo kutokana na kiwango alichokionyesha kwenye michuano ya Euro 2020.



875,802/-

# MVUVI KIGAMBONI AJISHINDIA MILIONI 4.9/- BONUS SPORTPESA

**Na Mwandishi Wetu**

MVUVI kutoka Kata ya Pembamnazi, maarufu Kigamboni Buyuni kwa Morris, amejishindia Sh. 4,940,242 katika Jackpot Bonus ya SportPesa ya katikati ya wiki iliyopita, baada ya kupatia kwa usahihi mechi 12 kati ya 13.

Akizungumza na mwandishi wetu baada ya kukabidhiwa hundi yake jana, Joseph alisema alianza kucheza na SportPesa miaka mitatu iliyopita baada ya kuona washindi ambao walikuwa wanatangazwa kupitia magazeti na hivyo kumfanya aamini kama akiamua na yeye siku moja anaweza kuwa mmoja wa washindi.

"Mimi ni mmoja wa watu ambao wanapenda kusoma sana magazeti, wakati ule wa mwaka 2019, nilipata kuona washindi wa michezo hii ya kubashiri wakitangazwa kwenye haya magazeti, hapo ndipo hamu ilinijia na mimi nijifunze kucheza," alisema.

Kuhusu SportPesa, Joseph anasema alivutiwa na viwango vya dau la ushindi ambavyo vimekuwa vinawekwa kwenye Jackpot.

"Naomba niseme mimi ni mchezaji mkubwa wa Jackpot. Nacheza hizi Jackpot mara nyingi kuliko multibet. Hii imetokana na kwamba dau la Jackpot mara zote lilikuwa linaanzia Sh 200,000,000 ambapo lilikuwa linapanda mpaka kufikia kiwango cha juu cha zaidi ya bilioni moja ambacho alishinda yule Florian Massawe."

Joseph alisema staili yake ya kucheza na kuweka mikeka huwa anaweka mitatu ama minne kila anapokuwa anaamua kubashiri Jackpot za SportPesa.

"Mimi huwa kila mwanzo wa wiki nikishaziona mechi huwa natumia siku kadhaa kuzitathmini timu. Baada ya hapo huwa na kawaida ya kuweka timu nne au saa nyingine naweka tatu kila jioni inapofika mpaka mechi zote zinaisha na kisha nafuatilia matokeo taratibu mpaka mechi ya mwisho," alifafanua na kuongeza.

"Katika kucheza kwangu, kwenye hii miaka mitatu, nimeshawahi kushinda viwango tofauti tofauti mara tano kabla ya ushindi huu ambapo kiwango cha juu kilikuwa Sh. 2,600,000. Katika mkeka huu nilioshinda nilikosa mechi ya Sporting Lisbon dhidi ya Frankfurt, hivyo kupata bonasi ya timu 12."

Meneja Uhusiano na Mawasiliano wa Sportpesa, Sabrina Msuya, amewataka Watanzania kuendelea kuiamini SportPesa, kwani sasa hivi kuna vitu vingi vilivyoboreshwa ikiwemo idadi ya mechi na masoko.

"Niwaombe tu wateja wetu na wapenda michezo muendelee kucheza kwa wingi na kujaribu bahati zenu kupitia Jackpot zetu hizi na pia Multibet na michezo ya Kasino". Wiki hii Jackpot imesimamia Sh. 396,445,790.




Mshindi wa Jackpot Bonus, Joseph Omary akionyesha mfano wa hundi ya Sh. 4,940,242 baada ya kubashiri kwa usahihi mechi 12 kati ya 13 kwenye Jackpot ya SportPesa wiki iliyopita. Supa Jackpot kwa wiki hii ni Sh. 1,048,875,802. **MPIGAPICHA WETU**

# KITENGE, PONELA WAMPASUA KICHWA MAYANGA LIGI KUU

**Na Hadija Mngwai**

NYOTA wa Mtibwa Sugar, Pascal Kitenge na Kasian Ponela, wanampasua kichwa kocha wa timu hiyo, Salumu Mayanga, kutokana na kutarajia kuwakosa katika mchezo dhidi ya Azam FC utakaopigwa keshokutwa, Jumamosi.

Kitenge ambaye ni 'kiraka' katika timu hiyo huku Ponela akicheza nafasi ya ulinzi hawatocheza mchezo kutokana na kuwa nje ya uwanja wakitumikia adhabu ya kadi.

Akizungumza na Nipashe jana, Ofisa Habari wa Mtibwa Sugar, Thobiasi Kifaru, alisema kwa sasa Kocha Mayanga yupo katika mkakati wa kusaka mbadala wa Kitenge na Ponela ili kikosi chake kisipate mtikisiko katika mechi hiyo watakaokuwa nyumbani.

" Katika mchezo wetu uliopita wachezaji wetu wawili Kitenge na Ponela walipata kadi nyekundu hivyo hawatoweza kucheza mchezo wetu unaofuata dhidi ya Azam FC.

"Kocha Mayanga yupo katika mchakato wa kusaka wachezaji watakaoweza kuziba nafasi zao ili kuwa na kikosi imara.

"Kipa wetu Farouk Shikalo aliyeumia katika mechi dhidi ya Simba na kubadilishwa kwa sasa yupo fiti na anaweza kuwa miongoni mwa wachezaji watakaoivaa Azam," alisema Kifaru.

Aidha, akizungumzia kuelekea mchezo huo alisema kuwa morali ya wachezaji ipo juu kuhakikisha wanafanikiwa kuibuka na pointi tatu ili kuondoa machungu ya kufungwa mabao matano dhidi ya Simba.

"Wachezaji wapo vizuri kuelekea mchezo huo, tunajiandaa kushinda licha ya kucheza ugenini," alisema.


SUPA JACKPOT
MECHI WIKI HII
BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 12/11/22 | 18:00 | Nottingham vs Crystal Palace | 3.04 | 3.19 | 2.37 |
| 02. 12/11/22 | 18:00 | Bristol City vs Watford | 2.89 | 3.39 | 2.36 |
| 03. 12/11/22 | 18:00 | Bournemouth vs Everton | 2.78 | 3.23 | 2.53 |
| 04. 12/11/22 | 18:00 | Huddersfield vs Swansea | 2.80 | 3.25 | 2.50 |
| 05. 12/11/22 | 18:00 | Preston vs Millwall | 2.41 | 3.13 | 3.03 |
| 06. 12/11/22 | 18:00 | Coventry vs QPR | 2.36 | 3.22 | 3.02 |
| 07. 12/11/22 | 20:00 | Basaksehir vs Galatasaray | 2.42 | 3.40 | 2.80 |
| 08. 12/11/22 | 20:00 | Sampdoria vs Lecce | 2.54 | 3.08 | 2.89 |
| 09. 12/11/22 | 20:00 | FC Sion vs St. Gallen | 2.80 | 3.60 | 2.37 |
| 10. 12/11/22 | 20:30 | Newcastle vs Chelsea | 2.32 | 3.34 | 2.99 |
| 11. 12/11/22 | 22:45 | Bologna vs Sassuolo | 2.38 | 3.34 | 2.89 |
| 12. 13/11/22 | 14:30 | Atalanta vs Inter | 2.90 | 3.54 | 2.29 |
| 13. 13/11/22 | 16:15 | FC Zurich vs Servette Geneva | 2.37 | 3.30 | 2.95 |
| 14. 13/11/22 | 17:00 | Istanbulspor vs Hatayspor | 2.58 | 3.22 | 2.73 |
| 15. 13/11/22 | 17:00 | Kayserispor vs Konyaspor | 2.58 | 3.28 | 2.68 |
| 16. 13/11/22 | 17:00 | Montpellier vs Reims | 2.45 | 3.38 | 2.73 |
| 17. 13/11/22 | 17:30 | Mainz vs Eintracht Frankfurt | 2.44 | 3.41 | 2.72 |

MECHI ZA USHINDI
"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE "2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

ALHAMISI - 10/11/2022

| MUDA | GAME ID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 13:00 | 2262 | Istanbulspor vs Etimesgut BS | 1.20 | 6.23 | 9.54 |
| 14:00 | 1660 | Goeztepe vs Tire 1922 | 1.84 | 3.36 | 3.85 |
| 14:00 | 2155 | FC Minaj vs Chernomorets Odessa | 2.27 | 3.16 | 2.92 |
| 14:00 | 3664 | Belenenses vs AD Machico | 1.22 | 5.41 | 10.63 |
| 14:00 | 3923 | Tuzlaspor vs Isparta 32 Spor | 1.40 | 4.39 | 6.24 |
| 15:00 | 1594 | KF Gjilani vs KF Drita | 3.21 | 3.16 | 2.12 |
| 15:00 | 2680 | Saudi Arabia vs Panama | 2.04 | 3.28 | 3.78 |
| 15:00 | 4175 | KF Ballkani vs KF Llapi | 1.53 | 4.00 | 5.07 |
| 15:00 | 5626 | Caykur Rizespor vs Kirklarelispor | 1.27 | 5.27 | 8.20 |
| 15:00 | 5925 | FCM Alexandria vs Universitatea Cluj | 5.66 | 4.00 | 1.48 |
| 16:00 | 1019 | Saint George FC vs Wolkite City FC | 1.28 | 4.68 | 9.74 |
| 16:00 | 2808 | Tanzania Prisons vs Coastal Union | 2.31 | 2.66 | 3.44 |
| 16:00 | 4257 | Dynamo Kiev vs Oleksandria | 1.61 | 3.84 | 4.56 |
| 16:00 | 5377 | Ararat Armenia vs Pyunik Yerevan | 2.06 | 3.11 | 3.40 |
| 16:00 | 5903 | Charlton U23 vs Cardiff City U21 | 2.19 | 4.80 | 2.45 |
| 16:30 | 2576 | ES Metlaoui vs EO Sidi Bouzid | 3.64 | 3.30 | 1.91 |
| 16:30 | 5144 | Club A Bizertin vs ES Sahel | 3.70 | 2.80 | 2.25 |
| 17:00 | 2112 | Dinamo Tbilisi vs FC Telavi | 1.34 | 4.18 | 8.74 |
| 17:00 | 4026 | U Craiova SA vs Voluntari | 2.36 | 3.00 | 2.91 |
| 17:00 | 5026 | ATK Mohun Bagan vs Northeast United FC | 1.19 | 6.04 | 10.72 |
| 17:00 | 5115 | Denizlispor vs Sanliurfaspor | 2.58 | 2.96 | 2.67 |
| 17:25 | 2722 | AL Nasr vs AL Tadamon | 1.80 | 3.60 | 4.20 |
| 18:30 | 5387 | Partizan vs Spartak Subotica | 1.11 | 7.40 | 15.58 |
| 19:00 | 1816 | Fatih Karagumruk vs Kirsehir Belediye Spor | 1.07 | 8.93 | 19.41 |
| 19:00 | 4805 | Dire Dawa Kenema FC vs Mekelakeya | 3.27 | 2.83 | 2.27 |
| 19:15 | 2522 | CSC Dumbravita vs CFR Cluj | 18.47 | 7.39 | 1.10 |
| 19:30 | 4116 | Viborg FF vs Midtjylland | 2.41 | 3.36 | 2.58 |
| 20:00 | 2412 | Pafos FC vs Anorthosis Famagusta | 1.95 | 3.35 | 3.85 |
| 20:00 | 4409 | Volos vs PAS Giannina | 1.70 | 3.62 | 4.76 |
| 20:30 | 2739 | Verona vs Juventus | 4.72 | 3.55 | 1.71 |
| 20:45 | 1808 | Cukaricki St vs Red Star Belgrade | 7.19 | 4.76 | 1.33 |
| 21:00 | 2260 | Sandvikens IF vs Orgryte IS | 2.34 | 3.53 | 2.87 |
| 21:00 | 2267 | Budapest Honved vs Vasas SC | 2.09 | 3.30 | 3.15 |
| 21:00 | 3970 | Kayserispor vs Sivas Dort Eylul | 1.01 | 12.67 | 29.23 |
| 21:00 | 4204 | Osters IF vs Varbergs Bois | 2.43 | 3.11 | 2.72 |
| 21:00 | 4767 | Falkenbergs vs Ostersunds | 2.29 | 3.63 | 2.87 |
| 21:00 | 5554 | Rayo Vallecano vs Celta Vigo | 2.15 | 3.21 | 3.41 |
| 21:30 | 4757 | Aarhus vs Nordsjalland | 2.33 | 3.30 | 2.72 |
| 22:00 | 2800 | Valencia vs Betis | 2.13 | 3.30 | 3.35 |
| 22:00 | 4537 | RS Waasland Beveren vs Royal Antwerp | 3.94 | 3.70 | 1.78 |
| 22:00 | 5042 | FC Otelul Galati vs Steaua Bucuresti | 3.90 | 3.32 | 1.84 |
| 22:00 | 5666 | Racing White Daring Molenbeek vs Kortrijk | 2.67 | 3.46 | 2.37 |
| 22:00 | 5900 | Feyenoord vs Cambuur | 1.19 | 6.53 | 11.87 |
| 22:30 | 1818 | Magdeburg vs SV Darmstadt | 3.22 | 3.52 | 2.06 |
| 22:30 | 4594 | Ionikos Nikea FC vs PAOK | 4.99 | 3.54 | 1.69 |
| 22:45 | 1705 | Sporting Braga vs Moreirense | 1.21 | 5.64 | 10.70 |
| 22:45 | 1927 | KFC Oosterzonen vs Anderlecht | 5.72 | 4.54 | 1.45 |
| 22:45 | 4199 | Lazio vs Monza | 1.58 | 4.06 | 4.95 |
| 23:00 | 3436 | Manchester Utd vs Aston Villa | 1.64 | 3.79 | 4.92 |
| 23:30 | 4501 | Real Madrid vs Cadiz CF | 1.15 | 7.43 | 16.07 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

Michezo
Alhamisi Novemba 10, 2022
Nipashe



UKURASA 29

**Mane azua mshtuko Kombe la Dunia Qatar**

# SIMBA YASHINDWA KUISHUSHA YANGA

●●● Kucheza na jukwaa kwa Inonga kwaigharimu huku Kibu akiikosesha...

**Na Adam Fungamwango**

MABAO ya winga wa zamani wa Yanga, Deus Kaseke, kipindi cha kwanza na Mmalawi Peter Banda kipindi cha pili, jana yaliifanya mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara kati ya Singida Big Stars na Simba kumalizika kwa sare ya bao 1-1 kwenye Uwanja wa Liti mkoani Singida, kila timu ikifikisha sare ya tatu na pointi 18.

Simba ambayo ilikuwa na pointi 17, imeshindwa kuishusha Yanga kileleni ambayo haikucheza mechi yoyote ya ligi jana, huku ikiwa na pointi 20 ambapo kama ingepata ushindi ingepata idadi hiyo ya pointi na kukaa kileleni kwani ina idadi kubwa ya mabao ya kufunga.

Kaseke aliifungia Singida Big Stars bao dakika ya 11 tu ya mchezo kutokana na uzembe wa beki Henock Inonga.

Beki huyo wa kati alileta mbwembwe kwenye eneo la hatari, akanyang'anywa mpira na Shafiq Batambuze ambaye aliimimina majalo iliyomkuta mchezaji wa zamani wa timu hiyo, Said Ndemla, akaiweka kwa Kaseke ambaye alinyoosha mguu, mpira ukagonga na kujaa wavuni.

Banda aliyeingia kipindi cha pili kuchukua nafasi ya Jonas Mkude na kuleta mabadiliko makubwa ya uchezaji kwenye kikosi, aliisawazishia Simba dakika ya 58.

Banda aliuchukua mpira kwenye winga wa kushoto akammegea pande Mzamiru Yassin ambaye naye alimrudishia, kabla ya kuondoka nao kwa kasi na kuingia nao hadi ndani ya eneo la hatari.

Wakati kipa Khomainy Abobakar akidhani atapiga krosi kwa Denis Kibu, hivyo kusogea kidogo mbele ya lango kabla ya Banda kuupiga kiufundi mpira ulioonekana kuwa krosi, lakini ukakatika na kujaa wavuni.

Mechi hiyo ilianza kwa kasi, dakika ya pili ya mchezo na kama Pape Sakho angekuwa na utulivu angeweza kuipatia Simba bao, alipomvisha kanzu kipa Aboubakar, lakini badala ya kuuwahi mbele, alijikanganya mwenyewe na mabeki wa Singida Big Stars wakaufagia mpira huo kwenye eneo la hatari.

Moses Phiri aliyekuwa chini ya uangalizi wa mabeki wawili, Abdulmajid Mangalo na Mkongomani Biemes Carno, aliunganisha vibaya mpira wa krosi ya Shomari Kapombe na kuikosesha Simba bao la wazi dakika ya saba.

Baada ya kufunga bao dakika ya 11, ilionekana kama wachezaji wa Simba walipoteana na kuwafanya Singida Big Star kutandaza kandanda safi kwa dakika 10 zilizofuata, ambapo baada ya hapo wakaamua kupaki basi kulinda bao lao.

Wekundu wa Msimbazi wangeweza kusawazisha bao dakika ya 22 kama kichwa cha Phiri kisingegonga mwamba. Mpira huo ulitokana na faulo ya Kapombe.

Kipa Aboubakar alifanya kazi ya ziada dakika ya 32 alipopangua kwa ustadi mpira wa faulo iliyopigwa na Mohamed Hussein 'Tshabalala'.

Kuingia kwa Banda kulileta mabadiliko makubwa na kama wachezaji wa Simba wangetulia au kuwa na ubunifu wangeweza kupata mabao mengi.

Ni wazi kukosekana kwa Clatous Chama na Augustine Okrah kumeonekana kuiathiri timu hiyo kwani wachezaji kama Sakho na Kibu Denis walishindwa kuvaa viatu vya ipasavyo.

Kibu alikosa mabao mengi ya wazi kiasi cha kocha Juma Mgunda kuamua kumtoa na kumuingiza Habib Kyombo, lakini dakika zilikuwa zimeshasonga mbele.

**CHEKECHA...**





Mshambuliaji wa Simba, Pape Sakho akipiga hesabu za 'kumchekecha' kiungo wa Singida Big Stars, Shafik Batambuze, kwenye mechi ya Ligi Kuu Bara iliyopigwa Uwanja wa Liti mkoani Singida jana na kumalizika kwa sare ya bao 1-1. **PICHA: SIMBA**

## Simba Queens kuoga mil. 400/-

**Na Somoe Ng'itu, RABAT**

WACHEZAJI wa Simba Queens, wameahidiwa kupewa kiasi cha Sh. milioni 400 endapo watafanikiwa kutwaa ubingwa wa Ligi ya Mabingwa Afrika kwa Wanawake katika mashindano hayo yanayoendelea nchini Morocco wakati jana usiku walikuwa na kibarua kigumu dhidi ya mabingwa watetezi, Mamelodi Sundowns Ladies ya Afrika Kusini kwenye mechi ya nusu fainali.

Ahadi hiyo imetolewa na Ofisa Mtendaji Mkuu wa Simba, Barbara Gonzalez, jana asubuhi alipokuwa akizungumza na wachezaji wa timu hiyo kuelekea mechi ya nusu fainali ya jana usiku katika michuano hiyo itakayomalizika Jumapili.

Barbara alisema kama Simba Queens itashindwa kubeba ubingwa, basi itapata kiasi cha Sh. milioni 250 endapo tu itafanikiwa kutinga hatua ya fainali na anaamini kikosi hicho kina uwezo huo.

"Naomba niwaambie hapa tumeshafuta ile ahadi ya awali, naomba msahau kuhusu Sh. milioni 100, sasa hivi naomba mfikirie ubingwa, sisi ni 'Unstoppable'," alisema Barbara.

Kiongozi huyo aliongeza kuwa anahitaji kuona wachezaji wanaongeza juhudi katika mechi zilizobaki kwa sababu wao ni moja ya timu nne bora za wanawake barani Afrika.

Aliwaambia macho ya Watanzania na mataifa mengine mbalimbali ya Afrika yanawatizama Simba Queens kutokana na kiwango walichokionyesha katika mechi zilizotangulia na amewataka waendelee kuwashangaza wote wanaowafuatilia.

Naye Mjumbe wa Bodi ya Wakurugenzi wa Simba, Asha Baraka, alisema anajua kila mchezo wana uwezo wa kupambana na kusaidia timu ifike malengo na wakati wa kuitangaza vema nchi na vipaji vyao umefika.

"Kwanza tulikuwa tunaomba tufike nusu fainali, tumefika, lakini binadamu ukiomba 10 ukapata, unaanza kuhitaji kupewa 15, ndio sisi sasa tunataka kikombe," Asha aliongeza.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042
9 770856 541002 >